# Mwanzo wa Mifarakano Ndani ya Islam

Na

Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad

Khalifatul Masihi II

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Mwanzo wa Mifarakano Ndani ya Islam

*Islam Mein Ikhtilaafaat Kaa Aaghaaz*
(Swahili Translation)

Tafsiri ya Kiswahili ya: *Islam Mein Ikhtilaafaat Kaa Aaghaaz* (Kiurdu)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad[ra]
Khalifatul Masihi II

**Mfasiri:**
Sheikh Bakri Abedi Kaluta
Sheikh Asif Mahmood Butt

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1919
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2020

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031
Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-529-3
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# Faharisi

**Neno la Mwenezi** ........ vii
**Haja ya Kuielewa Historia ya Kiislamu** ........ 1
Umuhimu wa Madhumuni ........ 2
Wakati Uliopita Wenye Shani wa Islam ........ 3
Waja wa Kwanza waliojitolea kwa Islam — Hadhrat Uthman[ra] na Hadhrat Ali[ra] ........ 5
Maelezo potofu ya wanahistoria wasio Waislamu ........ 5
Masahaba[ra] Hawakuwa Chanzo cha Fitina Ndani ya Islam ........ 6
Kwa nini hitilafu zilitokea katika zama za Khalifa wa Tatu? ........ 9
Habari za mwanzoni za Hadhrat Uthman[ra] ........ 9
Cheo cha Hadhrat Uthman[ra] Machoni mwa Mtume[saw] ........ 11
Fitina Ilizukia Wapi? ........ 12
Sababu Nne za Fitina ........ 14
Ukhalifa wa Kiislamu Ulikuwa ni Nidhamu ya Kidini ........ 16
Hakukuwa na Sababu ya Kuwadhania Vibaya Masahaba[ra] ........ 19
Kwa Nini Fitina Iliibuka Wakati wa Hadhrat Uthman[ra]? ........ 26
Kuteuliwa kwa Abu Musa Ash'ari[as] kuwa Mtawala wa Kufa ........ 82
Kufichuka kwa hila za Wafisadi ........ 83
Ni Lazima Kumtii Mtawala wa Zama ........ 86
Njama Nyingine Zaidi ya Wafisadi ........ 87
Kufichuka kwa Njama ........ 89
Hadhrat Uthman[ra] Awaita Waasi ........ 89
Hadhrat Uthman[ra] Kujithibitisha kutokuwa na hatia ........ 90
Hadhrat Uthman[ra] Kuwahurumia Wafisadi ........ 92
Njama nyingine kubwa ya Wafisadi ........ 95
Waasi Kuwasili Madina ........ 97
Watu wa Misri Kumwendea Hadhrat Ali[ra] ........ 100
Watu wa Kufa Kumwendea Hadhrat Zubair[ra] ........ 101
Watu wa Basra Kumwendea Hadhrat Talha[ra] ........ 101
Kuteuliwa kwa Muhammad bin Abi Bakr kuwa Mtawala wa Misri ........ 101
Uhakika wa Tofauti za Riwaya ........ 102
Kanuni ya Asili ya Kusahihisha Historia ........ 103

Kutokuwa na Hatia kwa Hadhrat Uthman[ra] na Masahaba[ra] Wengine ..... 104
Waasi Kuingia Tena Madina ..... 104
Watu wa Madina Kuwafahamisha Waasi ..... 106
Waasi Kuudhibiti Madina ..... 107
Masahaba[ra] Wakubwa Wawauliza Waasi Sababu ya Kurejea Kwao ..... 107
Hadhrat Uthman[ra] Kuwathibitishia Waasi kujitoa katika Shutuma yao ..... 109
Uhakika wa Njama ya Waasi ..... 110
Dalili Saba za Kuthibitisha Njama ya Barua ..... 112
Waasi Wawanyanyasa Watu wa Madina ..... 122
Nasaha za Hadhrat Uthman[ra] kwa Waasi ..... 123
Waasi Wavunja Fimbo ya Mtume[saw] ..... 124
Waasi Wapiga Changarawe Msikitini Mwa Mtume[saw] na Kumjeruhi Hadhrat Uthman[ra] ..... 125
Masahaba[ra] Wawa Tayari Kupigana Vita na Waasi ..... 126
Wenzi Wakubwa Watatu wa Waasi ..... 128
Ndani ya Madina ..... 128
Hadhrat Uthman[ra] Alazimishwa Kujiuzulu Ukhalifa ..... 130
Kuzingirwa kwa Nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] ..... 131
Hadhrat Ali[ra] Awanasihi Wazingiraji ..... 133
Waasi Walivyomtendea Hadhrat Ummi Habiba[ra] ..... 134
Mfano wa Ghera ya Kidini wa Hadhrat Ummi Habiba[ra] ..... 135
Hadhrat Aisha[ra] Ajitayarisha Kwenda Kuhiji ..... 136
Hadhrat Uthman[ra] Awaandikia Barua Watawala wa Mikoa ..... 137
Barua ya Hadhrat Uthman[ra] kwa Mahujaji ..... 138
Waasi Watupa Mawe Ndani ya Nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] ..... 141
Juhudi Nzuri za Masahaba[ra] za Kuiondoa Fitina ..... 142
Waasi Waishambulia Nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] ..... 147
Hadhrat Uthman[ra] Awausia Masahaba[ra] ..... 147
Kurejea kwa Mahujaji Kwawatia Hofu Waasi ..... 150
Masahaba[ra] Wapigana na Waasi ..... 152
Abdullah bin Salaam[ra] Awanasihi Waasi ..... 155
Waasi Wamuua Hadhrat Uthman[ra] ..... 157

Matukio Ya Kuuawa Shahidi kwa Hadhrat Uthman[ra]............158
Waasi Waipora Baitul Maal — Hazina.......................................162
Masahaba[ra] Wahamaki kwa Kifo cha Hadhrat Uthman[ra].......163
Muhtasari na Matokeo ya Matukio Yaliyotajwa.......................165

# NENO LA MWENEZI

Kitabu kilicho mikononi mwenu — 'Mwanzo wa Mifarakano Ndani ya Islam' — kwa hakika ni hotuba ya Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad[ra], Khalifa wa Pili wa Hadhrat Masihi Mau'udi[as], aliyoitoa alipokaribishwa na Martin Historical Society ya Islamia College Lahore, mnamo 26 Februari 1919.

Hotuba hii ilitolewa ndani ya Ukumbi wa Habibiyya, chini ya uenyekiti wa Seyid Abdul Qadir ambaye ni mwanahistoria maarufu — ambaye si Mwahmadiyya. Katika hotuba fupi ya uzinduzi mheshimiwa mwenyekiti alisema:

> "Msemaji wa leo ni mtu mwenye heshima na umaarufu na daraja kubwa hata kwamba sifikirii kuna mtu asiyemjua. Yu mwana wa yule mtu mtukufu mwenye shani adhimu aliyetikisisha ulimwengu wa Kikristo."

Hotuba hii ilisikilizwa kwa shauku na makini sana. Baada ya hotuba, mwenyekiti mheshimiwa akasema katika maneno yake ya kufungia kikao:

> "Waheshimiwa, mimi nami mimewahi kuzitupia macho kusara za historia, na nilipofika jioni ya leo hii ukumbini humu nilikuwa nafikiri kuwa mie pia naelewa sehemu kubwa ya historia ya Kiislamu, nami naweza kutoa maoni na rai yangu kuhusikana na elimu

> hii. Lakini sasa baada ya hotuba ya Jenabu Mirza Sahib yaonekana mimi bado ni mwanafunzi wa shule. Mwanga wa ujuzi wangu mbele ya mwanga wa ujuzi wa Jenabu Mirza Sahib ni kama mwanga wa hii (akiashiria kwenye taa iliyokuwa imewekwa mezani) na mwanga wa ile taa ya umeme (akiashiria juu kwa kidole kwenye ile taa). Waheshimiwa, jinsi Jenabu Mirza Sahib alivyotia mwanga kwenye sehemu ngumu ya historia ya Kiislamu kwa ufasaha na utaalamu, hii ndiyo hadhi yake tu."

Baada ya mwaka mmoja hotuba hii ilipochapishwa, Mheshimiwa Seyid Abdul Qadir akaandika kama utambalisho:

> "Jina la mwana mtaalamu, Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad, wa baba mtaalamu, ni uhakikisho tosha kwamba hotuba hii ni ya kitaalamu sana. Mimi pia ninayo elimu kidogo ya historia ya Kiislamu, nami naweza kudai kwamba kuna wanahistoria adimu, wakiwa Waislamu ama si Waislamu, walioweza kufikia kwenye kina cha chanzo hasa cha hitilafu zilizoibuka katika zama za Hadhrat Uthman[ra], na kufaulu kufahamu sababu za maasi ya kwanza ya kuhatarisha. Hadhrat Mirza Sahib si tu amefaulu kutambua sababu za maasi hayo, bali ameeleza kwa uwazi na kwa kufululiza matukio yale yaliyotikisisha kwa muda mrefu kasri ya Ukhalifa. Nafikiri madhumuni kama haya yaliyohakikisha kwa

hoja madhubuti hayajapata kusomwa na wapendao kupata elimu ya historia ya Kiislamu”.

Nawashukuru Sheikh Bakri Abedi Kaluta na Sheikh Asif Mahmood Butt waliochukua jukumu la kuifasiri hotuba hii ya muhimu kwa Kiswahili. Ndani mwake mna elimu na somo kwa Waaminio. Mwenyezi Mungu Awanufaishe wasomaji wote watakaozingatia kwa makini yaliyomo humu.

Kabla ya kupeleka tafsiri hii mtamboni kwa kuchapishwa, Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri wa zamani wa Tanzania na Sheikh Ahmad Adnan Hashmi wa Kenya walidurusu, kisha nikaisoma kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu. Sheikh Ansar Hussain alizipanga herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha *fometi*. Mungu Awapatia malipo bora waliosaidia kwa njia mbalimbali.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 22 Aprili 2020

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

نَحۡمَدُہٗ وَ نُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [2]

# HAJA YA KUIELEWA HISTORIA YA KIISLAMU

(Hotuba ya Hadhrat Fadhle Umar, Khalifatul Masih wa pili[ra], aliyoitoa mnamo tarehe 26 February mwaka 1919 katika kikao cha Martin Historical Society ya Islamia College, Lahore).

Umepita muda sasa ambapo kwa furaha kubwa sana nililisikia jambo hili kwamba ndani ya Chuo cha Islamia cha Lahore kumeanzishwa Jumuiya fulani ambapo wataalamu wa mambo ya historia watakuwa wakieleza utafiti wao. Nilifurahishwa sana na jambo hili, kwa sababu kuifahamu historia ni kichocheo kikubwa katika maendeleo ya mataifa, na kaumu yoyote ile ambayo haifahamu riwaya za historia yake ya nyuma, haiwezi asilan kupiga hatua ya maendeleo. Kuzifahamu hali za mababu zetu kunatoa mwongozo wa kuelekea kwenye malengo ya juu kabisa. Hivyo, nilipofahamu juu ya kuanzishwa kwa Jumuiya hii, basi kwa wazo hili kwamba wakati itakapotolewa humo mihadhara mingine yenye maudhui ya kihistoria, kutakuwemo na

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

mihadhara ya aina hii juu ya Historia ya Kiislamu, ambapo wanafunzi wa vyuo vya elimu wataweza kuwa na fununu kwamba majukumu ya mababu zao yalikuwa ni magumu kiasi gani na kwamba ni kwa namna gani walivyokuwa wakiyatekeleza kwa ubora na uimara, na watafahamu kwamba sisi ni watoto wa mababa wa aina gani na kwa kuwa kwetu vizazi vyao na warithi wao tunayo majukumu gani. Na kwa kuona vitendo vyenye shani vya mababu zao na shani zao za hali ya juu watapatwa na mawazo ya kuwa kama wao. Hivyo, mimi nilifurahishwa sana na kuanzishwa kwa Jumuiya hii. Na sasa nilipoambiwa nitoe hotuba ndani ya Jumuiya hii juu ya sehemu fulani ya Historia ya Kiislamu, nimeahirisha safari yangu kwa furaha kubwa na kukubali, kwa fursa hiyo, kueleza mbele yenu utafiti wangu wa baadhi ya madhumuni ya kihistoria.

## Umuhimu wa Madhumuni

Niliambiwa kwamba nieleze baadhi ya masuala ya historia ya Kiislamu. Na ingawa ndani ya historia ya Islam, zama muhimu kuliko zote ni zama zile ambamo Mtume[saw] kwa amri ya Mwenyezi Mungu, aliitangaza Islam duniani, na kwa juhudi kubwa ya miaka 23 akaacha athari ndani ya mioyo ya malaki ya watu na kuanzisha Jumuiya ya maelfu ya watu ambao mawazo yao, kauli na vitendo vyao vikawa ni Islam tu, lakini kwa kuwa msingi wa mfarakano ndani ya Islam uliwekwa

miaka kumi na mitano baada ya kufariki kwa Mtume[saw], na baada ya wakati huo ufa wa mfarakano ukawa unazidi kupanuka miongoni mwa Waislamu, na historia ya zama hizo hizo ikawa imefichika ndani ya mapazia yenye giza totoro, na mbele ya maadui wa Islam ni doa lenye kuchukiza juu ya Islam, na hata kwa walio marafiki wa Islam ni swali lenye kuumiza kichwa na ni wachache sana waliotaka kulivuka salama salimini bwawa hilo la tope la historia ya zama hizo na kuweza kufanikiwa katika dhamira yao. Ndio sababu nimependelea hivi kwamba leo niseme machache mbele yenu kuhusiana na haya.

## Wakati Uliopita Wenye Shani wa Islam

Nyinyi mtakuwa mnafahamu kwamba kazi ile ambayo Mwenyezi Mungu Amenikabidhi (yaani kuilea Jumuiya ya Ahmadiyya na kuyatimiza mahitajio yake na kuwazia juu ya maendeleo yake) ni kazi ya namna inayojumuisha sehemu nyingi. Hivyo, kwa ajili ya kuitekeleza, inakuwa ni jambo la lazima mno kwangu niwe na elimu ya yale madhumuni makhsus ya historia yanayohusiana na zama za ukhalifa. Ndio sababu juu ya kuwa na fursa kidogo, inanibidi niitalii historia ya zama hizo. Na ingawa kazi yetu ya asili ni kuihakiki na kuitafakari dini, lakini kutokana na kutalii huku, baadhi ya mambo yaliyojificha ya historia ya mwanzoni ya Islam, yamedhihirika kwangu kwa fadhili za Mwenyezi Mungu,

ambayo watu wengi wa zama hizi hawayafahamu. Na kutokana na kutofahamu huku, baadhi ya Waislamu wanakuwa wameichoka dini yao na wanaziona zama zao zilizopita kuwa za kutisha mno kiasi hiki kwamba kwa sababu hiyo hawawezi kuwa na matumaini yoyote ya mustakbali wenye shani. Lakini kukata kwao tamaa huku ni makosa, na mawazo yao kama haya si sahihi, na ni matokeo tu ya jambo hili kwamba wao hawana elimu sahihi ya historia ya Islam, waila wakati uliopita wa Islam ni wenye shani na usiokuwa na ila. Na wote waliokaa pamoja na Mtume[saw] walikuwa ni watu wenye khulka njema za hali ya juu hata kwamba mfano wao haupatikani kwa kaumu yoyote ile duniani hata kama iwe iliyolelewa na nabii yeyote. Ni wale tu waliokaa na Mtume[saw] ambao kuhusiana nao inaweza kusemwa kwamba wao wakimfuata Mwalimu na Bwana wao katika nyayo zake wakajipatia hali ya kiroho kiasi hiki kwamba hata walipokuwa wametingwa ndani ya migogoro ya hatari ya kisiasa, hawakuachana na ucha Mungu na uaminifu, na walikuwa wakitekeleza majukumu yao ya kitawala bila ya kulegea kama vile walivyokuwa katika wakati ule walipokuwa na dhiki mno na tandiko lao lilikuwa ni sakafu isiyokuwa na zulia ya msikiti wa Mtume[saw] na mito yao ilikuwa ni mikono yao, shughuli yao ilikuwa ni kusikiliza maneno yenye baraka ya Mtume[saw] na burudisho lao lilikuwa ni kufanya ibada ya Mwenyezi Mungu Mmoja.

## Waja wa Kwanza waliojitolea kwa Islam — Hadhrat Uthman[ra] na Hadhrat Ali[ra]

Huenda mtakuwa mmefahamu kwamba nia yangu, kwa wakati huu, ni kueleza kwa kiasi fulani, kuhusiana na Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra] na wa Hadhrat Ali[ra]. Hawa wawili ni miongoni mwa wale wa mwanzo waliojitolea kwa Islam na wale pia waliokuwa pamoja nao walikuwa ni miongoni mwa matunda bora kabisa ya Islam. Kukosoa uaminifu na ucha Mungu wao, kwa hakika, ni kuiaibisha Islam. Na Mwislamu yeyote atakayeutafakari ukweli huu, atalazimika kufikia kwenye matokeo haya kwamba dhati ya watu hao, kwa hakika, imeepukana na kila aina ya kujifarakanisha katika makundi. Na jambo hili sio lililokosa dalili, bali kurasa za historia zinatoa ushahidi wa jambo hili kwa yule anayezisoma kwa kufungua macho.

## Maelezo Potofu ya Wanahistoria Wasio Waislamu

Kulingana na utafiti wangu, chochote kinachoelezwa kuhusiana na watakatifu hawa na marafiki zao, ni njama za maadui wa Islamu. Na ingawa baada ya masahaba[ra] kupita, hata baadhi ya wale waliojiita Waislamu, wakiwa wakifuata matamanio yao, walitoa tuhuma dhidi ya mmoja wa watakatifu hao au mwingine, lakini juu ya yote hayo, ukweli daima umekuwa juu, na uhakika kamwe haufichiki nyuma ya pazia. Naam, katika zama hizi ambapo Waislamu wamekuwa hawaifahamu

historia yao, na wenyewe wakiwa hawaijui dini yao, maadui wa Islam, ama wamechukua riwaya za baadhi ya maadui toka kwenye historia ya Kiislamu au wamechukua maana potofu ya matukio sahihi na kutengeneza historia za aina hii ambazo kwazo masahaba[ra] na kwa kupitia kwao Islam ipate lawama. Kwa kuwa siku hizi miwani ya Waislamu ambayo wanaitumia kutazamia kila kitu imekuwa ni hawa hawa wanahistoria wasio Waislamu, hivyo wakakubali kila walichokieleza (hao wanahistoria). Wale watu ambao wenyewe walipata fursa ya kuvisoma vitabu historia kwa Kiarabu, hao pia kwa kuuhofu ukosoaji mkali wa (wanazuoni wa) Ulaya, wakazifahamu riwaya hizo za kipuuzi na za bandia zilizofanywa kuwa msingi wa utafiti wa waandishi wa Ulaya, kuwa sahihi na kuzipa kipaumbele, na kuziona riwaya zingine kuwa ni zenye makosa. Na kwa njia hii zama hizi zikakaribia kukosa watu wale waliojaribu kuyatazama matukio kwa uasilia wake.

## Masahaba[ra] Hawakuwa Chanzo cha Fitina Ndani ya Islam

Likumbukeni vema jambo hili kwamba dhana hii kuwa waliohusika na fitina ndani ya Islam walikuwa ni baadhi ya masahaba[ra] wakubwa, ni kosa kabisa. Hali ya watu hao kwa mtazamo wa jumla, haiwezi hata kufikiriwa kuwa wao walijaribu kuiangamiza Islam kutokana na

matashi au manufaa yao binafsi. Wale watu waliojaribu kuzitafuta ndani ya kundi la Masahabu sababu za kuzuka hitilafu na mifarakano ndani ya Waislamu, walifanya makosa makubwa. Chokochoko za fitina zilizalika sehemu nyingine, na ni katika kuzitafuta huko huko ndipo inaweza kutumainiwa kufikia kwenye matokeo yaliyo sahihi. Zile riwaya potofu zilizokuwa zimeenezwa kuhusu zama hizo, kama zichukuliwe kuwa ndio sahihi, basi hatabakia hata sahaba mmoja atakayeepuka kuwa na hisa katika fitina hiyo, na hapo hataonekana hata mmoja ambaye amekuwa amekaa imara kwa nguvu katika ucha Mungu na uaminifu, na hili linakuwa ni shambulio kwenye ukweli wa Islamu kiasi cha kuung'oa mzizi na msingi wake. Hadhrat Masih[as] anasema kuwa mti hujulikana kwa matunda yake. Na kwa mujibu wa riwaya hizo, matunda ya mti wa Islam yathibitika kuwa ni machungu kiasi hiki kwamba hakuna yeyote atakayekuwa tayari kuyapewa bure, achilia mbali kuyanunua. Lakini, je kuna mtu yeyote aliyesoma walau kidogo sana kuhusu nguvu takatifu ya Mtume[saw], aweza kuwa tayari kuliamini jambo hili? La hasha! Kufikiria hivi pia kuko mbali na akili kwamba wale watu waliokaa pamoja na Mtume[saw], waliokuwa masahaba[ra] wake wakubwa na waliojitolea kwake na waliokuwa na undugu wa karibu naye sana, wao pia pamoja na masahaba[ra] wengine wote bila ya kuacha hata mmoja, wakawa wameharibika kwa miaka

michache tu, kiasi hiki kwamba kwa sababu ya matamanio binafsi, sio kwamba kwa msingi wa tofauti fulani za kidini, wakawa wameingia kwenye mifarakano kiasi hiki kwamba madhara yake yakautikisa mzizi wa Islam. Lakini yasikitisha kwamba ingawa Waislamu hawasemi kwa matamshi kwamba masahaba[ra] walianzisha fitina kwa kuiangamiza Islam, lakini wakazifahamu kuwa ni riwaya za kweli za wale watu ambao hawakuikubali Islam sawa sawa, bali waliikubali Islam kwa kukiri tu kwa ulimi, na halafu kuzitegemea riwaya za watu wa aina hii ambao walikuwa ni maadui wakubwa wa Islam waliodhamiria kuifuta Islam, wakayakubali mambo hayo ambayo matokeo ya lazima ya kuyakubali ni kwamba, Mungu Apishe mbali, kundi la masahaba[ra] walikuwa hawana kabisa ucha Mungu na uaminifu.[3]

Katika maelezo yangu nitalizingatia jambo hili kwamba nisizitaje tarehe n.k. ili kusiwe na shida katika kufahamu na madhumuni yasiwe magumu kueleweka. Kwa kuwa makusudio hasa ya hotuba yangu hii ni kuwafahamisha wanafunzi wa vyuoni baadhi ya mambo muhimu ya mwanzoni mwa Islam na ni kutokana na sababu hii hii,

[3] Nimeshaongeza badhi ya kumbukumbu la kihistoria wakati wa kurudia kwa kuchapisha na kumlinda msomaji kupata shida imetegemewa na Tabarii tu. *Illa-ma-shaallah*. Mwandishi

kadri niwezavyo nitajiepusha kuzitumia ibara za Kiarabu na nitayaeleza matukio kwa namna ya hekaya.

## Kwa Nini Hitilafu Zilitokea Katika Zama za Khalifa wa Tatu?

Bila shaka jambo hili liko wazi kwa wasomi wote Waislamu kuwa alam za hitilafu ndani ya Waislamu zilidhihirika kwa uwazi mno katika zama za Khalifa wa Tatu. Kabla ya hapo katika zama za Hadhrat Abu Bakr[ra] na Hadhrat Umar[ra] hitilafu haikushika sura ya kutisha na Waislamu walikuwa na umoja imara kiasi hiki kwamba wote, marafiki kwa maadui, waliona kuwa mfarakano wake ni jambo lisilowezekana na ni kutokana na sababu hii hii watu kwa kawaida husema kuwa mfarakano huu ni matokeo ya udhaifu wa Khalifa wa Tatu, ilhali, kama nitakavyoeleza baadaye, uhakika haukuwa hivyo.

## Habari za Mwanzoni za Hadhrat Uthman[ra]

Baada ya Hadhrat Umar[ra] mtazamo wa masahaba[ra] wote uliangukia kwa Hadhrat Uthman[ra] kwa ajili ya kukalia kiti cha Ukhalifa, naye alichaguliwa katika kazi hiyo kwa mashauriano ya masahaba[ra] wakubwa. Yeye alikuwa ni mkwe wa Mtume[saw] aliyeoa mabinti wawili wa Mtume[saw] mmoja baada ya mwingine. Alipofariki binti huyo wa pili wa Mtume[saw], basi Mtume[saw] akasema kama ningekuwa na binti mwingine, huyo pia ningemuozesha Hadhrat Uthman[ra] Inafahamika kutokana na haya kwamba yeye alikuwa na daraja makhsus mbele ya

Mtume[saw]. Alikuwa na heshima maalum kwa watu wa Makka, na wakati huo — kulingana na hali za nchi ya Kiarabu — alikuwa ni mtu tajiri. Baada ya Hadhrat Abu Bakr[ra] kusilimu, miongoni mwa watu makhsus aliowachagua kuwahubiria, alikuwemo pia Hadhrat Uthman[ra] . Dhana ya Abu Bakr[ra] juu yake haikuwa yenye makosa, kwani akasilimu ndani ya siku chache tu za kuhubiriwa na kwa njia hii akajumuika na wale اَلسَّابِقُوْنَ الْاَوَّلُوْنَ , yaani, ndani ya kundi la wale waliosilimu mwanzoni mwa Islam ambao Kurani imewasifu kwa maneno ya kuonewa mno gera. Heshima na taadhima aliyoipata Uarabuni inaweza kufahamika kwa kiasi fulani kutokana na tukio hili kwamba wakati Mtume[saw] alipoenda Makka kwa sababu ya Ruya fulani na watu wa Makka kwa kupofushwa na bughudha na uadui wakamnyima ruhusa ya kufanya Umra, basi Mtume[saw] akatoa ushauri kwamba atumwe mtu fulani mwenye kuaminika kwa watu wa Makka kwa ajili ya kwenda kuliongelea suala hili na akawa amemchagua Hadhrat Umar[ra] kwa ajili hiyo. Hadhrat Umar[ra] akajibu, Ewe Mtume wa Allah! Mimi niko tayari kwenda, lakini kama kuna yeyote yule awezaye kufanya nao maongezi huko Makka basi huyo ni Hadhrat Uthman[ra], kwani yeye anayo heshima makhsus kwa watu hao. Hivyo kama mtu mwingine akienda basi hakuna matumaini ya kufanikiwa kwake kama vile yaliyopo kwa Hadhrat Uthman[ra]. Na Mtume[saw] pia akaliona neno lake hili kuwa ni sahihi na akamtuma yeye kwa ajili ya kazi hii.

Inafahamika kutokana na tukio hili kuwa Hadhrat Uthman[ra] alikuwa akitazamwa kwa mtazamo wa heshima hata na makafiri.

## Cheo cha Hadhrat Uthman[ra] Machoni mwa Mtume[saw]

Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akimheshimu sana. Wakati fulani Mtume[saw] akiwa amejinyoosha, Hadhrat Abu Bakr[ra] akaja na Mtume[saw] akaendelea vile vile kulala. Halafu akaja Hadhrat Umar[ra], naye akaendelea vile vile kujinyoosha. Halafu akaja Hadhrat Uthman[ra], basi mara moja akazifanya nguo zake sawa sawa na kusema kwamba Hadhrat Uthman[ra] ana tabia ya haya sana, hivyo mimi ninafanya hivi kwa kuzingatia hisia zake (Muslim Kitab Fadhailis Sahaba[ra], bab min fadhail Uthman bin 'Affaan). Yeye alikuwa ni miongoni mwa watu adimu, ambao hata kabla ya kusilimu hawakuwahi kuonja pombe hata kidogo wala kuikaribia zinaa. Na hizi zilikuwa ni sifa ambazo zilikuwa zikipatikana kwa watu wachache sana ndani ya nchi ya Arabuni ambapo kunywa pombe ilikuwa ni fahari na zinaa ilikuwa ni shughuli ya kila siku.

Ilmuradi, yeye hakuwa mtu wa kawaida. Alikuwa na khulka za daraja ya juu kabisa. Alikuwa pia ametukuka sana katika mtazamo wa kidunia. Alikuwa mstari wa mbele katika Islam. Mtume[saw] alipendezwa naye sana. Na Hadhrat Umar[ra] alimsema kuwa ni miongoni mwa wale watu sita ambao Mtume[saw] aliendelea kuridhika nao

kwa kiwango cha juu kabisa hadi kifo chake. Na halafu alikuwa ni mmoja miongoni mwa "*Asharah Mubasharah"* yaani wale watu kumi waliopewa bishara na Mtume[saw] ya kuingia peponi.[4] (Tirmidhii abwaabul manaaqib, manaaqibu Abdirrahman bin 'Auf).

Kwa miaka sita tangu alipoketi katika kiti cha Ukhalifa, hakukuibuka aina yoyote ya fitina katika utawala wake, bali kwa ujumla watu walipendezwa naye sana. Baada ya hapo ghafla ikaibuka fitina ambayo ikaongezeka na kufikia kiasi hiki kwamba hakuna yeyote aliyeweza kuisitisha na matokeo yake ikathibitika kuwa yenye madhara makubwa kwa Islam. Miaka elfu moja na mia tatu imeshapita lakini hadi sasa athari yake haijatoweka ndani ya umati wa Kiislamu.

## Fitina Ilizukia Wapi?

Sasa swali ni hili kwamba fitina hii ilizukia wapi? Baadhi ya watu wamesema kuwa chanzo chake ni Hadhrat Uthman[ra] na baadhi wamesema kuwa ni Hadhrat Ali[ra]. Baadhi wanasema kuwa Hadhrat Uthman[ra] alianzisha baadhi ya bidaa zilizowafanya Waislamu wahamaki. Na baadhi wanasema kwamba Hadhrat Ali[ra] alianzisha juhudi za siri za kuutwaa Ukhalifa na kuanzisha

[4] Kwa hakika Asharah Mubasharah umegeuka kuwa usemi, waila Mtume[saw] aliwapa bishara za kuingia peponi masahaba[ra] wengi zaidi ya hawa. 'Ashara Mubashara mradi wake ni wale Wahajirina kumi waliokuwa ni wajumbe wa kikao cha Shura cha Mtume[saw] na ambao aliwategemea sana.

upinzani dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] na kumuulisha ili yeye awe Khalifa. Lakini mambo yote haya mawili si sahihi. Hadhrat Uthman[ra] hakuanzisha bidaa yoyote ile wala Hadhrat Ali[ra] hakumuulisha ili aje awe Khalifa, au kushiriki katika njama za kumfanya auawe. Bali kulikuwepo na sababu zingine tu za fitina hiyo. Dhati za Hadhrat Uthman[ra] na za Hadhrat Ali[ra] zimeepukana kabisa na lawama za aina hii. Wao walikuwa ni watu watakatifu mno. Hadhrat Uthman[ra] alikuwa ni mtu ambaye kuhusiana naye Mtume[saw] alisema kwamba yeye aliihudumia Islam kiasi hiki kwamba sasa afanye chochote apendacho, Mwenyezi Mungu hatamuuliza. (Tirmidhi Abwaabul Manaaqib, bab manaaqib Uthman bin 'Affaan). Mradi wake haukuwa huu kwamba hata kama akengeuke hata toka katika Islam hataulizwa, bali ulikuwa ni huu kwamba ndani mwake mlikuwa na sifa bora kiasi hiki na kwamba alikuwa amepiga hatua katika wema kiasi hiki kwamba ilikuwa haiwezekani kuwa kitendo chake chochote kiwe kinyume na maagizo ya Mwenyezi Mungu. Hivyo, Hadhrat Uthman[ra] hakuwa mtu wa aina hii kwamba angeanzisha jambo lolote lililo kinyume na sheria wala Hadhrat Ali[ra] hakuwa mtu wa aina hii kwamba angefanya njama za siri kwa ajili ya kuupata Ukhalifa. Kadiri nilivyotafakari na kutalii, kuna sababu nne za fitina hii yenye kutisha.

## Sababu Nne za Fitina

Kwanza, kwa kawaida, tabia ya wanadamu huelekea katika kutafuta heshima na mali, isipokuwa tu wale watu ambao Mwenyezi Mungu hususan Ameisafisha mioyo yao. Baadhi ya watu miongoni mwa Waislamu wapya, ambao hawakuwa na imani zilizokamilika, walipoona heshima walizopata masahaba[ra] na vyeo vyao na maendeleo na utawala wao, wakaanza kufanya husuda. Na kama vile ilivyokuwa desturi tangu kale, wakaanza kuwa na matumaini ya kwamba watu hao waachane na kazi zote za kiutawala na kuzikabidhi kazi zote hizo kwetu na wawape watu wengine pia fursa ya kudhihirisha vipawa vyao. Watu hao pia walikuwa wakiona vibaya kwamba mbali ya kuwa utawala ulikuwa mikononi mwa masahaba, walikuwa pia wakipata hisa makhsus katika mali. Hivyo, watu hawa wakawa wanaungulia ndani kwa ndani na wakawa wakiyasubiri mabadiliko yatakayoiangamiza nidhamu hii ili utawala uje mikononi mwa watu hao, na hao pia waweze kuonyesha vipawa vyao na wapate heshima za kidunia na mali. Katika serikali za kidunia, mawazo ya aina hii, kwa kiwango fulani, yanaweza kusameheka, bali kwa nyakati zingine yanaweza pia kusemwa kuwa ni yenye kuingia akilini, kwa sababu msingi wa serikali za kidunia uko moja kwa moja juu ya sababu za kidhahiri, na

miongoni mwa sababu za kidhahiri za maendeleo, sababu kubwa sana ni kuingiza pia ndani ya utawala mawazo mapya na roho mpya, ambayo huwezekana katika sura hii hii tu kwamba wale watendaji wa mwanzoni wajiengue kazini na kuwaachia nafasi wengine.

Pili: Kwa kuwa utawala wa kidunia hupata mamlaka kutokana na uwakilishi wa umma, hivyo inakuwa ni muhimu kwake kuheshimu rai za umma. Na inakuwa ni lazima kwamba wale watu wanakuwa wanajihusisha hasa katika utekelezaji wa kazi zake ambao ndio wawakilishi wa rai za umma. Lakini katika silsila za kidini mambo yapo kinyume kabisa na hayo. Huko kushikamana na sheria iliyowekwa kunatangulia kanuni zote, na rai za mtu binafsi zimekatazwa kabisa, isipokuwa tu katika yale masuala ambayo sheria haikuyaongelea. Halafu, silsila za kidini hupata madaraka toka kwa Mwenyezi Mungu, na wale ambao hatamu ya nidhamu yake imo mikononi mwao faradhi yao huwa kwamba wasiwaache watu waende kombo katika masuala ya kidini, na badala ya wao kueleza mawazo ya watu, wao huwajibika kuyaelekeza mawazo ya watu kwenye mahitajio ambayo yanaafikiana na yale yaliyoandaliwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya zama hizo.

## Ukhalifa wa Kiislamu Ulikuwa ni Nidhamu ya Kidini

Ilmuradi, kwa sababu ya kutoufahamu uhakika wa Islam, masawali haya yakawa yanazalika ndani ya mioyo ya watu hawa. Wao hawakuwa wanafikiria kuwa Ukhalifa wa Kiislamu haukuwa utawala wa kidunia wala masahaba[ra] hawakuwa maamiri wa kawaida wa Dola, bali Ukhalifa wa Kiislamu ulikuwa ni nidhamu ya kidini na ulistawishwa kwa sheria makhsus za Kurani Tukufu zilizotajwa kwenye sura An nuur, na masahaba[ra] walikuwa ni nguzo zile za dini ambao Mwenyezi Mungu Alifaradhisha kuwafuata kwa ajili ya kuyapata madaraja ya kiroho. Masahaba wakiziacha shughuli zao, wakiishi katika kila aina ya umaskini na ufukara, wakiyahatarisha maisha yao, wakiacha kukaa pamoja na wapenzi wao na jamaa zao, wakiziacha watani wao na wakiachana na mawazo yao na jadhba zao, wakaaumua kukaa pamoja na Mtume[saw] na kumpenda, na baadhi yao kwa robo karne wakiwa wanafunzi wa Mtume[saw] wakajifunza Islam somo kwa somo na kwa kuitekeleza wakajiimarisha kimatendo. Wao walikuwa wakifahamu kwamba nini maana ya Islam, makusudio yake ni nini, uhakika wake ni upi, ni namna gani ya kuyatekeleza mafundisho yake na ni faida zipi zaweza kupatikana kwa kuyatekeleza. Hivyo, wao hawakuwa wafalme wa serikali ya kidunia au mawaziri wake. Wao walikuwa ni

waalimu wa dini ya mwisho kabisa na wa sheria iliyoletwa na Khaatamun Nabiyyiin[saw]. Na ilifaradhishwa kwao kwamba watoe ufafanuzi wa Islam kwa amali zao, kwa tabia zao, kwa harakati zao na kwa mienendo yao na kuyaimarisha mafundisho yake ndani ya mioyo ya watu na kuwafanya wayatekeleze. Wao hawakuwa wenye kuuhami udikteta, bali wao walikuwa ni wenye kuihami sheria yenye nuru, wao waliichukia dunia, na kama wangekuwa na hiari wangejitenga na dunia na kwenda kuishi upwekeni na kujifariji nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Lakini wao walikuwa wamelazimika katika jukumu hili ambalo Mwenyezi Mungu na Mtume[saw] wake waliliweka juu ya mabega yao.[5] Hivyo chochote wlichokuwa wakikifanya hawakukifanya kwa matashi yao wenyewe, bali walikuwa wakifanya chini ya hukumu ya Mwenyezi Mungu na kulingana na maagizo ya Mtume[saw] Wake, na lilikuwa ni kosa la hatari sana kuwafanyia husuda au kuwadhania vibaya. Ama lawama hii kwamba kwa nini masahaba[ra]

[5] Kutokana na matukio ya baadae ya historia ya Kiislamu jambo hili linathibitika kwa uwazi kabisa kwamba kujihusisha kwa masahaba[ra] kulikuwa na faida na baraka kiasi gani, kwa sababu, katika kuondoa kuwahusisha masahaba[ra] kwa muda fulani, Mwenyezi Mungu Alifahamisha kwamba matokeo mabaya kiasi gani yanaweza kutokea kwa kutengana nao. Wakati huo Uislamu ulifanyiwa dhihaka kwa mikono ya watu waliokuwa wakijiita Waislamu kiasi hiki kwamba mioyo yapata hofu kwa kuzisoma hali hizo na miili inasisimka. (Mirza Mahmud Ahmad).

hususan ndio waliokuwa wakipewa mali, hii ilikuwa pia ni wasiwasi, kwa sababu chochote walichokuwa wakikipata masahaba, walikuwa wakipata kulingana na haki zao. Wao hawakuwa wakichukua kwa kuziminya haki za watu wengine. Bali kila mtu, hata kama aliyesilimu jana, alikuwa akipata haki yake vile vile alivyopata mtu aliyetangulia katika imani. Naam, kazi ya masahaba[ra] na juhudi yao na kujitolea kwao kulipita watu wengine na huduma zao za zamani zilikuwa zikiongezea hizo. Hivyo wao walikuwa na haki zaidi kuliko watu wengine sio kwa dhuluma, bali kwa uadilifu, ndio sababu walikuwa wakipewa zaidi kwa kulinganishwa na watu wengine. Wao hawakujipangia hisa zao, bali Mwenyezi Mungu na Mtume[saw] wake ndio waliopanga hisa zao. Kama watu hao wasingetendewa katika hali makhsus, sasa zile bishara zingetimiaje ambazo zilitolewa ndani ya Kurani na Hadithi za Mtume[saw] juu ya maendeleo ya watu hao na kupata kwao neema na ustawi na kuhusiana na utajiri wao. Kama Hadhrat Umar[ra], wakati wa kuanguka kwa utawala wa Kisra na wakati wa kuziteka mali zake asingempa na kumvalisha Suraka bin Malik bangili za Kisra, neno lile la Mtume[saw] lingetimiaje pale aliposema kwamba ninaziona bangili za Kisra mkononi mwa Suraka. Bali mimi nitasema hivi pia kwamba chochote walichokuwa wakipata masahaba[ra] hawakuwa wakipata kwa kunyang'anya haki za wengine, bali kila mtu, hata

yule aliyekuwa akifanya kazi kidogo tu ya utawala, alikuwa akipewa haki yake, na Makhalifa walikuwa waangalifu sana katika hili. Masahaba walikuwa wakipewa tu haki yao na wao kutokana na kazi zao na huduma zao za awali, bila shaka walikuwa wakipata zaidi ya wengine, na halafu miongoni mwao walikuwako waliokuwa wakishiriki katika vita zilizokuwa zikiendelea na katika zawadi zilizotokana na huduma hizo, wao pia walikuwa wanastahiki malipo hayo kama watu wengine. Lakini jambo hili pia linapaswa likumbukwe kwamba inathibitika kutokana na historia kuwa masahaba[ra] hawakuwa na desturi ya kuzilimbikiza mali hizo au kuzitumia kwa ajili yao binafsi, bali wao walikuwa wakichukua hisa yao kwa ajili tu ya kuuthibitisha ukweli wa maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume[saw] wake, waila kila mmoja miongoni mwao alikuwa hana kifani katika ukarimu na mkono wa kutoa, na mali zao zilikuwa zikitumika katika kuwatunza maskini na kuwatatulia matatizo yao.

## Hakukuwa na Sababu ya Kuwadhania Vibaya Masahaba[ra]

Kwa uchache, ile husuda na dhana mbaya dhidi ya masahaba[ra] iliyofanywa na baadhi ya watu haikuwa na sababu yoyote. Lakini kusiwe na sababu au kuwe na sababu, mbegu yake ilipandwa na tabaka moja miongoni mwa watu waliokuwa hawajui uhakika wa dini

wakawaona wao kuwa wamejitwalia mali pasipo haki, na wakawa wanasubiri kwamba ni lini waipate fursa yoyote na kuwaweka kando watu hao na wamiliki utawala na mali ya serikali. Sababu ya pili ya ufisadi huu ilikuwa ni kwamba Islam ilitoa uhuru wa kutoa mawazo na uhuru wa vitendo na usawa wa watu katika kiwango ambacho hakikupatikana hapo kabla hata kwa watu wenye mawazo makubwa ya kifalsafa. Na kama ilivyo desturi kwamba baadhi ya watu ambao ndani kwa ndani wana viini vya maradhi, hao hata wapate vyakula vizuri vya hali ya juu kabisa, badala ya kufaidika navyo hudhurika. Kutokana na kanuni hii ya uhuru wa mawazo na vitendo, baadhi ya watu, badala ya kufaidika, wakapata hasara, na wakashindwa kujiweka katika mipaka yake. Mwanzo wa maradhi haya ulianzia toka zama za Mtume[saw] wakati Mwislamu fulani wa jina tu aliyekuwa na roho chafu aliposema maneno haya mbele ya Mtume[saw]: ‘Ewe Mtume wa Mungu! tenda kwa uchamungu, kwani hukufanya uadilifu katika ugawaji wa mali.’ Hapo Mtume[saw] akasema:

إِنَّهُ يَخْرُجُ مِنْ ضِئْضِئِ هٰذَا قَوْمٌ يَتْلُوْنَ كِتَابَ اللّٰهِ رَطْبًا لَا يُجَاوِزُ حَنَاجِرَهُمْ يَمْرُقُوْنَ مِنَ الدِّيْنِ

كَمَا يَمْرُقُ السَّهْمُ مِنَ الرَّمِيَّةِ

(Bukhari Kitabul Maghaazi, bab ba‘th Ali ibni Abii Taalib wa Khalid bin Walid ilal Yaman qabla hajjatil wadaai)

Yaani, itatokea kaumu fulani toka katika vizazi vya mtu huyu ambao wataisoma sana Kurani Tukufu lakini

haitateremka chini ya halkumu zao nao watatoka katika dini kama vile mshale unavyokosa shabaha.

Mara ya pili moto uliojificha wa ya mawazo ya aina hii ulitoa mwako wake katika zama za Hadhrat Umar[ra] wakati mtu fulani aliposimama katika kikao na kumshutumu mtu kama Umar[ra] asiyejipendelea nafsi yake na Khalifa aliye mhifadhi wa mali ya umati wa Muhammad[saw] kwamba: 'Hiyo shati umeipataje?' Lakini katika nyakati zote hizo mbili fitina hiyo haikuchukua sura yoyote ya kutisha kwa sababu hadi wakati huo hakukuwa na ardhi iliyokuwa tayari kuiistawisha wala haukuwa msimu wenye kuiafiki. Naam, katika zama za Hadhrat Uthman[ra] mambo yote haya mawili yakapatikana na mmea huu, ambao mimi nitausema kuwa ni mmea wa vurugu, ukawa umesimama kwenye shina lenye nguvu sana na katika zama za Hadhrat Ali[ra] ukawa umestawi kiasi hiki kwamba matawi yake yakawa yamekaribia kueneza kivuli chake duniani kote, lakini Hadhrat Ali[ra] akayatambua madhara yake katika wakati uliofaa na kwa mkono wa nguvu akaukata na kuuangusha, na ingawa hakuweza kuufuta kabisa, angalau aliidhibiti athari yake.

Sababu ya tatu, kwa rai yangu, ni hii kwamba kutokana na athari za miale yenye nuru ya Islam, watu wengi walifanya mabadiliko makubwa sana ya maisha yao, lakini athari hiyo isingeweza kuuondoa kikamilifu

upungufu ule ambao huwa daima unamfanya mwanadamu ahitaji kupata mwalimu kwa ajili ya kupata elimu ya dini na dunia. Wakati wa Mtume[saw], ambapo watu walisilimu makundi kwa makundi, hapo pia hatari hii ilikuwepo, lakini yeye[saw] alikuwa na ahadi makhsus ya Mwenyezi Mungu kuwa watu wale waliokuwa wakisilimu ndani ya zama hizo za maendeleo, wataepushwa na athari mbaya. Kwa mujibu huo, ingawa baada ya kifo chake likazuka wimbi kubwa la uasi wa kuritadi, lakini mara moja likazama na watu wakaufahamu uhakika wa Islam. Lakini baada yake, baada ya ushindi wa Iran, Siria na Misri, na kutokana na kuchanganyikana kwa Islam na dini zingine, ushindi ule wa kiroho ilioupata Islam, huo huo ukawa sababu ya vurugu katika mfumo wake wa kisiasa. Mamilioni ya watu waliingia ndani ya Islam na kwa kuyaona mafundisho yake yenye shani wakawa waliojitolea kiasi hiki kwamba wakawa tayari hata kutoa uhai wao. Lakini idadi hii ya watu wapya waliosilimu ikaongezeka kiasi ya kwamba haikuweza kufanyika mpango wenye kuridhisha wa kuwaelimisha barabara. Kama ilivyo kawaida na inavyofahamika kutokana na mtaala wa kina wa akili ya mwanadamu, kutokana na jadhba iliyokuwepo hapo mwanzoni, haja ya kuwalea na kuwafundisha watu hao haikusikika. Walikuwa wakitenda yale waliyoyaona Waislamu wakiyatenda na kila hukumu walikuwa wakiitekeleza kwa furaha. Lakini

kadiri ile jadhba ya awali ilivyoenda ikipungua, wale watu ambao hawakupata fursa ya kupata ulezi wa kiroho wakaanza kuona ugumu kutekeleza hukumu za Kiislamu. Na ile jadhba mpya ilipoanza kupoa, tabia za zamani zikaanza tena kupata nguvu. Makosa yako kwa kila mwanadamu, na mwanadamu hujifunza hatua kwa hatua. Kama watu hao wangejali kupata chochoe, basi wangejikwaa kwa muda fulani hatimaye wangejifunza. Lakini, ama wakati wa Mtume[saw] kulikuwa na hali hii kwamba mtu fulani alipofanya kosa fulani, basi ingawa kwa kuelezwa kwa ishara na Mtume[saw] kwamba haifai kujiumbua wakati Mungu Amekusitiri, lakini hata hivyo bado akalikiri kosa lake na kutokuwa na hofu ya kupewa adhabu ya kuuawa kwa kupigwa mawe, au sasa ambapo watu hao wakawa wanaona vibaya pindi wapewapo hata adhabu ndogo tu kwa ajili ya kustawisha sheria. Hivyo, kwa sababu ya Islam kutoingia ndani ya mioyo, baadhi ya watu wakawa hawajizuii kuvunja sheria na wakati mipaka ya sheria ilipokuwa ikitekelezwa wakawa wanachukia na kumlaumu Khalifa na magavana wake na kuweka mioyoni kinyongo dhidi yao na kufanya njama za kuing'oa na kuitupilia mbali nidhamu hiyo.

Sababu ya nne ya fitina hii, kwa rai yangu, ilikuwa ni hii kwamba maendeleo ya Islam yalifanyika kwa njia ya kasi isiyo ya kawaida kwa kiasi hiki kwamba maadui zake hawakuweza kukadiria hapo mwanzoni. Watu wa

Makka nao, kwa kujiringia nguvu zao na dhana yao juu ya udhaifu wa Mtume[saw], wakawa wamejikalia tu hadi Makka ikatekwa na Islam kuenea Bara Arabu yote. Kaisari wa Roma na Kisra wa Iran walikuwa wakiitazama nguvu hii iliyokuwa ikichipukia kwa jicho la dharau na kubeza kama vile mpigaji mweleka mwenye nguvu amtizamavyo mtoto atambaaye akijaribu kusimama mara ya kwanza.

Dharuba moja tu ya Muhammad[saw] ikausambaratisha utawala wa Irani na dola la Kiyunani. Wakati Waislamu walipokuwa wakipambana na tawala hizo zenye nguvu ambazo kwa mamia na maelfu ya miaka zimekuwa zikiwafanya watumwa wanadamu wengine, na idadi ndogo ya majeshi ya Waislamu wenye zana chache za vita walizokuwa nazo, wakiwa wanapigana vita na idadi kubwa ya majeshi yaliyokuwa yamesheheni silaha nyingi, hadi wakati huo maadui wa Islam walikuwa wakidhani tu kwamba mafanikio ya Waislamu ni ya muda mfupi tu na karibuni mawimbi haya yatabadili mwelekeo na watu hawa wanaoibuka kama tufani watatoweka tu kama kimbunga. Lakini wakashangazwa mno wakati ambapo ndani ya miaka michache tu vikwazo vyote vikaondoka na bendera ya Islam ikaanza kupepea katika pande zote nne za dunia. Haya yalikuwa ni mafanikio ambayo yalizifanya akili za maadui zipigwe bumbuazi na kujikuta wamezama ndani ya bahari ya mshangao na mastaajabu.

Na masahaba[ra] na wafuasi wao wakaanza kuonekana kuwa si watu wa kawaida machoni mwa maadui nao wakapoteza matumaini yote. Lakini ulipopita muda fulani baada ya ushindi, na mshangao na kustaajabu kule kulikokuweko mioyoni mwao kulipopungua na walipoanza kuchanganyikana na masahaba, hofu yao ya mwanzoni na hisia yao ya hatari ikaondoka, hapo yakazalika mawazo ya kupambana na Islam na kustawisha dini zilizo batili. Hawakuwa na uwezo wa kuyakabili mafundisho matukufu ya Islam kwa dalili, tawala zao zilishafutika, na wakawa na vita moja tu waliyokuwa wakiitumia dhidi ya haki, kutumia nguvu na udhalimu ukawa umekatika, sasa ikawa imebakia sura moja tu yaani kwa kujisingizia kuwa rafiki wafanye kazi ya adui na kwa kuanzisha kidhahiri maafikiano wazalishe hitilafu. Hivyo baadhi ya watu wenye mioyo migumu ambao baada ya kuiona nuru ya Islam, wakaendelea kuwa vipofu, waliikubali Islam kwa dhahiri tu, na huku wakiwa ni Waislamu, wakaweka nia ya kuiangamiza Islam. Kwa kuwa maendeleo ya Islam yalikuwa yameambatana na Ukhalifa na haikuwezekana mbwamwitu kuwashambulia kondoo mbele ya mchungaji, hivyo ikashauriwa kwamba Ukhalifa ufutwe na kuikata kamba hii ya umoja ambayo kwayo Waislamu wote duniani wameshikamana, ili Waislamu wazikose baraka za umoja, na kutokana na kutokuwepo kwa mwangalizi, waitumie fursa hiyo kwa kuipata njia yoyote

ile ya kuziendeleza tena dini potofu na kusiwepo na hatari yoyote kudhihiri kwa ulaghai na upotofu.

Hizi ndizo zile vyanzo vinne ambavyo, kwa rai yangu, vilikuwa ndizo sababu za kuenea kwa fitina hii kubwa, ambazo zilitikisa misingi ya dola la Kiislamu katika zama za Hadhrat Uthman[ra] na zilikuja nyakati fulani juu yake ambapo adui akaanza kulifurahia jambo hili moyoni mwake kwamba paa na kuta zote za ngome hii yenye shani sasa zitaporomoka ardhini na dini hii itafutika milele, dini ambayo ilijitabiria mustakbal huu wenye shani kwamba هُوَ الَّذِیۡۤ اَرۡسَلَ رَسُوۡلَہٗ بِالۡہُدٰی وَ دِیۡنِ الۡحَقِّ لِیُظۡہِرَہٗ عَلَی الدِّیۡنِ کُلِّہٖ وَ لَوۡ کَرِہَ الۡمُشۡرِکُوۡنَ (As Saff, 61:10) Yaani, ni Mungu Aliyemtuma Mtume wake pamoja na dini ya kweli ili Aishindishe dini hiyo juu ya dini zote batili ingawa makafiri wasipende.

## Kwa Nini Fitina Iliibuka Wakati wa Hadhrat Uthman[ra]?

Mimi nimebainisha vyanzo vya asili vya fitina hiyo kutokana na matukio ya kihistoria yaliyotokea katika siku za mwisho za Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra]. Yawe sahihi au si sahihi, wenyewe mtapima baada ya kuyaelewa matukio ambayo kwayo nimetoa matokeo hayo. Lakini kabla sijayabainisha yale matukio, ninapenda pia kuongelea kuhusiana na swali hili kwamba kwa nini fitina hii iliibuka wakati wa Hadhrat Uthman[ra]? Jambo lilikuwa hivi kwamba katika zama za

Hadhrat Umar[ra] watu walisilimu kwa wingi sana. Miongoni mwa hao Waislamu wapya, wengi wao walikuwa ni wale wasioijua lugha ya Kiarabu na hivyo haikuwa rahisi kwao kujifunza dini ya Islam kama ilivyokuwa kwa Waarabu, na hata wale waliojua Kiarabu, kutokana na kuchanganyika na Wairani na Wasiria, wakawa kwa karne kadhaa mawindo ya mawazo yale machafu yaliyokuwa ni matokeo ya lazima ya utamaduni wa wakati huo. Mbali na hayo, kwa sababu ya vita walizokuwa wakipigana na Wairani na Wakristo, mara nyingi masahaba[ra] na wafuasi wao walikuwa wakitumia nguvu zao zote katika kujibu mashambulizi ya maadui vitani. Upande mmoja kuwashughulikia adui wa nje, na upande wa pili wengi wa Waislamu wapya kutofahamu Kiarabu au kuathirika na fikara za kigeni, zilikuwa ni sababu kubwa mbili za jambo hili kwamba wengi wa Waislamu wapya hawakuweza kuifahamu dini kama ipasavyo. Katika zama za Hadhrat Umar[ra], kwa kuwa mlolongo wa vita ulikuwa ukiendelea katika sehemu kubwa na kila wakati kulikuwa na hatari ya kushambuliwa na adui, watu wakawa hawakupata fursa ya kuyawazia mambo mengine. Na halafu kutokana na kuendelea kukabiliana na adui, ni dhahir kwamba jadhba ya kidini ikawa inarutubishwa mara kwa mara na hivyo kuusitiri upungufu wa mafundisho ya kidini. Hali hii hii iliendelea hata katika zama za mwanzoni za Hadhrat

Uthman[ra]. Baadhi ya vita zilikuwa zikiendelea na baadhi ya athari za awali ziliendelea kubaki ndani ya mioyo ya watu. Wakati amani ilipopatikana kwa kiasi fulani, na pia athari ya jadhba ya hapo nyuma ilipopungua, hapo ndipo udhaifu ule wa kidini ulipojidhirisha na maadui wa Islam pia wakaiona fursa hiyo kama nyota ya jaha iliyowaangukia na kujizatiti kwenye utukutu. Kwa uchache, fitina hii haikutokana na kitendo chochote cha Hadhrat Uthman[ra], bali hali hizi zingetokea katika wakati wa Khalifa yeyote yule fitina ingeibuka. Na kosa la Hadhrat Uthman[ra] ni hili tu kwamba alikalia kiti cha Ukhalifa katika zama ambapo yeye hakuhusika na kuanza kwa machafuko hayo zaidi ya Hadhrat Abu Bakr[ra] na Hadhrat Umar[ra], na ni nani awezaye kusema kwamba machafuko hayo yalikuwa ni matokeo ya udhaifu fulani wa wazee hao wawili. Mimi nashangaa kwamba ni namna gani baadhi ya watu wanasema kwamba machafuko hayo ni matokeo ya udhaifu fulani wa Hadhrat Uthman[ra] ilhali Hadhrat Umar[ra] ambaye hata hakuweza kufikiria Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra] aliitambua mbegu ya machafuko haya katika zama za Ukhalifa wake na kuwatanabahisha kwayo Makureishi kwa maneno yenye mkazo. Imeandikwa kwamba Hadhrat Umar[ra] alikuwa hawaruhusu masahaba[ra] maarufu kutoka (kwenda kupigana jihadi). Na yeyote kati yao alipomwomba ruhusa alikuwa akimwambia kwamba je ile jihadi mliyofanya pamoja na Mtume[saw]

haitoshi?[6] Hatimaye, wakati fulani, masahaba[ra] wakalalamika ndipo akawaambia: Mimi nimeichunga Islam kama vile ngamia anavyofugwa. Kwanza ngamia huzaliwa, halafu hukua, halafu huota meno mawili, halafu huwa wa meno manne halafu huwa wa meno sita, halafu hutokeza meno yake ya chonge. Sasa hebu semeni, yule ambaye meno yake ya chonge yametokeza, huyo anaweza kusubiri jambo gani tena minghairi ya udhaifu. Sikilizeni! Islam sasa imefikia kwenye ukingo wa upeo wake. Makureishi wanataka kwamba mali yote waichukue wenyewe na watu wengine wakose.[7] Sikilizeni! Maadam Umar bin Khatab yu hai, ataendelea kuwakaba Makureishi ili wasitumbukie ndani ya moto wa fitina. (Tabarii, J. 6, uk. 3025-3026, chapa ya Beirut).

Inafahamika kutokana na maneno haya ya Hadhrat Umar[ra] kwamba aliona kwa watu mawazo ya aina hii dhidi ya masahaba[ra] kwamba wao wanapata sehemu zaidi. Ndio sababu alikuwa hawaruhusu masahaba[ra]

---

[6] Alikuwa na makusudio mawili kwa haya. Kwanza lilikuwa hili kwamba kulikuwa kunapatika kundi la waalimu huko Madina na pili wazo lake lilikuwa ni kwamba kwa kuwa masahaba[ra] kutokana na kutangulia kwao kuamini na kutokana na huduma walizofanya katika zama za Mtume[saw], walikuwa wakipata hisa makhsus toka Hazina; kama watu hawa wangeshiriki kwenye vita basi wangepata hisa zingine zaidi na watu wengine wangechukia kwamba mali zote wanapata wenyewe.

[7] Yaani kwa kutangulia kwao kuamini wapate hisa na sasa pia wapate hisa kwa kufanya jihadi, basi watu wengine watakosa.

kutoka kwenda kwenye vita vya Jihadi isipokuwa wale wachache ambao bila ya uwepo wao kazi za majeshi zisingeweza kufanyika, ili watu wasiingie katika mtihani kwa kupokea kwao hisa mara mbili, na alikuwa akihisi kwamba Islam ilikuwa imefikia kwenye nukta ya juu kabisa ya maendeleo na sasa hatari inayoweza kuwepo ni ya kuporomoka tu, sio kutarajia maendeleo.

Baada ya kwisha kubainisha kwa kiasi hiki, sasa ninaeleza mlolongo ule wa matukio ambapo uhakika wa hitilafu zote zilizotokea wakati wa Hadhrat Uthman[ra] unadhihirika.

Nilieleza kwamba mwanzoni mwa Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra] hatukuona ufisadi wowote ule hadi miaka sita, bali yaonekana kwamba watu, kwa kawaida, walipendezwa naye. (Tabarii, J. 5, uk. 2840, chapa ya Beirut). Bali yafahamika kutokana na historia kwamba ndani ya kipindi hicho yeye alipendwa zaidi na watu kuliko hata Hadhrat Umar[ra]. Sio tu alipendwa bali watu walikuwa na heba yake pia, kama vile mshairi wa zama hizo akitoa ushahidi wa jambo hilo ndani ya beti zake;[8]

---

8

لَا تَأْكُلُوْا اَبَدًا جِيْرَانَكُمْ سَرَفًا اَهْلَ الدَّعَارَةِ فِيْ مُلْكِ ابْنِ عَفَّانِ
اِنَّ ابْنَ عَفَّانَ الَّذِيْ جَرَّبْتُمْ فَطِمُ اللُّصُوْصِ بِحُكْمِ الْفُرْقَانِ
مَا زَالَ يَعْمَلُ بِالْكِتٰبِ مُهَيْمِنًا فِيْ كُلِّ عُنُقٍ مِنْهُمْ وَ بَنَانِ

Tafsiri:

kwa kusema: Enyi mafasik! Msidhulumu mali za watu na kuzila ndani ya utawala wa Uthman[ra], kwa sababu Ibnu Affaan ni yule ambaye tayari mmeshapata uzoefu naye, yeye huwaua wanyang'anyi chini ya hukumu ya Kurani Tukufu na siku zote ni mwenye kuzihifadhi hukumu za Kurani Tukufu na huzitekeleza hukumu zake juu ya viungo vya miili ya watu. (Tabarii J. 5, uk. 2841, chapa ya Beirut) Lakini baada ya miaka sita, mnamo mwaka wa saba, tunaiona harakati fulani ikija, na harakati hiyo si dhidi ya Hadhrat Uthman[ra], bali ni ama dhidi ya masahaba[ra] au dhidi ya baadhi ya magavana. Hivyo, Tabarii anabainisha kwamba Hadhrat Uthman[ra] alikuwa akitilia sana maanani haki za watu. Lakini wale watu ambao hawakupata fursa ya awali ya kutangulia kujiunga na Islam, wao hawakuwa wakipata heshima sawa na wale Waislamu wa zamani kwenye vikao wala kwenye nafasi za utawala wala hawakuwa na haki sawa nao kwenye mgao wa mali. Kutokana na hayo, baada ya muda fulani, baadhi ya watu wakaanza kukosoa kupewa fadhila hiyo na wakaanza kuiona hiyo

1. Msile pasipo haki, Enyi wafisadi, (mali ya) majirani zenu, katika utawala wa Ibni 'Affaan[ra].
2. Kwa yakini, Ibni 'Affaan[ra] mliyeishamjaribu, ni mwenye kukatakata majabazi kwa hukumu ya Furkani.
3. Yeye daima akatenda sawa na Kitabu — akiwa msimamizi — katika kila shingo miongoni mwao na ncha za vyanda.

kuwa ni dhuluma. Lakini watu hawa walikuwa pia wakiwaogopa Waislamu na wakawa hawadhihirishi mawazo yao kwa hofu ya kupingwa na watu, bali waliitumia njia hii kwamba kwa siri wakawa wanawahamasisha watu dhidi ya masahaba[ra]. Na walipokuwa wakimpata Mwislamu asiyejua uhakika au bedui yeyote aliyeachwa huru toka utumwani, basi wakawa wanawatolea manung'uniko yao, nao kutokana na kutotambua kwao au wenyewe kwa kusudio la kupata nafasi fulani, baadhi ya watu wakawa wanashirikiana nao. Polepole idadi ya watu wa kundi hili ikaanza kuongezeka na hatimaye kuwa kubwa. (Tabarii, J. 5, uk. 2849-2850, chapa ya Beirut)

Fitina yoyote inapotaka kutokea, basi sababu zake pia huanza kukusanyika visivyo kawaida. Huku baadhi ya watu wenye silika za husuda walianza kuhamaki dhidi ya masahaba[ra] na huko ile jadhba ya Islam ambayo mwanzoni huwemo ndani ya kila moyo wa mwenye kubadili dini ikaanza kupungua ndani ya mioyo ya Waislamu hao wapya, ambao hawakupata fursa ya kukaa pamoja na Mtume[saw] wala hawakupata fursa ya kukaa sana na wale watu waliopata fursa ya kukaa na Mtume[saw], bali waliposilimu tu wakadhani kwamba tayari wameshajifunza kila kitu. Jadhba ya Islam ilipopungua tu, ule mwelekeo wa Islam uliokuwa mioyoni mwao ukapungua na halafu wakaanza tena

kufurahia maasi yale waliyokuwa nayo kabla ya kusilimu. Walipopata adhabu ya makosa yao waliyoyatenda, basi badala ya kujirekebisha wakawa wenye mwelekeo wa kuwaharibu wale waliowaadhibu na hatimaye wakathibitika kuwa ni waundaji wa kikwazo kikubwa katika umoja wa Kiislamu. Makao Makuu ya watu hao yalikuwa ni (mji wa) Kufa, lakini jambo la ajabu kabisa ni hili kwamba Madina kwenyewe kulitokea tukio la aina fulani ambalo kwalo inakuja fahamika kwamba wakati huo baadhi ya watu walikuwa hawaifahamu Islam kama vile siku hizi baadhi ya watu majahili waishio ndani ya kiza totoro. Humran ibn Abaan alikuwa ni mtu aliyemuoa mwanamke fulani aliyekuwa ndani ya eda yake. Hadhrat Uthman[ra] alipofahamu jambo hili, alimkasirikia na kumtenganisha na mwanamke yule na mbali na hayo akamfukuza Madina mtu yule na kumpeleka Basra (Tabarii, J. 6, uk. 2923, chapa ya Beirut). Inafahamika, kutokana na tukio hili, kwamba ni jinsi gani baadhi ya watu kwa kusilimu tu wakajiona wao wameshakuwa wanazuoni wa Kiislamu na hawakuona haja ya kufanya utafiti zaidi au hivi kwamba chini ya fikara mbali mbali zisizo za dini wakadhani kuitekeleza sheria kuwa ni kitendo cha kipuuzi. Hili ni tukio moja tu na yumkini ndani ya Madina ambayo ilikuwa ndio Makao Makuu ya Islam hakukuwa na mtu mwingine asiyejua wa aina hii minghairi ya huyo. Lakini ndani ya miji mingine baadhi ya watu walikuwa wanaendelea

kuzidi katika maasi. Hivyo, inafahamika kutokana na hali zilizokuwepo huko Kufa kwamba kundi moja la vijana likawa linafanya ujambazi. Imeandikwa kwamba wakati fulani watu hao walidhamiria kwenda kufanya ujambazi katika nyumba ya mtu fulani aliyeitwa Ali bin Haismaan Al Khuza'ii na wakati wa usiku walipasua sehemu ya ukuta wa nyumba yake ili kuingia ndani. Yeye alifahamu na kutoka nje na upanga. Lakini alipowaona kuwa ni wengi akapiga mayowe (ya kuomba msaada). Hapo watu hao wakamwambia: Nyamanza! Tutaiondoa hofu yako yote kwa dharuba moja tu, na wakamuua. Wakati huo huo majirani wakagutuka na kukusanyika na wakawakamata majambazi hao. Hadhrat Abu Shuraih[ra] aliyekuwa sahaba wa Mtume[saw] na pia jirani ya mtu huyo na ambaye aliiona hali yote hiyo akiwa ukutani kwake, yeye alitoa ushahidi kwamba kweli ni watu hao hao ndio waliomuua Ali na halikadhalika mtoto wake pia alitoa ushahidi, na habari hiyo akiandika akampelekea Hadhrat Uthman[ra]. Yeye akatoa fatuwa ya wote hao kuuawa, na Walid bin Utbah, aliyekuwa siku hizo gavana wa kufa aliyewekwa na Hadhrat Uthman[ra] akawaua majambazi wote hao katika uwanja nje ya lango kuu la mji (Tabarii, J. 5, uk. 2840-2841, chapa ya Beirut). Kwa dhahir hili huonekana kuwa ni tukio la kawaida tu, lakini kwa kutazama hali za zama hizo inafahamika kuwa halikuwa tukio la kawaida. Kadiri Islam ilivyoendelea, mlolongo wa maasi ukawa

umekatika kabisa na watu wakawa katika amani kiasi hiki kwamba wakawa hata hawana hofu ya kulala milango wazi. Hata kwamba Hadhrat Umar[ra] akawakataza magavana kujenga sehemu za kuweka walinzi. Ingawa kwa agizo hili makusudio ya Hadhrat Umar[ra] yalikuwa ni kwamba watu waweze kuyafikisha kwa urahisi malalamiko yao kwa magavana, lakini agizo hili lingeweza tu kutolewa wakati ambapo amani ilikuwa imefikia kipeo. Halafu katika tukio hili jambo makhsus lilikuwa ni hili pia kwamba watoto wa watu wenye nguvu na wenye mali nao pia walishiriki katika ujambazi huu, ambao walikuwa ni watu wenye hadhi katika maeneo yao. Hivyo, tukio hili halikuwa tukio la kawaida, bali lilikuwa linaashiria kwenye mapinduzi makubwa ambayo yangewezaje kuwa nini minghairi ya haya kwamba ile taadhima ya Islam iliyokuwemo ndani ya mioyo ya watu wasiojua sasa ilikuwa inapungua na sasa wao wanarejea tena kwenye tabia zao. Na sio maskini tu, bali hata matajiri nao walikuwa tayari kujipatia heshima zao za zamani kwa njia ya mauaji. Hadhrat Abu Shuraih[ra] aliyekuwa sahaba wa Mtume[saw], alilifahamu vema jambo hili na wakati huo huo akauza miliki zake zote na kurejea Madina pamwe na ahali zake na kuacha kuishi Kufa. Kuhama kwake Kufa kwa sababu ya tukio hilo kunatoa ushahidi tosha wa jambo hili kwamba mfano huu wa pekee ulikuwa unatoa

ishara ya matukio ya hatari ya siku zijazo. Katika siku hizo hizo fitina nyingine ikaanza kujitokeza.

Abdullah bin Sabaa alikuwa Myahudi fulani ambaye kwa sababu ya mama yake akawa anaitwa Ibnus Saudaa. Alikuwa mwenyeji wa Yemen na alikuwa ni mwenye mawazo maovu sana. Baada ya kuyaona maendeleo ya Islam, akasilimu kwa lengo hili kwamba kwa namna fulani aingize fitina ndani ya Waislamu. Kwa rai yangu, fitina za zama hizo, zinatokana na mtu huyu mfisadi, naye ndiye alikuwa roho ya hizo. Inaonekana kuwa mwelekeo wake kwenye shari ulikuwa umeingia kwenye asili yake. Kufanya njama za siri ilikuwa ndio tabia yake na alikuwa na umahiri mkubwa wa kuwatambua watu wa kumfaa yeye. Alikuwa akiongea na kila mtu kulingana na tabia ya mtu huyo na alikuwa akihamasisha uovu nyuma ya pazia la wema na kutokana na sababu hii hii watu makini wakawa wanadanganyika naye. Yeye alisilimu ndani ya nusu ya kwanza ya Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra] na akazitembelea nchi zote za Kiislamu kwa lengo la kuzifahamu mwenyewe hali za kila sehemu. Hakuweza kufanikiwa ndani ya mji wa Madina. Mji wa Makka, kwa wakati huo, ulikuwa umejitenga kabisa na siasa. Mbali na makao ya Ukhalifa (Madina), makao makuu ya kisiasa kwa wakati huo yalikuwa ni Basra, Kufa, Damaskas na Fustat. Kwanza aliyatembelea maeneo hayo na akatumia mwenendo huu

kwamba akawa anawatafuta wale watu waliokuwa wameadhibiwa na kwa sababu hii walikuwa na usongo na serikali, na kukutana nao na kufikia kwao tu. Hivyo, kwanza kabisa aliendа Basra na kufikia kwa jambazi Hakim bin Jabalah aliyezuiliwa nyumbani, na kuanza kuwakusanya watu wenye mwelekeo kama wake na kuunda kikundi chao. Kwa kuwa kazi ndio ilikuwa inaanza na mtu huyu alikuwa ni mwerevu, hakuwa anaeleza jambo wazi wazi, bali alikuwa akiwaita kwenye fitina kwa ishara. Na kama vile daima alikuwa ameshika njia yake, aliendelea kutoa mawaidha na nasaha, na kuwa hiyo akapata kuheshimika ndani ya mioyo ya watu hao na wakaanza kuyakubali maneno yake. Mkuu wa Mkoa wa Basra, Abdullah bin 'Aamir, alipopata habari zake, akamuuliza hali yake na sababu ya kuja kwake. Akamjibu kwa kumtumia ujumbe akisema: 'Mimi ni mtu ninayetokana na Watu wa Kitabu ambaye nimependezwa na Islam, nami napenda kuishi chini ya hifadhi yako.' Kwa kuwa Abdullah bin 'Aamir alikuwa ameshapata taarifa ya hali halisi, hivyo hakuukubali udhuru wake na akamwambia: 'Habari nilizo nazo kuhusiana nawe ni kinyume na hayo, kwa hiyo utoke kwenye eneo langu.' Kwa hiyo, akaondoka Basra na kwenda Kufa. (Tabarii, J. 6, uk. 2922, chapa ya Beirut), lakini akawa ameshapanda mbegu ya ufisadi, uasi na chuki dhidi ya Islam ambayo baadae ikastawi na kuwa mti mkubwa.

Kwa rai yangu, hili lilikuwa ni kosa la kwanza kabisa la kisiasa lililotokea. Kama Mkuu wa Basra, badala ya kumfukuza, angemkamata na kumfunga kwa kumuweka hatiani basi pengine fitina hiyo ingeminywa hapo hapo. Ibnu Saudaa alipotoka tu nyumbani kwake alikuwa na nia hii kwamba awashe moto wa fitina ya uasi akitembelea ulimwengu wote wa Kiislamu. Kuondoka kwake Basra kuliafikiana kabisa na dhamira yake. Alipofika Kufa akaanza tena zile zile harakati zake za Basra na hatimae huko pia akafukuzwa, lakini hapa pia akawa ameshapanda mbegu ya ufisadi wake ambayo baadaye ikawa mti mkubwa sana. Na kufukuzwa kwake wakati huu likawa limefanyika tena kosa lile la kwanza la kisiasa. Mtu huyu alipotoka Kufa akaenda Shamu lakini huko hakupata fursa yoyote ya kuimarika. Huko Hadhrat Muawiya[ra] alikuwa akitawala kwa ustadi kiasi hiki kwamba hakuwapata watu ambao angeweza kufikia kwao wala hakuwapata watu ambao wangekuwa wawakilishi wake. Hivyo, akalazimika kuondoka Shamu kwa huzuni na kukata tamaa na kuendelea mbele na safari yake na kuelekea upande wa Misri. Lakini kabla ya kuondoka Shamu akawa ameshaibua fitina nyingine.

Hadhrat Abu Dhar Ghifari[ra] alikuwa ni miongoni mwa masahaba[ra] wa mwanzoni wa Mtume[saw] na alikuwa ni sahaba mwema mno na mcha Mungu. Tangu aamini alidumu kuzidi kumpenda Mtume[saw] na akaishi naye

kwa muda mrefu. Kama vile kila mtu anayo tabia yake tofauti, yeye alipozisikia nasaha hizi za Mtume[saw] kwamba mwaminio anatakiwa aishi kwa kujitenga na dunia, basi yeye, kulingana na tabia yake, akawa anafahamu kuwa haijuzu kukusanya mali na akawa anauchukia utajiri na akawa pia akiwafahamisha watu wengine kuwa haifai kukusanya mali, chochote alicho nacho mtu anapaswa kuwagawia masikini. Lakini tabia yake hii ilikuwa ni ya tangu mwanzo. Na hata katika zama za Hadhrat Abu Bakr[ra], Waislamu walipoupata utajiri, yeye alikuwa akitenda hivi hivi. Ibnu Saudaa alipokuwa akipita huko Shamu, alipoiona ndani mwake (Abu Dhar[ra]) jadhba makhsus ya kuupinga utajiri, na kufahamu kwamba anawataka matajiri wazigawe mali zao kwa maskini, basi alipokuwa akipita huko Shamu akakutana na Hadhrat Abu Dhar[ra] aliyekuwa akiishi huko wakati huo na kumwambia: 'Tazama, ni chukizo kiasi gani! Muawiya alikuwa akizisema mali za Baitul Mal (Hazina) kuwa ni mali za Allah; ina maana gani kuweka sharti ya mali za Baitul Mal, kila kitu ni cha Mwenyezi Mungu. Sasa kwa nini yeye hasa anazisema mali hizo kuwa ni za Mwenyezi Mungu? Ni kwa sababu hii tu kwamba aipoteze haki ya Waislamu iliyomo ndani ya mali hiyo, na akiyaondoa jina lao apate kuzila mali hizo. Hadhrat Abu Dhar[ra] tangu mwanzo alikuwa anawashawishi watu kwamba matajiri wanapaswa kuzigawa mali zao zote kwa maskini kwa sababu

sehemu ya kustarehe kwa ajili ya mwaminio ni Akhera tu, na alikuwa haifahamu kabisa nia na fitina ya mtu huyo. Hivyo akadanganywa na mtu huyo na kudhani kwamba kweli si sahihi kuziita mali za Baitul Mal kuwa ni mali za Allah, humo mnakuwa na hatari ya kuzifisidi mali. Ibnu Saudaa, kwa njia hii, akawa amemlipia kisasi Hadhrat Muawiya[ra] katika jambo hili kwamba kwa nini hakumpa nafasi ya kutekeleza dhamira yake huko Shamu (Siria). Hadhrat Abu Dhar[ra] akafika kwa Muawiya[ra] na kumfahamisha: 'Wewe waziita mali za Waislamu kuwa ni mali za Allah!' Yeye akajibu: Ee Abu Dhar! Mwenyezi Mungu Akuhurumie, je sisi sote si waja wa Mungu? Mali hizi si za Mwenyezi Mungu? Na viumbe vyote sio viumbe vya Mwenyezi Mungu? Na hukumu haiko mikononi mwa Mwenyezi Mungu? Yaani, wakati waja pia ni wa Mwenyezi Mungu na maagizo yatolewayo pia ni yake, sasa tena haki za watu zawezaje kupotea kwa kuziita mali hizo kuwa ni mali za Mwenyezi Mungu? Zile haki Alizoziainisha Mwenyezi Mungu, watazipata viumbe wake sawa na maagizo Yake. Jibu hili lilikuwa murua kiasi hiki kwamba Hadhrat Abu Dhar[ra] hakuweza kabisa kutoa jibu lake, lakini kwa kuwa alikuwa na jadhba makhsus katika suala hilo na Ibnu Saudaa alikuwa ameshatia shaka fulani ndani ya moyo wake, kwa hiyo, kwa tahadhari, akampatia Hadhrat Muawiya[ra] ushauri huo huo kwamba aachane na neno hili. Hadhrat Muawiya[ra] akajibu

kwamba "mimi sintosema hata kidogo kuwa mali hiyo si ya Mwenyezi Mungu naam tangu sasa nitakuwa nikiziita mali za Waislamu. Ibnu Saudaa alipoona silaha hii kwa kadiri fulani imefanya kazi, basi akawafikia masahaba[ra] wengine na kutaka kuwachochea, lakini wao hawakuwa watu wapweke kama alivyokuwa Hadhrat Abu Dhar[ra]. Walikuwa wakizifahamu hila za mtu huyu. Abu Dardaa[ra] alipoyasikia tu maneno yake akasema: Wewe u nani usemaye maneno kama haya ya kuleta fitina; kwa haki ya Mwenyezi Mungu wewe ni Myahudi. Alipokata tamaa kwa mtu huyu, akamfikia kiongozi wa Ma-Ansaar aliyekuwa mtu wa karibu sana na Mtume[saw] aliyeitwa 'Ubada bin Samit na kumuambia maneno fulani ya fitina. Hadhrat 'Ubada bin Samit akamkamata na kumpeleka kwa Hadhrat Muawiya[ra] na kumuambia huyu ndiye yule mtu aliyemtuma kwako Abu Dhar Ghifari. Ibnu Saudaa alipoona kazi yake haifanikiwi huko Sham basi akaelekea Misri na huko maneno yake yakawa yamejaa jadhba mpya ndani ya moyo wa Hadhrat Abu Dhar[ra] na kwa nguvu zaidi kuliko hapo mwanzo, akawapa Waislamu nasaha kwamba wote wazigawe mali zao kwa watu. Usemi huu wa Hadhrat Abu Dhar[ra] kwamba mtu yeyote hastahili kujilimbikizia mali, si sahihi, kwa sababu masahaba[ra] hawakuwa wakijilimbikizia mali, bali daima walikuwa wakizigawa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu. Naam, bila shaka wao walikuwa ni matajiri, na huko hakusemwi

kuwa ni kujilimbikizia mali. Kulimbikizia mali ni kutozitumia mali hizo katika kuwasaidia maskini na kutotoa sadaka. Hata wakati wa Mtume[saw] mwenyewe, baadhi ya masahaba[ra] zake walikuwa ni matajiri. Kama wangekuwa si matajiri, Hadhrat Uthman[ra] angewezaje kutoa masurufu ya safari kwa ajili ya maaskari elfu kumi wakati wa vita vya Tabuk? Lakini Mtume[saw] hakuwaambia chochote watu hao, bali watu wengine baadhi yao walikuwa ni watu wake wa karibu. Kwa uchache, kuwa mwenye mali hakukuwa ni kosa lolote, bali kulikuwa kunaafikiana kabisa na bishara za Kurani Tukufu, na Hadhrat Abu Dhar[ra] alikuwa amekosea katika suala hili. Lakini kwa hali yoyote ilivyokuwa, Hadhrat Abu Dhar[ra] alikuwa ameshikamana na mawazo yake. Lakini pamoja na hayo, lilikuwepo jambo hili kwamba alikuwa akitoa nasaha kulingana na mawazo yake lakini alikuwa hachukui sheria mkononi mwake na alikuwa akiyazingatia maagizo ya Mtume[saw]. Lakini wale watu aliokuwa akikaa na kuongea nao mambo haya hawakuutambua ucha Mungu na utakaso wake, na wakawa wanapata maana nyingine ya maneno yake. Hatimaye matokeo ya maneno haya yakawa kwamba baadhi ya maskini wakaanza kuwadhuru matajiri na kutaka kuzichukua kwa nguvu haki zao toka kwao. Wao wakashitaki kwa Hadhrat Muawiya[ra] naye akalipeleka suala hili kwa Hadhrat Uthman[ra] Hadhrat Uthman[ra] akaagiza kwamba Abu Dhar[ra] aletwe Madina kwa

heshima na taadhima. Hadhrat Abu Dhar[ra] akaenda Madina chini ya hukumu hii. Hadhrat Uthman[ra] akmuuliza: 'Kwa nini watu wa Shamu wanalalamika dhidi yako?' Yeye akajibu kuwa: "Mimi nahitilafiana nao katika jambo hili kwamba kwanza wasitamke 'mali za Allah, pili ni hili kwamba matajiri wasijilimbikizie mali." Hadhrat Uthman[ra] akasema: 'Ewe Abu Dhar! Jukumu lile alilonitwisha Mwenyezi Mungu ni kazi yangu kulitekeleza, na hii ni faradhi kwangu kwamba nizichukue zile haki zilizoko juu ya raia na kwamba niwape mafunzo ya kuihudumia dini na ya kuwa na msimamo wa wastani. Lakini hii si kazi yangu kwamba niwalazimishe wajitenge na dunia.' Hadhrat Abu Dhar[ra] akasema: 'Basi niruhusu nielekee sehemu nyingine kwa sababu Madina sasa hapanifai.' Hadhrat Uthman[ra] akasema: 'Je utaiacha nyumba hii na kuifuata ile nyumba iliyo mbaya zaidi?' Abu Dhar[ra] akajibu kwamba: 'Mtume[saw] aliniambia; "Mji wa Madina utakapoenea hadi kufikia Sal'a basi wakati huo usiishi Madina." Hapo Hadhrat Uthman[ra] akamwambia: 'Tekeleza agizo la Mtume[saw], na akampa ngamia kadhaa na watumwa wawili na kumruhusu kuondoka Madina huku akimwambia kwa msisitizo: 'Usikate moja kwa moja mahusiano na Madina, bali uwe unakuja', nasaha ambazo Hadhrat Abu Dhar[ra] alidumu kuzitekeleza. (Tabarii, J. 5, uk. 2860, chapa ya Beirut). Hii ilikuwa ni fitina ya nne iliyoibuka, na ingawa Hadhrat Abu Dhar[ra]

alitumiwa kama silaha, lakini, kwa hakika, kwenye mawazo ya Abu Dhar[ra] hakukuwepo na yale waliyokuwa nayo wafisadi na wala hakuwa akizifahamu hila za watu hao. Juu ya tofauti alizokuwa nazo Hadhrat Abu Dhar[ra] yeye hakuelekea hata kidogo kwenye kujichukulia sheria mikononi mwake na alikuwa akiitii serikali kwa namna hii kwamba ingawa kwa kuzingatia hali fulani makhsus ili kumuepusha na fitina na usumbufu, Mtume[saw] alimpa agizo la kuondoka Madina kwa wakati fulani makhsus, aliona haifai kuitekeleza hukumu hiyo bila ya kupata kwanza ruhusa ya Hadhrat Uthman[ra]. Na halafu alipoondoka Madina na kwenda kuishi Rabdha, Mkuu wa huko alipomuomba awe Imam wa kusalisha, basi alikataa kwa kumuambia: 'Wewe ndiye Mkuu wa hapa, kwa hiyo wewe ndiye unayestahili kuwa Imamu? Hii inathibitisha kwamba hakuwa kabisa akikengeuka katika utii kwa viongozi na wala hakuiona vurugu kuwa ni kitu chenye kujuzu.

Hali ya kutokuwa na makuu ya Hadhrat Abu Dhar[ra] yaweza kufahamika vyema kwa jambo hili kwamba wakati alipokuwa akigombana na Muawiya[ra] kutokana na kudanganywa na Ibnu Saudaa, kwamba mali za Baitul maal (Hazina) hazipaswi kuitwa mali ya Allah na hata akaleta mashitaka haya kwa Hadhrat Uthman[ra], yeye mara kwa mara aliendelea kutumia neno hili katika mazungumzo yake. Hivyo, baada ya ufisadi huo wakati

akiwa huko Rabdha, msafara fulani ulifika hapo. Watu wa huo msafara wakamuambia: 'Tumewaona wenzako, ni matajiri kweli kweli lakini wewe uko katika hali ya ufukara kiasi hiki!' Yeye akawajibu: اِنَّهُمْ لَيْسَ فِيْ مَالِ اللهِ حَقٌّ اِلَّا وَلِيْ مِثْلُهٗ yaani hawana haki yoyote katika mali ya Mwenyezi Mungu (Mali ya hazina) ila nami ninayo haki kama hiyo hiyo. (Tabarii, J. 5, uk. 2864, chapa ya Beirut). Halikadhalika akamuita hata Kiongozi wa eneo hilo aliyekuwa Mhabeshi kuwa ni: رَقِيْقٌ مِّنْ مَّالِ اللهِ yaani mtumwa wa mali ya Mwenyezi Mungu. Hivyo, inafahamika kutokana na hiyo kwamba hata yeye mwenyewe alikuwa akiitumia istilahi hiyo na ingawa alikuwa akilipinga neno hili, kulitamka neno hili bila kujali kunatoa ushahidi wa jambo hili kwamba masahaba, kwa kawaida, walikuwa wakiitumia istilahi hiyo, lakini kutokana na ghiliba ya Ibnu Saudaa, jambo hili likawa limemtoka akilini mwake.

Fitina hii, ambayo inafaa kuitwa fitina ya Ubolsheviki, haikuweza kung'ara huko Shamu kutokana na mbinu bora za Hadhrat Muawiya[ra], lakini kwa sura mbalimblai wazo hili likawa limeenea sehemu zingine na kuzisaidia kazi za Ibnu Saudaa.

Ibnu Saudaa aliondoka Shamu na kuwasili Misri na ni sehemu hii hii ndio akaichagua kuwa Makao Makuu ya kazi zake. Kwa kuwa sehemu hii ilikuwa mbali sana na Makao makuu ya Ukhalifa na halafu masahaba[ra]

walikuwa hawafiki sana huku, kulinganisha na sehemu zingine, ambapo kutokana na hali hiyo watu wa huko wakawa si wenye uhusiano sana na dini kama wengine na wakawa wako tayari zaidi kujihusisha na fitina. Hivyo, Naibu fulani wa Ibnu Saudaa aliyekuwa mwenyeji wa Kufa ambaye habari zake zitatajwa hapo baadaye, muda mfupi tu baada ya matukio hayo, alipofukuzwa nchini akitoa jibu la swali la Hadhrat Muawiya[ra] kwamba ni hali zipi za wanachama waliopo katika nchi mbali mbali wa kikundi kipya, alisema: 'Wamewasiliana nami kwa barua nami nimewaelewesha lakini wao hawakunielewesha. Watu wa Madina ni watu wenye kutamani sana uasi lakini ni wenye uwezo mdogo kabisa wa utekelezaji wake. Na watu wa Kufa hulaumu mambo madogo madogo lakini hawana hofu yoyote ya kujishughulisha na madhambi makubwa makubwa. Na watu wa Basra hufanya mashambulizi ya pamoja lakini husambaratika na kukimbia. Naam, ni watu wa Misri ndio wenye uwezo wa kufisidi zaidi kuliko wote, lakini ndani mwao mna kasoro hii kwamba baadae ni wepesi sana wa kujuta. Baadae akabainisha hali ya Shamu kwamba: 'Wao ni wenye kuwatii sana viongozi wao na ni wenye kutowatii kabisa wale wanaowapotosha.[9] Rai

[9] Kama vile itakavyothibitishwa hapo mbele huo ulikuwa ni uongo wake kwamba watu wa Madina walikuwa wamesalimika na fitina hii. (nyongeza wakati wa kudurusu)

hii ni ya Ibnul Kawaa aliyekuwa ni mmoja wa wanachama wa kundi la Ibnu Saudaa na kutokana na rai hii inafahamika kwamba ni Misri tu ndio palikuwa sehemu bora kabisa ambapo Ibnu Saudaa angeweza kuweka kituo, na mtazamo wake wenye kina, wa ufisadi, ukafahamu jambo hili na kumfanya apachague mahali hapa kuwa maskani yake na kupafanya kuwa Makao Makuu ya ufisadi, na kwa haraka sana akapata kundi la wafuasi wake.

Sasa katika nchi zote hizo kukawa kumestawi vituo vya ufisadi na Ibnu Saudaa akaanza, kwa hadhari na busara kubwa, kuwakusanya pamoja nae wale watu wote waliowahi kuadhibiwa au ndugu na jamaa zao au wale ambao kwa sababu yoyote ile walikuwa hawaridhiki na hali zao na alikuwa akitoa makusudio yake kwa kila mtu kulingana na tabia yake ili aipate huruma yake. Madina ilikuwa imehifadhika na ufisadi na Shamu ilikuwa imeepukana nao kabisa. Kulikuwa na vituo vitatu ambapo fitina hii ilikuwa ikitayarishwa: Basra, Kufa na Misri. Misri ilikuwa ndio Makao yao Makuu. Lakini kama wafitini wenye uzoefu wa zama hizo na wenye akili za kifalsafa, Ibnu Saudaa alijiweka nyuma ya pazia. Yeye huyo huyo ndiye alikuwa roho ya shughuli yote hiyo, lakini mbele alikuwa akiwatanguliza watu wengine. Kutokana na ukaribu na ubora wa kisiasa iliokuwa nao Kufa na Basra wakati huo, miji yote hii miwili

inaonekana kuhusika zaidi na mabadiliko hayo, lakini ikitazamwa kwa undani kidogo, basi inadhihirika kwa uwazi kabisa katika kurasa za historia kwamba hatamu ya harakati zote hizi ilikuwa mkononi mwa Ibnu Saudaa aliyekuwa ameketi huko Misri.

Mimi nimeshaeleza hapo awali kwamba huko Kufa kundi fulani la watu lilivamia nyumba ya bwana fulani aliyeitwa Ali bin Haismaan Al Khuzaa'ii na kumuua, na wauaji wakauawa kwenye lango la mji. Mababa wa vijana hao (waliouawa) walichukizwa sana na jambo hili, nao wakawa wanataka kulipiza kisasi kwa Mtawala wa sehemu hiyo, Walid bin 'Utbah, na walikuwa wakisubiri fursa itokee ili walipe kisasi. Watu hawa wakawa silaha yenye manufaa iliyokuwemo mkononi mwa kundi hilo la watu wenye kuendesha fitina, ambao waliwatumia sana. Kwa ajili ya kulipiza kisasi kwa Walid, waliwaandaa majasusi fulani ili watakapoipata aibu yoyote ile ya Walid wawafahamishe. Majasusi iliwabidi waonyeshe hatua yoyote ile. Siku moja walikuja na kuwapa taarifa kwamba Walid hunywa pombe akishirikiana na rafiki yake fulani aitwaye Abu Zubair aliyesilimu kutokea Ukristo. Waasi hao wakaibuka na kuanza kutangaza mji mzima kwamba: Mtazameni huyo kiongozi wenu, ndani kwa ndani akijificha anakunywa pombe na rafiki zake. Watu wa kawaida huwa wanashindwa kujizuia na jadhba. Kundi kubwa la watu

wakajiunga nao baada ya kuisikia habari hii na wote wakaenda kuihusuru nyumba ya Walid. Hakukuwepo na mlango wowote. Wote kwa kupitia msikitini wakaingia ndani kwa mkumbo (mlango wa nyumbani kwake ulikuwa unafungukia msikitini) na Walid akafahamu hayo wakati walipokuwa wameshamfikia. Alishtuka alipowaona na kwa haraka akakitupa kitu fulani chini ya uvungu wa kitanda. Hapo wakadhani kuwa sasa siri imefichuka na mwizi amekamatwa. Ghafla mtu mmoja bila ya hili wala lile akauingiza mkono wake uvunguni na kukitoa kitu kile. Walipoitazama wakaiona kuwa ni sahani iliyokuwa ndani yake na chakula cha Mkuu wa mkoa wa Kufa na mlikuwa pia na kicha cha zabibu, ambavyo alivificha kwa sababu tu ya kuona haya kwamba ni chakula hiki tu kilichotayarishwa kwa ajili ya Mkuu wa Mkoa ulio tajiri kabisa. Baada ya kuyaona haya ndipo watu wakatunduwaa na wote wakafedheheka na kuondoka wakilaumiana kwamba wamefanya kosa la hatari sana kwa kudanganywa na baadhi ya wakorofi na kutozingatia hukumu za sheria. Lakini Walid, kwa aibu, aliziminya habari hizo na kutomfahamisha Hadhrat Uthman[ra] jambo hili. Lakini hii ilikuwa ni huruma yake iliyofanywa kwa watu wasiostahili ambayo baadae ikaja kuthibitika kuwa na madhara makubwa sana kwake na kwa yule alishika madaraka baada yake. Waasi, badala ya kuathirika na huruma hiyo, wakajiona wamedhalilika zaidi na wakaanza kufanya njama zaidi za

kumuangamiza Walid kuliko hapo kabla na wakaenda kama ujumbe kwa Hadhrat Uthman[ra] wa kutaka Walid aenguliwe. Lakini Hadhrat Uthman[ra] akakataa kumuengua Mkuu (huyo) wa Mkoa bila ya kuwa na kosa. Watu hawa wakarejea na kuanza kuwakusanya watu wote wale waliopata kuadhibiwa na kujumuika nao na kushauriana kwamba ni lazima wamdhalilishe Walid kwa namna yoyote ile, iwe ya kweli au ya uongo. Abu Zainab na Abu Maura', ni watu wawili ambao walibeba dhima ya jambo hili kwamba wao watalitekeleza jambo hili na wakaanza kuhudhuria kwenye vikao vya Walid. Siku moja wakaipata fursa wakati ambapo kulikuwa hakuna yeyote na Walid akiwa amelala kwenye sehemu ya wanaume iliyokuwa imetenganishwa na sehemu ya wanawake kwa pazia. Watu hao wawili wakaichomoa pete yake taratibu na kukimbilia Madina na kudai kwamba wamemuona Walid akiwa amelewa, na uthibitisho wake ni hii pete ambayo tulimvua mkononi mwake wakati akiwa amelewa bila ya yeye kuwa na habari.' Hadhrat Uthman[ra] akawauliza: 'Je alikunywa pombe mbele yenu?' Hawakuwa na ujasiri wa kukiri jambo hili kwa sababu kunywa mbele yao kungethibitisha kwamba wao pia walishiriki kunywa pombe pamoja na Walid, na wakasema kwamba: 'Hapana! Tulimuona akitapika matapishi ya pombe.' Ushahidi wa jambo hili ulikuwa ni pete yake iliyokuwepo na mashahidi hao walikuwepo, na

walikuwepo pia waasi wengine waliokuja nao kuutilia nguvu ushahidi wao. Nao pia walikuwa wakilisadikisha tukio hili kwa ushahidi usio kizibiti. Ulichukuliwa ushauri wa masahaba[ra] na ikahukumiwa kuwa Walid apewe adhabu ya kisheria kwa kunywa pombe. Akaitwa toka Kufa na akapewa adhabu ya kuchapwa mijeledi huko Madina kwa kosa la kunywa pombe. Ingawa Walid alijitetea na kumfahamisha Hadhrat Uthman[ra] hila zao, lakini Hadhrat Uthman[ra] akasema: Kwa hukumu ya sheria utapata adhabu kulingana na maelezo ya mashahidi. Naam yule mwenye kutoa ushahidi wa uongo atapata adhabu ya Mwenyezi Mungu.'

(Tabraii, J. 5, uk. 2846-2847, chapa ya Beirut)

Walid akaachishwa kazi na kupakaziwa shutuma ya uongo na kwa ushauri wa masahaba, Hadhrat Uthman[ra] akamuadhibu na kwa kuwa mashahidi na ushahidi wa mazingira dhidi yake ulikuwepo, ilikuwa ni lazima aadhibiwe chini ya sheria. Said bin Al-'Aas akatumwa Kufa kuwa Mkuu wa Mkoa badala yake. Alipofika Kufa akashangaa kuiona hali ya huko. Wahuni wote na watu wasiojua dini walikuwa wameshika hatamu na watu waungwana walikuwa wamedhibitiwa na kutiishwa. Yeye akamfahamisha Hadhrat Uthman[ra] hali hii ambaye naye akatoa nasaha hii kwamba wale watu waliojitolea sana wakawa wanatangulia kufika kupambana na maadui, watendee kwa heshima; lakini ikiwa watu hao

hawaonyeshi mwelekeo kwenye dini, basi bila shaka waweke watu wengine mahali pao walio watu wa dini zaidi.

Wakati fitina hiyo ilipokuwa ikiendelea huko Kufa, Basra nako hakukuwa kimya. Huko pia, kwa kupitia Hakim bin Jabalah, mwakilishi wa Ibnu Saudaa na wenzake, wakawa wanazieneza kwa watu tuhuma za uongo dhidi ya manaibu wa Hadhrat Uthman[ra].

Misri ambayo yalikuwa hasa ndio Makao Makuu, huko ufisadi ndio ulienea zaidi. Huko Abdullah bin Sabaa hakuleta tu vurugu za kisiasa, bali alikuwa pia akiiharibu dini ya watu, lakini kwa njia hii kwamba wale Waislamu wasiojua dini wamuone kuwa muaminifu sana. Hivyo, yeye alikuwa akitoa mafundisho haya kwamba: 'Ni ajabu kwamba baadhi ya Waislamu wanaitakidi kwamba Masihi[as] atakuja tena duniani lakini hawaamini kwamba Mtume[saw] atatumwa tena ilhali Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani kwamba: اِنَّ الَّذِیۡ فَرَضَ عَلَیۡکَ الۡقُرۡاٰنَ لَرَآدُّکَ اِلٰی مَعَادٍ ؕ Yaani, Yule Mwenyezi Mungu Aliyekufaradhishia Kurani ni lazima Atakurudisha kwenye sehemu ya kurejea.[10] (Al Qasas, 28:86) Wafuasi

[10] Bishara hii ni ya ushindi wa Makka ambapo mtu huyu aliipotosha na kuifanya kuwa ni itikadi ya kurudi tena kwa Mtume[saw]. Kwa kuwa mara kwa mara watu huenda Makka kwa nia ya kuhiji na kupata thawabu hivyo jina lake pia ni Ma'ad, yaani sehemu ile ambayo watu hurudi mara kwa mara.

wake wengi waliliamini fundisho lake hili na wakakubaliana na ujio wa mara ya pili duniani wa Mtume[saw], ilhali Kurani Tukufu inakataa kwa nguvu kabisa kuja tena duniani kwa watu waliokwisha kufa. Naam, hii yawezekana kwamba kwa ajili ya kuyanawirisha majina yao, Mwenyezi Mungu Amuinue mtu fulani kwa khulka na sifa zao hizo hizo, lakini jambo hili ni tofauti kabisa na *Tanaasukh* au itikadi ya mtu kuja tena duniani na hili ni jambo lililo wazi na mashuhuri. Mbali na itikadi hiyo ya kurejea kwa Mtume[saw], Abdullah bin Sabaa alianza pia kueneza habari hii kwamba manabii elfu wamepita na kila nabii alikuwa na wasii (mrithi) wake na wasii wa Mtume[saw] ni Hadhrat Ali[ra], Mtume[saw] alikuwa Khaatamul Ambiyaa na Hadhrat Ali[ra] ni Khaatamul Ausiyaa. Halafu akawa anasema kuwa ni nani awezaye kuwa mdhalimu mkubwa kuliko yule amshambuliaye wasii wa Mtume[saw] na kumnyang'anya haki yake.

Kwa uchache, mbali na mbinu za kisiasa alizozitumia mtu huyu kwa ajili ya kuleta mfarakano ndani ya Islam, aliieneza pia fitina ya kidini na alikuwa akidhamiria kuziharibu itikadi za Waislamu, lakini alikuwa akichukua tahadhari hii kwamba watu waendelee kumfahamu kuwa ni Mwislamu.

Miaka mitatu ikapita ndani ya hali hii, na watu hawa waasi wakaendelea kufanya harakati zao kwa siri na

kulikuza kundi lao. Lakini ndani ya kipindi hicho cha miaka mitatu hakukutokea tukio lolote makhsus ila lile la Muhammad bin Abi Bakr na Muhammad bin Abi Hudhaifa, watu wawili waliokuwa wenyeji wa Madina, walijiingiza pia kiasi fulani katika fitina hii. Muhammad bin Abi Bakr alikuwa ni mwana wa mwisho wa Hadhrat Abu Bakr[ra] ambaye mbali ya sifa hii tu kwamba alikuwa ni mtoto wa Hadhrat Abu Bakr[ra], hakuwa na fadhila yoyote kidini. Na Muhammad bin Abi Hudhaifa alikuwa ni yatima fulani aliyelelewa na Hadhrat Uthman[ra] lakini alipokua akawa mpinzani wake makhsus ambapo sababu zake nitazieleza sasa hivi. Mnamo mwaka wa nne, fitina hiyo ikashika sura yenye kutisha sana na waanzilishi wake wakaona sasa inafaa kudhihirisha wazi wazi mawazo yao na kuifuta hofu ya serikali. Katika jambo hili pia ni Kufa ndiyo ikawa mwanzilishi.

Kama nilivyokwisha eleza hapo mwanzo baada ya Walid bin ‘Utbah, Said bin Al-‘Aas akawekwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kufa. Yeye tangu mwanzo alitumia njia hii kwamba alikuwa akiwaruhusu tu watu wema wa mji waje kwake, lakini wakati mwingine alikuwa pia akifanya hivi kwamba alikuwa akiita kikao cha watu wote ambamo watu wa kila tabaka, waliruhusiwa wakati huo, kuja kwake. Siku moja alikuwa ameketi kwenye kikao cha aina hii na ukatajwa ukarimu wa Hadhrat Talha[ra], na

mtu fulani akasema kwamba yeye (Hadhrat Talha[ra]) ni mtu mkarimu sana. Hapo ikatoka kauli kinywani mwa Said kwamba: 'Yeye ana mali nyingi ndio sababu anatoa, kama na sisi tungekuwa na mali basi nasi pia tungetoa hivyo hivyo.' Kijana fulani akatamka bila ya kutafakari kwa kusema: 'Laiti ardhi fulani iliyokuwa miongoni mwa mali za serikali na iliyowekwa kwa ajili ya faida ya Waislamu wote ingekuwa katika miliki yako. Hapo baadhi ya watu wa kundi hilo la fitina, ambao walikuwa wakisubiri fursa yoyote itokee wapate kutoa dukuduku lao, wakahamaki na kuanza kudhihirisha kuwa mtu huyo alitamka neno hili kwa kuashiriwa na Said, mtawala wa Kufa, na alilisema kwa sababu hii kwamba ili itayarishwe njia ya kuweza kuzitafuna mali hizo, na hivyo wakainuka na kuanza kumpiga mtu huyo mbele ya Said. Baba mtu akainuka kumuokoa mwanae naye pia akapata kipigo barabara. Said alikuwa akiwakataza lakini hawakumsikiliza hata kidogo na hivyo kuendelea kuwapiga mpaka wakazimia. Watu walipopata habari hii kwamba baadhi ya watu wamefanya ukorofi wa aina hii mbele ya Said basi wakachukua silaha na kujumuika nyumbani (kwa Mkuu wa Mkoa). Watu hao (wakorofi) wakajitupa kwa Said na kuomba msamaha na pia kuomba hifadhi kwake. Ukarimu wa Mwarabu halafu Mkureishi, ungewezaje kuvumilia katika fursa kama hii kwamba adui amuombe hifadhi halafu amkatalie. Said alitoka nje na kuwaambia watu kwamba: 'Baadhi ya

watu walikuwa wamegombana sasa hakuna chochote kila kitu ki heri. Watu wakarejea majumbani mwao na hao watu wakaanza tena kurudia ukorofi wao. Lakini Said alipokuwa na yakini kwamba sasa hakuna hatari yoyote kwa watu hao basi akawaruhusu waondoke na akawaambia wale watu waliopigwa kwamba kwa kuwa watu hao nilishawapa hifadhi basi msiyatangaze makosa yao waila itakuwa fedheha kwangu, naam! na kuweni na yakini kwamba siku zijazo watu hawa hawataweza tena kuja ndani ya kikao changu.

Kusudio lenyewe la wakorofi hao lilikuwa limeshatimia, yaani kuleta ufisadi ndani ya nidhamu ya Kiislamu. Sasa wakiketi majumbani mwao wakaanza kutangaza mambo mabaya dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] na Said. Watu wakachukizwa sana na harakati zao hizi na wakamshtakia Said kwamba hawa wanafanya ukorofi wa aina hii na kutangaza mabaya dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] na dhidi yako na wanataka kuuvunja umoja wa Islam, sisi hatuwezi kulivumilia jambo hili, hivyo lishughulikie jambo hili.' Yeye akawaambia: 'Nyinyi wenyewe mfahamisheni Hadhrat Uthman[ra] matukio yote, hatua zitachukuliwa sawa na maagizo yake. Watu wote wenye heshima zao wakamfahamisha Hadhrat Uthman[ra] juu ya matukio yote, naye akamuagiza Said kwamba: 'Kama Viongozi wa Kufa wataafikiana na jambo hili, basi watu hao wafukuzwe hapo na

kuhamishiwa Shamu, uwapeleke kwa Amir Muawiya[ra]. Huku akamuandikia Amir Muawiya[ra] kwamba: 'Watu fulani ambao wamejiandaa kufanya ufisadi kwa uwazi kabisa watakuja kwako wakitokea Kufa. Waandalie maskani yao na ujaribu kuwarekebisha. Kama wakijisahihisha na kujirekebisha basi uwatendee kwa upole na uyamezee makosa yao ya nyuma na kama watang'ang'ania kwenye ukorofi basi uwape adhabu ya ukorofi.

Hukumu hii ya Hadhrat Uthman[ra] ilikuwa ni ya busara mno, kwa sababu, kwa upande mmoja, kubakia kwa watu hao huko Kufa kungewaghadhabisha wale watu waliokuwa wanaujua vema uasi wao na hivyo kulikuwa na hatari kwamba isije wakapata kuwadhuru wakihamaki. Na kwa upande wa pili, kubaki kwao kulikuwa pia na madhara kutokana na kuwa kwao wenyeji wa eneo hilo na kwa kiwango fulani walikuwa pia ni watu wenye kusikilizwa. Kama wangebakia huko basi wangekuwa sababu ya kuwaharibu watu wengine.[11] Lakini hukumu hii ilitolewa katika wakati ule ambapo haikuweza kuleta faida zaidi. Kama Ibnu 'Aamir, Mkuu wa Basra, pia angeomba ushauri kwa Hadhrat Uthman[ra] kuhusiana na Ibnu Saudaa na agizo la aina hii

[11] Sehemu walikopelekwa watu hawa baada ya kufukuzwa hawakuwa na fursa ya kuwaharibu watu wa huko, kwa sababu huko waliwekwa chini ya uangalizi na ulinzi makhsus.

lingetolewa pia kwa ajili yake, basi pengine hali za baadae zingekuwa tofauti kabisa na hali hizo. Lakini hali ya Waislamu kwa wakati huo ilikuwa inataka kwamba kudra ya aina hii hii itendeke na ndivyo ikawa.

Watu hawa waliofukuzwa nchini na ambao wanapaswa kusemwa kuwa walikuwa ndio nguzo ya kundi la Ibnu Sabaa, idadi yao ilikuwa inakaribia kumi (ingawa kuna hitilafu juu ya idadi yao sahihi). Kwa kuwarekebisha, mwanzoni Hadhrat Muawiya[ra] alitumia mbinu hii kwamba aliwapa heshima kubwa na taadhima. Alikuwa akila nao chakula na mara nyingi alipopata nafasi alikuwa akiwatembelea na kuketi nao. Baada ya siku chache akawapa nasaha kwa kuwaambia: 'Nimesikia kwamba nyinyi mnawachukia Makureish,[12] haifai kufanya hivyo. Mwenyezi Mungu Aliwapa heshima Waarabu kupitia hao hao Makureish. Viongozi wenu ni ngao kwa ajili yenu, kwa hiyo msitengane na ngao. Wao wanavumilia shida kwa ajili yenu na wanawajali. Kama

---

[12] Kutokana na maneno ya Hadhrat Muawiya[ra] na majibu ya watu hao, inadhihirika kwa uwazi kabisa kwamba watu hawa hawakuwa na upinzani dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] na watawala aliowateua, bali walikuwa na husuda dhidi ya Makureish au kwa maneno mengine dhidi ya watu waliotangulia katika imani. Kama angekuwepo sahaba mwingine kuwa Khalifa mahali pa Hadhrat Uthman[ra] na wangekuwepo watawala wengine mahala pa watawala wale aliowateua Hadhrat Uthman[ra], hapo pia watu hawa wangewafanyia husuda ya aina hiyo hiyo, kwa sababu kusudio lao lilikuwa ni kupata tu utawala.

hamtaithamini hali hii, basi Mwenyezi Mungu Atawateulieni viongozi ambao watawadhulumuni mno na kutoijali subira yenu na mtakuwa ndani ya adhabu humu duniani na Akhera pia mtashiriki ndani ya adhabu ya hao wafalme madhalimu kwa sababu nyinyi ndinyi mtakuwa sababu ya wao kutawala. Baada ya kusikia nasaha hii ya Hadhrat Muawiya[ra], mmoja kati yao akajibu kwa kusema: 'Acha kuwataja Makureish, hawakuwahi hapo kabla kuwa wengi zaidi yetu wala sasa, na ngao ile uliyoitaja, ikinyang'anywa, ni sisi tu ndio tutakaoipata. Hadhrat Muawiya[ra] akasema: 'Nimefahamu kuwa nyinyi watu pia ni wapumbavu. Mimi nakuambieni mambo ya Islam nanyi mwanikumbusha zama za ujahili. Suala sio uchache au uwingi wa Makureish, bali ni la jukumu lile ambalo Islam imeliweka juu yao. Bila shaka Makureish ni wachache, lakini wakati Mwenyezi Mungu Amewapa heshima kwa dini na daima, kutokana na uhusiano wao na Makka, Mwenyezi Mungu Amekuwa Akiwalinda, hivyo ni nani awezaye kushindana na fadhili za Mwenyezi Mungu? Walipokuwa makafiri pia Aliwalinda kutokana na uhsiano wao huu kidogo na Makka. Sasa baada ya wao kuwa Waislamu wamekuwa ni wenye kuistawisha dini yake, sasa je Mwenyezi Mungu Atawaangamiza? Kumbukeni kwamba nyinyi, baada ya kuuona ushindi wa Islam mkasilimu kwa shauku, sasa Shetani anawatumieni nyinyi kama silaha yake ili

kuiangamiza Islam na anataka kutia ufa ndani ya Islam. Lakini fitina ile mtakayoiibua, Mwenyezi Mungu Atakuingizeni ndani ya fitina kubwa zaidi kuliko hiyo. Kwa rai yangu, nyinyi ni watu ambao hamstahili hata kidogo kutiliwa maanani. Wale watu waliomuandikia Khalifa kuhusiana nanyi walifanya makosa; hakuna faida yoyote inayoweza kutegemewa toka kwenu wala hasara. Baada ya kusikia nasaha zote za Hadhrat Muawiya[ra], watu hao wakasema: 'Tunakuamuru utengane na cheo chako.' Hadhrat Muawiya[ra] akasema: 'Kama Khalifa na Viongozi wa Waislamu watasema hivyo basi leo hii hii nitaachia ngazi, nyinyi ni nani wa kuingilia mambo haya? Ninakunasihini muachane na njia hii na shikamaneni na wema. Mwenyezi Mungu Hufanya Mwenyewe kazi yake. Kama kazi ingefanywa kulingana na rai yenu, basi kazi ya Islam ingeangamia. Kwa hakika nyinyi mna chuki dhidi ya dini ya Islam. Yaliyomo mioyoni mwenu ni tofauti na yaliyomo katika matamshi yenu, lakini lazima siku moja Mwenyezi Mungu Atazidhihirisha nia zenu na mipango yenu ya siri. Kwa uchache, Hadhrat Muawiya[ra] aliendelea kuwafahamisha kwa muda mrefu nao wakawa wanaendelea na upuuzi wao mpaka hatimae walipokosa majibu wakamvamia Hadhrat Muawiya[ra] na kutaka kumpiga. Hadhrat Muawiya[ra] akawakaripia na kuwaambia: 'Hapa sio Kufa, hapa ni Shamu. Kama watu wa Shamu watalifahamu jambo hili, basi hawatanyamaza kama watu wa Kufa walipoamriwa

na Said, bali watu hawataijali hata kauli yangu na watawapondeni. Baada ya kuyasema haya Hadhrat Muawiya[ra] aliondoka toka kwenye kikao hicho na kuwarejesha watu hao huko Kufa na akamuandikia Hadhrat Uthman[ra] kwamba: 'Kutokana na upumbavu na ujahili wa watu hawa, hawastahili kutiliwa maanani. Haifai kabisa kuwajali; na Said, mtawala wa Kufa, pia aandikiwe kwamba asiwajali, hao ni watu wasio na dini na ni wenye chuki dhidi ya Islam, wanataka kupora mali za wasiokuwa Waislamu waishio katika utawala wa Waislamu ambao walipa kodi, na fitina ndio tabia yao. Hawana nguvu yoyote wenyewe kuweza kuleta madhara bila ya msaada wa wengine.'

Rai hii ya Hadhrat Muawiya[ra] ilikuwa ni sahihi kabisa, lakini hakuwa akifahamu kwamba nje ya eneo lake, huko Misri, kulikuwa na roho iliyojificha ilyokuwa ikiwatumia watu wote hao na kuwa kwao majahili na mazuzu ndiko kuliisaidia kazi yake.

Watu hao walipotoka Damascus wakaachana na dhamira yao ya kuelekea Kufa, kwa sababu watu wa huko walishaufahamu ukorofi wao na wakawa na hofu kwamba huko yatawakuta madhara na hivyo wakaelekea upande wa Jazira. Mkuu wa Mkoa wa huko alikuwa ni Abdur Rahman, aliyekuwa ni mwana wa yule Jenerali mashuhuri ambaye alionyesha duniani kote mfano wenye kung'aa wa ujasiri na ushujaa, yaani Khalid bin

Walid. Wakati alipofahamu hali ya ujio wa watu hao, mara moja aliwaita na kuwaambia: 'Nimezisikia habari zenu. Mwenyezi Mungu Asinifanikishe ikiwa nitashindwa kuwarekebisheni. Nyinyi mwafahamu kwamba mimi ni mtoto wa mtu yule aliyeiondoa fitina ya kuritadi na aliyekuwa akifanikiwa katika hali ngumu ngumu. Nitaona kama mtaweza pia kuongea nami kama mlivyokuwa mkiongea na Muawiya[ra] na Said[ra]. Sikilizeni! Ikiwa mtafanya jambo lolote la fitina, nitakupeni aina ya adhabu ambayo mtadumu kuikumbuka.' Baada ya kusema haya akawaweka chini ya uangalizi na kuwaamuru daima wawe pamoja naye. Alipokuwa akisafiri alikuwa akienda nao na aliwafanya wao wawe wakitembea kwa miguu na kuwauliza: 'Sasa mna hali gani? Yule asiyejirekebisha kwa wema dawa yake ni adhabu. Nyinyi kwa nini sasa hamsemi?' Watu hao wakawa wanadhihirisha majuto na kutubia uasi wao. Baada ya muda fulani kupita katika hali hii, Abdur Rahman bin Khalid bin Walid akafikiria kuwa watu hao wamerekebika na akamtuma mmoja wao aliyekuwa akiitwa Malik, kwa Hadhrat Uthmanra na kumuambia: 'Nenda huko ukaombe msamaha.' Akaja kwa Hadhrat Uthman[ra] na kutubia na kudhihirisha majuto na pia akawaombea msamaha wenzake. Yeye akawasamehe na kuwauliza kuwa wangependa kuishi wapi. Malik akasema: Sasa tungependa kuishi kwa Abdu Rahman

bin Khalid. Hadhrat Uthman[ra] akatoa ruhusa na mtu huyo akarejea kwa Abdur-Rahman bin Khalid.

Shauku ya mtu huyo ya kutaka kuishi na Abdu Rahman yaonyesha kwamba moyo wa mtu huyo, kwa wakati huo, ulikuwa bila shaka yoyote umeshatakasika, kwa sababu kama isingekuwa hivyo, basi asingeonyesha shauku ya kurejea kwa mtu yule ambaye hakuvumilia utukutu hata kwa dakika moja. Lakini matukio ya baadae yanaonyesha kwamba toba yake ilikuwa ni ya muda tu na dhana hii ya Hadhrat Muawiya[ra] ilikuwa ni sahihi kwamba watu hawa ni wapumbavu ambao wanaweza tu kutumika kama silaha ya utendaji.

Ndani ya kipindi hicho, Abdullah bin Sabaa hakuwa amekaa kimya, bali tangu kitambo fulani yeye alikuwa amechukua mwenendo huu kwamba alikuwa anawatuma wawakilishi wake katika maeneo yote na kueneza mawazo yake. Hakuna shaka yoyote kwamba mtu huyu, kwa hakika, alikuwa ni mtu mwenye akili na werevu usio wa kawaida. Maagizo aliyowatolea wawakilishi wake yanaangazia vizuri sana muundo wa ubongo wake. Alipokuwa akiwaaga wawakilishi wake alikuwa akiwaagiza kwamba: 'Msiwe wenye papara ya kuyatoa mawazo yenu mbele ya watu, bali muwe kwanza mkitoa mawaidha na nasaha na kuwasikilizisha watu hukumu za sheria na muwe mkitoa maagizo ya mambo mema na kukataza mabaya. Watu

watakapouona mwenendo wenu huu, mioyo yao itavutiwa nanyi na kuyasikiliza kwa shauku maneno yenu na watakutegemeeni, ndipo muyatoe kwa ustadi mawazo yenu hasa, nao watayakubali kwa haraka sana. Na pia mchukue tahadhari hii kwamba mwanzoni msitamke maneno yoyote dhidi ya Hadhrat Uthman[ra], bali muwahamakishe watu dhidi ya manaibu wake. Kusudio lake kutokana na haya lilikuwa kwamba kutokana na uhusiano wao makhsus wa kidini na Hadhrat Uthman[ra], watu wangeghadhabika kusikia maneno mabaya dhidi yake, lakini kwa kuyasikia maneno dhidi ya maamiri, hisia zao za kidini hazitaathiriwa na hivyo watayakubali. Wakati nyoyo zao zitakapokuwa nyeusi kwa njia hii, na ule ukaidi uzalikao kwa kujiunga katika kundi fulani utakapozalika, basi hapo itakuwa rahisi hata kuwahamakisha dhidi ya Hadhrat Uthman[ra].

Mtu huyo alipoona kwamba kila mara mabaya ya viongozi wa mikoa yanapoelezwa, watu wenye busara wanakataa kuyakubali, kwa sababu kutokana na ushuhuda wao wenyewe, wanayafahamu madai hayo kuwa ni ya uongo na yasiyo ya uhakika, na hamaki kwa jumla haienei nchini, hivyo akatumia mbinu nyingine yenye hatari, nayo ni hii kwamba akawaagiza manaibu wake kuwa badala ya kujaribu kuwapaka matope wakuu wa mikoa katika maeneo walioko, wayaandike maovu

yao na kuyapeleka maeneo mengine, kwa sababu watu wa maeneo mengine, kwa kutoyafahamu mazingira ya maeneo husika, watayakubali maneno yao kwa urahisi. Hivyo sawa na ushauri huu, waasi wa kila sehemu wakaandika mashtaka ya uongo na dhuluma za kubuniwa dhidi ya viongozi wa maeneo yao na kuyatuma kwa watu wanaoonea huruma wa maeneo mengine, nao wakawa wanawasomea watu barua hizo, na watu wengi kwa sababu ya kutozijua hali zilizoko katika nchi hizo zingine, wengi wakawa na yakini kuwa maneno hayo ni ya ukweli na wakawa wanahuzunika kwamba ndugu zetu wa maeneo fulani na fulani wamo katika misiba mikubwa, na wakawa wanashukuru pia kwamba kwa fadhili za Allah Mkuu wetu ni mwema, hatuna matatizo yoyote, nao walikuwa hawafahamu kwamba watu wa nchi zingine walikuwa wakijifahamu kuwa wao wamo katika utulivu na kuwaona wao kuwa wamo ndani ya matatizo na kushukuru kwa hali waliyokuwa nayo na kuzihuzunikia hali zao. Kwa kuwa watu wa Madina walikuwa wakipokea barua toka pande zote, wale watu miongoni mwao waliokuwa wakizikiri barua hizo kuwa ni sahihi wakawa wanadhani kwamba pengine dhuluma zinatendeka katika nchi zote na misiba mikubwa inawaelemea Waislamu. Kwa uchache, hila hii ya uongo ya Abdullah bin Sabaa ikathibitika kufanikiwa sana, na kwa njia hii akapata maelfu ya

wanaomuunga mkono, ambao ilikuwa vigumu kuwapata bila ya hila hii.

Mkanganyiko huu ulipoanza kupita kiasi na hata masahaba[ra] nao walipoanza kupokea barua za aina hii, ambamo mlikuwa na malalamiko dhidi ya magavana, basi wakakutana na kumuuliza Hadhrat Uthman[ra]: 'Je hufahamu nini kinachotokea huko nje?' Akajibu: 'Taarifa zinazonifikia zinadhihirisha kwamba mambo ni shwari.' masahaba[ra] wakamwambia: 'Barua zenye madhumuni haya zinatufikia toka nje, zapaswa kuhakikiwa.' Hapo Hadhrat Uthman[ra] akaomba ushauri wao kwamba uchunguzi ufanyike vipi. Na kulingana na ushauri wao akamtuma Usama bin Zaid[ra] huko Basra, Muhammad bin Muslim[ra] Kufa, Abdullah bin Umar[ra] Shamu na 'Ammaar bin Yaasir[ra] akamtuma. Misri, kwamba wakafanye uchunguzi wa hali za huko na kutoa taarifa kwamba je ni kweli kuwa viongozi wanawadhulumu raia kupita kiasi na kuwanyang'anya haki zao? Na minghairi ya watu hawa wanne, akawatuma watu wengine pia katika nchi mbali mbali ili watoe taarifa za hali za huko. (Tabarii, J. 6, uk. 2943, chapa ya Beirut)

Watu hao wakaenda na baada ya kufanya utafiti wote wakatoa taarifa kuwa sehemu zote kuna amani na Waislamu wanaishi kwa uhuru kabisa na hakuna yeyote anayewanyang'anya haki zao na viongozi wanatenda

kwa uadilifu na haki. Lakini 'Ammaar bin Yaasir[ra] akachelewa kurejea, na habari yoyote haikupatikana kuhusiana naye. Kwa nini 'Ammaar bin Yaasir alichelewa, hiyo nitaitaja baadae. Kwanza ninataka kueleza kuhusiana na ujumbe huu wa watafiti na umuhimu wa uchunguzi wao. Kwa sababu kwa kuzielewa vema habari za watu hawa (waliotumwa kufanya uchunguzi) uhakika hasa wa fitina hii unadhihirika. Jambo la kwanza kabisa linalostahili kuzingatiwa ni hili kwamba viongozi wote watatu wa ujumbe huo waliorejea na kuja kutoa taarifa, walikuwa ni watu wa daraja gani. Kwa sababu hali za watu wanaofanya uchunguzi zadhihirisha thamani ya uchunguzi huo. Kama ndani ya ujumbe huo wangetumwa watu wa aina hii ambao ni watu wenye matashi fulani kwa Hadhrat Uthman[ra] au kwa manaibu wake au hali yao ya kidini na ya kidunia isingekuwa ya hali ya juu kiasi hiki ya kutokuwa na hofu ya watawala au ya kuwa na tamaa fulani kwao, basi ingeweza kusemwa kwamba watu hawa waliepuka kueleza ukweli kwa sababu ya hofu au tamaa fulani. Lakini lawama za aina hii haziwezi asilan kuwepo juu ya watu hawa. Na Hadhrat Uthman[ra] alitoa uthibitisho wa wazi wa nia yake njema kwa kuwachagua watu hawa kwa ajili ya kazi hii. Usama[ra] aliyepelekwa Basra alikuwa ni mtu wa aina hii kwamba sio tu alikuwa ni mwana wa Hadhrat Zaid[ra] aliyekuwa ni miongoni mwa waaminio wa mwanzo, bali

alikuwa ni miongoni mwa watu waliokuwa wapenzi wa Mtume[saw] na waliokuwa karibu naye. Naye ndiye yule ambaye Mtume[saw] alimpa uongozi wa jeshi lile adhimu alilokuwa akiliandaa katika maradhi yake alimofia, na humo aliwafanya kuwa chini ya uongozi wake masahaba[ra] wakubwa sana kama vile Hadhrat Umar[ra]. Na uteuzi huu wa Mtume[saw] haukuwa kwa ajili ya kumfurahisha, bali matukio ya baadae yalithibitisha kwamba alikuwa na uwezo wa kufanya mambo makubwa makubwa. Mtume[saw] alikuwa akimpenda mno kiasi ya kwamba walioshuhudia walikuwa wanashindwa kutofautisha kama alikuwa akimpenda zaidi yeye au Hadhrat Imam Hasan[ra]. Pia Muhammad bin Muslim[ra] aliyetumwa huko Kufa alikuwa ni miongoni mwa masahaba[ra] wenye shani ya juu na miongoni mwa masahaba[ra] alikuwa akitazamwa kwa mtazamo wa heshima makhsus na kuenziwa mno.

Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] aliyetumwa huko Shamu alikuwa ni miongoni mwa watu wa aina hii wasiohitaji kutambulishwa. Alikuwa ni miongoni mwa Waislamu wa zama za mwanzo, na shani yake katika utawa na ucha Mungu ilikuwa hivi kwamba hata masahaba[ra] wakubwa walikuwa wakimpa heshima makhsus kutokana na sifa zake hizo. Kama kulikuwa na sahaba yeyote baada ya Hadhrat Ali[ra] ambaye masahaba[ra] na waja wa Mwenyezi Mungu walimwelekea kwa ajili ya

Ukhalifa, basi alikuwa ni yeye. Lakini yeye alipendelea kujitenga na dunia. Katika masuala ya kidini yeye alikuwa na ghera kiasi hiki kwamba wakati mwingine alikuwa akijadiliana kwa ukali hata na Hadhrat Umar[ra] bin Khattab mwenyewe. Kwa uchache, yeye alikuwa haogopi kusema ukweli. Uteuzi wake kwa ajili ya kwenda Shamu ulikuwa ni uteuzi bora kabisa, kwa sababu kwamba Hadhrat Muawiya[ra] alikuwa mtawala wa Shamu kwa muda mrefu na watu wa huko walikuwa wakimuogopa sana na kutokana na akili nyingi alizokuwa nazo, kuufanyia utafiti uongozi wake haikuwa kazi ya mtu yeyote wa kawaida. Kumpeleka mtu mwingine sehemu hiyo kulikuwa hakuna faida na pia watu wasingeridhika na uchunguzi wake. Lakini kutokana na kiwango chake cha juu cha imani na ghera yake juu ya Islam na uhuru wa mawazo na uchamungu, zilikuwa ni sifa ambazo Muawiya[ra] asingeweza kufurukuta mbele yake wala hofu ya Muawiya[ra] isingeweza kumkumba mtu yeyote yule mbele ya mtu huyu.

Kwa uchache, wale watu waliotumwa kwenda kufanya uchunguzi walikuwa ni wenye shani ya hali ya juu na wasiokuwa na tamaa yoyote na hakuna mtu yeyote angekuwa na nafasi ya kulaumu uchunguzi wao. Hivyo, masahaba[ra] hawa watatu pamoja na wengine waliotumwa katika nchi zingine, kutoa uamuzi wa aina

moja kwamba kuna amani na utulivu kabisa nchini, hakuna alama yoyote ya dhuluma, watawala wanatenda kwa haki na uadilifu, na kama kuna lawama yoyote juu yao, basi ni hii kwamba wanawalazimisha watu kuwa ndani ya sheria, huu ni uamuzi ambao hakuna shaka yoyote inayobakia baada yake. Na inaonekana kwa uwazi kabisa kwamba fitina zote hizi zilikuwa ni ukorofi wa wakorofi wachache na matokeo ya uchochezi wa Abdullah bin Sabaa, waila Hadhrat Uthman[ra] na manaibu wake walikuwa wameepukana na kila aina ya shutuma.

Ukweli ni huu tu kwamba vurugu zote hizi zilikuwa ni matokeo ya mpango wa siri ambao waanzilishi wake hasa walikuwa ni Wayahudi ambao walishiriki pamoja nao baadhi ya Waislamu waliojiingiza kwenye tamaa ya dunia na waliokwisha toka kwenye dini. Waila viongozi wa nchi hawakuwa na kosa lolote wala hawakuwa chimbuko la fitina hii. Kosa lao lilikuwa kwa kiasi hiki tu kwamba Hadhrat Uthman[ra] aliwateua kwa ajili ya kazi hii na 'kosa' la Hadhrat Uthman[ra] lilikuwa ni hili kwamba juu ya uzee na udhaifu wa mwili aliokuwa nao aliendelea kuishikilia kamba ya umoja wa Islam na alikuwa ameubeba mzigo wa umma wa Kiislamu na alikuwa akijali kuisimamisha sheria ya Kiislamu na alikuwa hawaruhusu waasi na wadhalimu kuwadhulumu dhaifu na wanyonge jinsi watakavyo. Na jambo hili

linasadikishwa pia na tukio hili kwamba kikao fulani cha hawa hawa wapendao uasi kilifanyika huko Kufa na humo mliongelewa suala la kuwafitinisha Waislamu, basi watu wote, kwa pamoja wakatoa rai hii kwamba:

لَا وَاللّٰهِ لَا يُرْفَعُ رَأْسٌ مَا دَامَ عُثْمَانُ عَلَى النَّاسِ

Yaani, Wallahi hakuna yeyote awezaye kunyanyua kichwa maadamu Uthman[ra] anatawala. Ni dhati ya huyo huyo Uthman[ra] iliyoudhibiti uasi. Ilikuwa ni lazima kumuondoa ili kuweza kutimiza malengo yao kwa uhuru.

Mimi nilieleza kwamba ‘Ammar bin Yaasir aliyetumwa kuelekea Misri hakurejea. Habari zake zilichelewa kufika kiasi hiki kwamba watu wa Madina wakadhani labda ameuawa. Lakini hakika yenyewe ilikuwa kwamba kutokana na tabia yake ya kupendelea maisha ya kawaida na kutokana na kutofahamu kwake mbinu za kisiasa basi akanasa ndani ya makucha ya waasi hao waliokuwa wanafunzi wa Abdullah bin Sabaa. Kwa kuwa Abdullah bin Sabaa alikuwepo mwenyewe huko Misri na hakuwa ameghafilika na jambo hili kwamba ikiwa ujumbe huu wa kufanya uchunguzi utatoa uamuzi kwamba nchini kote kuna amani na utulivu, basi watu wote watakuwa wapinzai wetu. Uamuzi wa kupeleka ujumbe huu ulikuwa wa ghafla kiasi ya kwamba hawakuweza kufanya mpango wowote kwenye sehemu

zingine. Lakini mpango wa Misri ulikuwa ni rahisi kwa ajili yake. 'Ammaar bin Yasir alipoingia tu Misri akampokea na kuanza kumueleza maovu na dhuluma za mtawala wa Misri. Hakuweza kusalimika na athari za ufasaha wake na badala ya kufanya uchunguzi usioegemea upande wowote, hakwenda hata kwa mtawala wa Misri wala hakufanya uchunguzi wa kina, bali aliliendea hilo hilo kundi la waasi na kwa kuungana nao hao hao na akaanza kutoa lawama.

Miongoni mwa masahaba, kama kulikuwa na mtu yeyote aliyethibitika kwa yakini kabisa kunasa kwenye mtego wa kundi hili la waasi, basi huyo ni 'Ammar bin Yasir pekee. Mbali naye hakukuwa na sahaba yeyote maarufu aliyeshiriki katika harakati hizi. Na kama imeelezwa kushiriki kwa yeyote yule basi kwa riwaya zingine habari hii imepingwa pia. Kulikuwa na sababu moja makhsus iliyosababisha 'Ammar bin Yasir adanganywe na watu hao, nayo ni hii kwamba mara tu alipowasili Misri, kundi fulani la watu, ambao kwa dhahiri walionekana kuwa ni watu wenye kuaminika na waliokuwa wajanja na domokaya wakakutana naye na kwa ustadi wa hali ya juu kabisa wakaanza kumtolea mashtaka dhidi ya mtawala wa Misri. Kwa bahati, mtawala huyo wa Misri alikuwa ni mtu ambaye alishawahi kuwa mpinzani mkubwa wa Mtume[saw], na kuhusiana naye, wakati wa ushindi wa Makka, yeye[saw]

aliagiza kwamba mtu huyo auawe hata kama akipatikana ndani ya Kaaba. Na ingawa baadae alimsamehe, bughudha ya upinzani wake wa awali ilikuwa bado imo ndani ya mioyo ya baadhi ya masahaba, akiwemo pia 'Ammar. Hivyo, baada ya kuyasikia maneno ya watu hawa, 'Ammar mara moja akaathirika na kuzikiri kuwa ni sahihi shutuma zile alizoshitakiwa, Wasabai yaani wenzi wa Abdullah bin Sabaa, wakaitumia fursa hiyo kwa kulisisitizia sana jambo hilo dhidi yake. Hivyo, nia njema na uhalisia wa Hadhrat Uthman[ra] unaweza kukadiriwa kwa hali hii kwamba ingawa wajumbe wote ukimuondoa mtu mmoja, waliwatolea hukumu watawala ya kutokuwa na hatia, Hadhrat Uthman[ra] akaithamini rai hii moja iliyokuwa kinyume na akatuma barua kwa watu wa maeneo yote, ambayo madhumuni yake yalikuwa haya kwamba tangu nimekuwa Khalifa, matendo yangu yamekuwa ni kuamuru mema na kukataza maovu, na ndugu na jamaa zangu hawana haki zaidi ya Waislamu wengine. Lakini nimefahamu kutoka kwa baadhi ya watu waishio Madina kwamba watawala wanawapiga watu na kuwatukana. Hivyo, kwa kupitia barua hii, ninawatangazia watu wote kwamba yeyote yule aliyetukanwa faraghani au kupigwa, huyo akutane nami wakati wa Hija huko Makka na dhuluma yoyote aliyotendewa, iwe kwa mikono yangu au kwa mikono ya watendaji wangu, alipize kisasi kwangu au kwa watendaji wangu, au asamehe, Mwenyezi Mungu Huwapa malipo

watoao sadaka. Barua hii fupi, lakini yenye kutia uchungu, iliposomwa kwenye mimbari katika nchi zote, basi ulimwengu wa Islam ukatikisika kuanzia kona moja hadi nyingine na wasikilizaji wakashindwa kujizuia na kulia na wote wakamuombea dua Hadhrat Uthman[ra] na wakadhihirisha masikitiko yao dhidi ya waeneza fitina waliokuwa wakimshambulia yule mtu aliyekuwa na uchungu na umati wa Kiislamu na aliyeubeba mzigo wake. (Tabarii, J. 6, uk. 2944, chapa ya Beirut)

Hadhrat Uthman[ra] hakuishia hapo, bali akawataka watendaji wake watoe majibu makhsus ya shutuma zile zilizoelekezwa kwao. Wakati watawala wote walipojumuika, akawaambia: "Kuna nini kwamba nyinyi mnalalamikiwa? Hofu yanijia kwamba isije ikawa mambo haya yakawa ni sahihi. Hapo wote wakamjibu kwamba wewe ukiwatuma watu wanaoaminika, umeishatambua kuwa hakuna dhuluma yoyote inayofanyika wala hakuna dhuluma yoyote, wala hakuna kazi yoyote iliyo kinyume cha sheria, na watu wale wenye kuaminika uliowatuma, waliwauliza watu wote hali ya mambo, hakuna hata mtu mmoja aliyejitokeza kulalamika kuhusiana na hayo yaliyoelezwa, sasa inabakia nafasi gani ya kushuku? Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, watu hao hawakusema ukweli wala hawakutumia ucha Mungu, na lawama zao hazina uhakika wowote, haiwezi kujuzu kumshika mtu kwa

mambo haya yasiyo na msingi na yasiyoweza kutegemewa.

Hadhrat Uthman[ra] akasema: 'Basi nishaurini nini kifanyike.' Hapo akapewa ushauri wa aina mbali mbali ambao muhtasari wake ulikuwa huu huu kwamba: 'Inapobidi kutumia ukali basi utumie ukali na usiwape waasi hao ulaini wa aina hii, kwani kwa kufanya hivyo wanazidi kuwa majasiri. Ni adhabu tu inayoweza kumrekebisha mtu mkorofi; upole atendewe yule ambaye upole utamnufaisha. Baada ya kusikia ushauri wa wote, Hadhrat Uthman[ra] akasema: 'Zile habari za fitina alizokwisha zieleza Mtume[saw], hizo lazima zitatokea, naam, kwa muda fulani, zinaweza kusitishwa kwa upendo na upole. Hivyo mimi, nitaendelea kuwatendea kwa upole, ila kwa yale tu yanayokiuka sheria za Allah, ili mtu yeyote asiwe na hoja ya kweli dhidi yangu. Mwenyezi Mungu Anajua kuwa mimi nilifanya kila lililowezekana kuwatendea watu mema. Abarikiwe Uthman[ra] kama afe kabla ya kuanza kwa mafuriko ya fitina yatakayoikumba Islam. Hivyo, nendeni mkawatendee watu kwa upole na muwape haki zao na muyamezee makosa yao. Naam, kama mtu yeyote yule azivunje sheria za Mwenyezi Mungu, basi watu wa aina hiyo wasitendewe kwa upole na msamaha.

Aliporejea kutoka Hija, Hadhrat Muawiya[ra] pia alikuja Madina pamoja na Hadhrat Uthman[ra]. Alikaa kwa siku

chache na alipotaka kurejea, akakutana faraghani na Hadhrat Uthman[ra] na kumuomba kwamba: 'Inaonekana fitina inaongezeka, kama iko ruhusa basi ningependa kuongea machache kuhusiana nayo.' Akasema: 'Ongea.' Hapo yeye akasema: 'Kwanza ushauri wangu ni huu kwamba twende pamoja nami huko Shamu kwa sababu Shamu kuna kila aina ya amani na hakuna aina yoyote ile ya ufisadi, isije ikaibuka ghafla aina yoyote ile ya uasi, halafu kukawa hakuwezekani kufanyika mpango wowote ule. Hadhrat Uthman[ra] akamjibu: 'Mimi, kwa sura yoyote ile, siwezi kuuacha ujirani wa Mtume[saw] hata kama mwili wangu ukatwe vipande vipande. Hadhrat Muawiya[ra] akasema: 'Basi ushauri wangu wa pili ni huu, niruhusu nitume kikosi cha jeshi la Shamu kwa ajili ya kukulinda, hakuna yeyote atakayeweza kufanya ukorofi mbele ya watu hao. Hadhrat Uthman[ra] akajibu: 'Siwezi kuitupia Baitul Maal mzigo wa aina hii kwa ajili ya kuulinda uhai wa Uthman wala sipendi kuwadhikisha watu wa Madina kwa kuwawekea jeshi. Hapo Hadhrat Muawiya[ra] akasema: 'Basi ushauri wa tatu ni huu kwamba wakiwepo masahaba[ra] basi watu hawa wanao ujasiri wa kumteua yeyote miongoni mwao (masahaba) kama Uthman[ra] asiwepo. Watawanye watu hao (masahaba) katika nchi mbali mbali.' Hadhrat Uthman[ra] akajibu: 'Hii yawezekanaje kwamba mimi niwatawanye wale watu ambao Mtume[saw] aliwakusanya?' Hapo Muawiya[ra] akalia na kusema: 'Ikiwa hukubaliani na

mpango wowote kati ya hiyo mipango ya kukulinda niliyoitoa, basi angalau ufanye hivi kwamba uwatangazie watu kuwa kama nafsi yangu itadhurika basi Muawiya atakuwa na haki ya kunilipizia kisasi, huenda watu wakaihofia hiyo na kujiepusha na ukorofi. Hadhrat Uthman[ra] akasema: 'Muawiya! Kilichokadiriwa kutokea kitatokea tu. Mimi siwezi kufanya hivyo, kwa sababu wewe ni mtu mkali, isije ukawasumbua Waislamu.' Hapo Hadhrat Muawiya[ra] akainuka ili kuondoka huku akilia na kusema: 'Ninafahamu huenda huu ukawa ni mkutano wetu wa mwisho,' Baada ya kutoka nje akawaambia masahaba: 'Uhai wa Islam unakutegemeeni nyinyi, Hadhrat Uthman[ra] sasa amekuwa dhaifu kabisa na fitina inaongezeka, kuweni waangalizi wake.' Baada ya kusema hayo, Muawiya[ra] akaelekea Shamu.

Kutokuwepo kwa Wakuu wa mikoa katika maeneo yao haikuwa fursa ya kuachwa na Abdullah bin Sabaa ipite hivi hivi. Mara moja yeye akatuma barua sehemu zote kwamba: 'Hii ndio fursa, tunapaswa kufanya chochote wakati huu, teueni siku moja ya kuwashambulia kwa ghafla watawala wa maeneo yenu.' Lakini watawala wakawahi kurudi walipokuwa bado wakishauriana. Wasabai wa maeneo mengine wakakata tamaa lakini Wasabai (yaani wafuasi wa Abdullah bin Sabaa) wa Kufa, ambao tangu mwanzoni walikuwa na tabia ya kuwa mbele mbele katika uasi, wao hawakuiachilia fursa

hii iwaponyoke. Mtu mmoja aliyeitwa Yazid bin Qais alifanya mkutano ndani ya msikiti wa Kufa na kutangaza kwamba sasa Hadhrat Uthman[ra] anapaswa kuondolewa kwenye Ukhalifa. Qa'qaa' bin Amr[ra], aliyekuwa Afisa wa jeshi wa eneo hilo, aliposikia hayo alikuja kutaka kumkamata. Yeye akatoa udhuru mbele ya afisa huyo kwa kusema: 'Mimi siko nje ya utii. Sisi tumejumuika tu kwa sababu hii kwamba tufanye mkutano kuhusiana na Said bin Al 'Aas kuwa aondolewe hapa na kuletwa afisa mwingine.' Akasema hakukuwa na haja ya kufanya mkutano kwa hilo, yaandikeni malalamiko yenu na kuyatuma kwa Hadhrat Uthman[ra]. Yeye atamteua mtu mwingine kuwa mtawala na kumtuma, kuna uzito gani katika jambo hilo.' Maneno haya aliyasema kwa sababu hii kwamba katika zama za ukhalifa, kwa kutilia maanani utulivu wa watu, kulipokuwa kukitokea tatizo lolote dhidi ya mtawala, basi mara nyingi alikuwa akibadilishwa. Baada ya kusikia jibu hili la Qa'qaa', kwa dhahiri, watu hawa walitawanyika, lakini wakawa wanafanya mipango kwa siri. Hatimaye Yazid bin Qais, ambaye kwa wakati huo alikuwa ndiye kiongozi wa Wasabai wa huko Kufa, alimpa mtu fulani barua na kuituma huko Hims na kusema kwamba wale watu waliofukuzwa huko Kufa — na ambao tukio lao limeelezwa hapo awali — awalete. Yeye akaichukua barua hiyo na kuwaendea watu hao. Madhumuni ya barua hiyo yalikuwa hivi kwamba: 'Watu wa Misri

wameungana nasi na fursa imekuwa nzuri sana. Itakapowasili tu barua hii mrejee bila ya kuchelewa hata dakika moja.'

Ni jambo la ajabu kiasi gani kwamba wale wenye kumpinga na kumkosoa Khalifa wa zama aliyetangulia katika kuipokea imani na aliyekuwa mume wa binti ya Mtume[saw], wawe ni wale wenye kuacha sala. Yawezekanaje kwamba ghera ya Islam izalike kwa wale tu wasio na dini? Kama kweli kungekuwa na kasoro kwa Hadhrat Uthman[ra] au kwa viongozi wake aliowateua, kama kungekuwa na jambo lolote lililo kinyume na sheria, kama kungekuwa na udhaifu wowote, basi watu ambao wangeonyesha jadhba ya kupinga wangekuwa ni Ali, Talha, Zubair, Saad bin Al Waqqas, Abdullah bin Umar, Usama bin Zaid, Abdullah bin Abbas, Abu Musa Ash'ari, Hudhaifa bin Al-Yamaan, Abu Huraira, Abdullah bin Salaam, 'Ubada bin Samit na Muhammad bin Maslama[ra] — Mungu awe radhi nao — na sio Yazid bin Qais na Ashtar.

Mjumbe aliichukua barua hii na kuwasili Jazira na kuwakabidhi wale waliofukuzwa Kufa. Walipoisoma barua hii wote hawakuipenda ispokuwa Ashtar, kwa sababu wao walikwishauona ukali wa Abdur Rahman. Lakini Ashtar aliyekwenda Madina na kurejea baada ya kumuomba msamaha Hadhrat Uthman[ra], toba yake haikudumu na wakati huo huo akaelekea Kufa. Wale

wenzake walipoona kwamba Ashtar amerejea Kufa basi wao wakahofia kwamba Abdur Rahman hatakuwa na yakini na maneno yao na atadhani kwamba mambo yote haya yametendeka kwa ushauri wao. Kutokana na hofu hii, hao nao pia wakatoroka. Abdur Rahman alipofahamu akatuma watu kuwafuata lakini hawakuweza kuwakamata. Maalik Al-Ashtar akachanja mbuga kwa kasi na kuwasili Kufa. Kuingia mjini mikono mitupu aliona hakuendani na hadhi yake. Mtu huyu aliyekuwa akitokea Jazira aliyesafiri kwa kasi akipumzika kwenye kila kitu cha pili — badala ya kila kituo — kuja kukutana na wenzake, akaanza kutangaza kuwa anatokea Madina, na ili kuwahamakisha watu akasema: 'Sasa hivi nimeachana na Said bin Al 'Aas, nimesafiri naye kwa umbali wa kituo kimoja. Anatangaza wazi wazi akisema kuwa nitawadhalilisha wanawake wa Kufa, na anasema kwamba raslimali za Kufa ni mali za Wakureish na anasoma ubeti huu kwa fahari:

وَيْلٌ لِّاَشْرَافِ النِّسَآءِ مِنِّىْ      صَمَحْمَحٌ كَأَنَّنِىْ مِنْ جِنّ

Yaani, Wanawake wenye hadhi watapatwa na msiba kutokana nami; mimi ni mtu mwenye nguvu kiasi hiki kana kwamba ninatokana na majinni.'

(Tabarii, J. 6, uk. 2929, chapa ya Beirut)

Watu waliposikia maneno yake haya akili zao zikachanganyikiwa na wakawa na yakini na maneno

yake haya, na mara moja mori ukaenea. Watu wenye akili na busara wakafahamisha sana kuwa huu ni udanganyifu, msidanganyike. Lakini nani ausitishe mori wa watu, hakuna yeyote aliyekuwa akiyasikia maneno yao. Mtu mmoja akasimama na kutangaza: 'Yule anayetaka Said bin Al-'Aas, mtawala wa Kufa, Arudishwe na kutaka kumpendekeza mtawala mwingine basi huyo anapaswa mara moja aungane na Yazid bin Qais.' Kutokana na tangazo hili watu wakaenda mbio mbio na msikitini hapakubakia na mtu isipokuwa watu wenye busara, wenye kuheshimika na viongozi. Umar bin Al Jarid alikuwa amekaimu nafasi ya Said. Yeye akaanza kuwapa mawaidha wale watu waliobakia kwamba: 'Enyi watu! Ikumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu kwamba sisi tulikuwa maadui, Yeye Akaingiza umoja ndani ya mioyo yenu na mkawa ndugu. Mlikuwa mmesimama kandoni mwa shimo la maangamio na Mwenyezi Mungu Akakuokoeni nalo. Hivyo msijiingize wenyewe ndani ya msiba ule ambao Mwenyezi Mungu Alikuokoeni nao. Je ninyi hamuitambui haki baada ya Islam, mwongozo wa Mwenyezi Mungu na Suna za Mtume[saw] na hamji kuelekea kwenye mlango wa haki? Hapo Qa'qaa' bin 'Amr[ra] akamwambia: Unataka kuisitisha fitina hii kwa mawaidha? Ondoa tumaini hilo. Hakuna kitu chochote kiwezacho kusitisha fujo hizo mbali ya upanga, na zama hizo haziko mbali ambapo upanga pia utachomolewa, wakati huo watu hawa watalia kama wanambuzi na watatamani kwamba zama

hizi zirejee, lakini hata hivyo Mwenyezi Mungu Hatawarejeshea tena zama hizi mpaka Kiama. Watu wakajumuika nje ya mji na kuelekea upande wa Madina wakimsubiri Said bin Al-'Aas. Alipotokea wakamwambia: 'Rudi ulikotoka, hatuna haja na wewe.' Said akasema: 'Je hii ni busara kweli kwamba watu wamejumuika kiasi hiki na kutoka kwa ajili ya kazi hii? Kuna haja gani ya watu elfu moja kumzuia mtu mmoja? Ilikuwa yatosha hii tu kwamba mumtume mtu mmoja kwa Khalifa na mwingine mumtume kwangu.' Baada ya kusema haya akamgeuza farasi wake na kurejea Madina ili kwenda kumtahadharisha Hadhrat Uthman[ra]. Na hawa watu wakabaki wamepigwa bumbuazi. Wakati huo huo akaonekana mtumwa wake fulani, na watu hao wakamuua.

Said bin Al-'Aas alipowasili Madina akampasha Hadhrat Uthman[ra] habari ya fitina yote hii. Hadhrat Uthman[ra] akamuuliza, je watu hao wamesimama kunipinga? Said akajibu, wao wanadhihirisha tu kwamba Mtawala abadilishwe.' Akauliza: Wao wanamtaka nani? Said akajibu, wao wanamtaka Abu Musa Ash'ari[ra].

## Kuteuliwa kwa Abu Musa Ash'ari[as] kuwa Mtawala wa Kufa

Hadhrat Uthman[ra] akasema: 'Sisi tumemteua Abu Musa Ash'ari[as] kuwa Mtawala wa Kufa, na kwa haki ya Mwenyezi Mungu, sintowapa watu hao udhuru wowote ule na sintowaacha wawe na dalili yoyote ile na nitakuwa

na subira juu ya maneno yao kutokana na maagizo ya Mtume[saw] hadi ufike wakati ule wanaoudhamiria', yaani wa kumuengua Hadhrat Uthman[ra]. Fitina hii ilidhihirisha kwamba watu hawa walikuwa hawajiepushi na aina yoyote ile ya uongo na udanganyifu.

## Kufichuka kwa Hila za Wafisadi

Kutoroka kwa Maalik al-Ashtar toka Jazira na kudhihirisha kuwa alitoka Madina, kumzulia lawama ya uongo Said bin Al-'Aas na kutunga maneno ya aibu na kumnasibishia, hayakuwa mambo ambayo yabakize asili ya dhamira yao na matamanio yao ya siri kufichika, bali kutokana na mambo hayo, inafahamika kwa uwazi kabisa kuwa watu hawa walikuwa hawaijui kabisa Islam. Islam haisemi kuwa uongo unajuzu wala haiukubali ulaghai. Ni kosa kubwa ndani ya Islam kutoa tuhuma za uongo. Lakini hawa wenye kudhihirisha mapenzi ya Islam na kudhihirisha ghera kwa ajili yake wanasema uongo, wanatoa tuhuma za uongo na hawaoni aibu yoyote kutokana na kazi hizo. Hivyo, watu wa aina hii kupiga kelele dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] ni uthibitisho wa kutosha wa jambo hili kwamba fujo zote hizo hazikusababishwa na kasoro yoyote ile ya kweli, bali ni matokeo ya kuwa mbali na Islam na kutokuwa na dini.

Mdhihiriko wa pili wa tukio hili ni kwamba watu hao hawakuwa na lalamiko la aina yoyote ile la kweli dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] na magavana wake, kwa sababu

kama kweli kungekuwa na lalamiko, sasa kulikuwa na haja gani ya kubuni uongo? Kuunda kwa malalamiko ya uongo tu ni uthibitisho wa kutosha wa jambo hili kwamba watu hao hawakuwa na malalamiko ya kweli. Matokeo yake, sisi twaona kwamba kabla ya kuja kwa Ashtar, wakati Yazid alipofanya mkutano, kulikuwa na maaskari wachache tu walioshiriki kwenye mkutano huo na walipozuiwa na Qa‘qaa‘, watu hawa wakaogopa na kusitisha kufanya mkutano. Lakini ndani ya mwezi huo huo twaona kwamba baada ya kuathirika na uongo wa Ashtar, kundi kubwa la watu wa Kufa wakaungana na watu hao na kutoka Kufa kwa ajili ya kumzuia Said na kumtaka mtawala mwingine. Huu ni ushahidi wa jambo hili kwamba mwanzoni watu walikuwa hawaafikiani na mambo yao, kwa sababu hawakuwa na njia yoyote ya kuwatia jadhba. Ashtar alipoivumbua njia hii iliyokuwa ikichochea ghera ya watu, basi kundi moja la watu likadanganyika na kuungana nao.

Kutokana na kudhihirika kwa fitina hiyo, jambo hili pia linakuwa wazi kwamba upinzani hasa wa watu hao ulikuwa ni dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] na sio dhidi ya magavana wake. Kwa sababu mwanzoni, watu hawa walikuwa wakitaka kuhamakisha jadhba dhidi yake tu, lakini walipoona kwamba watu hawawezi kushiriki nao katika jambo hili, bali walikuwa wanaelekea katika kuwapinga, ndipo wakaanza kuwahamakisha watu dhidi

ya watawala. Kuelekea upande wa Madina pamoja na kundi kubwa la watu kunathibitisha kwamba nia yao haikuwa njema kwa Hadhrat Uthman[ra]. Kwa kumuua bila sababu yoyote mtumwa aliyeachwa huru na Said bin Al-'Aas, pia yadhihirika kwamba watu hawa hawakujiepusha kufanya uhalifu wa aina yoyote katika kutimiza makusudio yao.

Yaonekana kwamba watu hawa sasa wakaanza kulihisi jambo hili kwamba ikiwa watachelewa kidogo basi umma wa Waislamu watafahamu kikamilifu uhakika wa fitina yao. Ndio sababu kwa hali yoyote ile wakawa wanafikiria namna ya kutimiza lengo lao kwa haraka sana. Lakini Hadhrat Uthman[ra], kwa busara zake, akauvunja tena udhuru wao, na mara moja akawapa watu hawa taarifa za kumteua Abu Musa Ash'ari[ra] kuwa mtawala. Kurudi kwa Said bin Al-'Aas na kuwataarifu watu wa Madina dhamira zao, basi matarajio yao yakawa yameshaharibika na mara moja njama zao walizofikiria za kuiteka Madina zikawa zimeshabatilika, na watu hawa wakawa wameshalazimika kurejea. Sasa kuteuliwa kwa Abu Musa Ash'ari[as] kuwa mtawala, kila udhuru wao ukawa umevunjika kabisa, kwa sababu watu hawa tangu zamani walikuwa wakitaka utawala wake.

Wakati Abu Musa Ash'ari[ra] alipofahamu kuwa ameteuliwa kuwa mtawala wa Kufa, basi akawakusanya watu wote na kusema: 'Enyi watu! Msitoke tena kwa

ajili ya kazi za aina hiyo na mshikamane na Jamaat na utii na muwe na subira na msiwe na papara, kwa sababu sasa mnaye kati yenu Amir, yaani mimi nimeteuliwa kuwa Amir.' Hapo watu hao wakaomba wakisema: 'Tuongoze katika sala.' Akalikataa ombi hili na kusema: 'Hapana, hii haiwezekani kabisa.

## Ni Lazima Kumtii Mtawala wa Zama

Msipokiri utii kamili kwa Hadhrat Uthman[ra] na kuzikubali hukumu zake, basi mimi sintakuwa Imamu wenu kuwasalisha. Hapo watu hao wakatoa ahadi ya jambo hili kwamba siku zijazo watatii kikamilifu na watazikubali hukumu zake. Ndipo Hadhrat Musa Ash'ari[as] akawasalisha. Halikadhalika Abu Musa Ash'ari[as] akawaambia: 'Sikilizeni! Mimi nilisikia kwa Mtume[saw] kwamba yeyote, katika wakati ambapo watu wako chini ya Imamu mmoja, atakayesimama kwa ajili ya kuleta mfarakano na kwa ajili ya kuisambaratisha Jumuiya, basi huyo muueni hata kama awe nani. *(Muslim Kitabul Imaara, babu hukmi man farraqa Amral muslimina wa huwa mujtamiun).* Na Mtume[saw] hakuweka sharti la uadilifu wa Imam, yaani nyinyi hamuwezi kusema kuwa Hadhrat Uthman[ra] sio mwadilifu, kwa sababu hata kama hii ikubaliwe, bado kitendo chenu hiki hakitajuzu. Kwa sababu Mtume[saw] hakuweka sharti la 'mwadilifu', bali alisema hivi tu kwamba kama awepo mtawala yeyote kwa watu.

Haya ndio yale mawazo ya watu ambao waliutumia umri wao kwa ajili ya kuihudumia Islam na walioisikia Islam kwa kinywa cha Mtume[saw], na wakaitekeleza mbele yake na kupata ithibati ya kukubalika. Watu hawa, achilia mbali kusali nyuma ya waasi, hawakuwa wakipenda hata kuwa Imam wao, na walikuwa wakiwafahamu hao kuwa ni wenye kustahili kuuawa. Je mtu yeyote anaweza kusema kuhusiana na watu hao kuwa walishiriki kwenye fitina dhidi ya Uthman[ra]? Au yaweza kusemwa kwamba Hadhrat Uthman[ra] na magavana wake walikuwa wakitilifu haki za raia? Au yaweza kukubalika mbele ya kuwepo matukio hayo kwamba hao waasi walikuwa wakifanya uasi kwa ajili ya watu hawa? Hapana, bali hili kundi la wafisadi walikuwa tayari kufanya uasi baada ya kuwaonea husuda masahaba[ra] na walikuwa wakificha mawazo yao ya moyoni. Makusudio yao hasa yalikuwa ni kuuangamiza utawala wa Kiislamu, na makusudio haya yasingeweza kupatikana bila ya kumuengua Hadhrat Uthman[ra]. Baadhi ya majahili au Waislamu wasiokuwa na mwelekeo wa dini pia, bila ya kuufahamu udanganyifu wao huo, kutokana na ubinafsi au kutokuwa werevu, wakaungana nao.

## Njama Nyingine Zaidi ya Wafisadi

Kuteuliwa kwa Hadhrat Abu Musa Ash'ari[as] kuwa mtawala kukawafanya watu hao wasibakiwe na sababu yoyote ile ya kueneza fitina. Lakini wanaharakati wa asili wa fitina hii wasingeweza kulipenda jambo hili kwamba

juhudi zao zote ziangamie kwa namna hii. Hivyo, mawasiliano ya barua yakaanza na ikaamuliwa kwamba watu kadha toka kila nchi waende Madina kama wawakilishi. Huko pia washauriane namna ya utendaji wa siku zijazo, na Hadhrat Uthman[ra] aulizwe baadhi ya maswali ili mambo hayo yaenee nchi zote, na watu wawe na yakini kwamba zile shutuma alizokuwa akilaumiwa Hadhrat Uthman[ra] zimesha thibitishwa. Baada ya kufanya mashauriano haya, watu hawa wakatoka majumbani mwao na wote wakaelekea Madina. Walipokaribia Madina, Hadhrat Uthman[ra] akapata taarifa ya kuja kwao. Akawatuma watu wawili waende kupata undani wao na kufanya uchunguzi wa nia hasa ya ujio wao na kutoa taarifa. Watu hawa wawili walienda na kukutana na msafara huo nje ya Madina. Walipoongea na wachunguzi hao wawili wakaeleza hali zao. Wachunguzi hao wakawauliza kama kuna mtu yeyote miongoni mwa watu wa Madina aliye pamoja nao. Hapo kundi hilo la wafisadi likasema kuwa wako watu watatu na mbali nao hakuna mtu yeyote wa nne anayewahurumia. Wawili hao wakawauliza: 'Sasa dhamira yenu ni nini?' Wakasema: 'Dhamira ni hii kwamba baada ya kwenda Madina, tutaongea na Hadhrat Uthman[ra], kuhusiana na baadhi ya mambo fulani ambayo tayari tulishayaingiza mioyoni mwa watu, halafu tutarejea katika nchi zetu na tutawaambia watu kwamba tumemtolea shutuma nyingi Hadhrat Uthman[ra]

na tumezithibitisha ukweli wake. Lakini amekataa kuachana na mambo haya wala hakufanya toba. Halafu tutatoka kwa kisingizio cha Hija na baada ya kufika Madina tutamzingira. Kama atajiengua kwenye Ukhalifa basi itakuwa heri, waila tutamuua.

## Kufichuka kwa Njama

Wapelelezi hao wawili walipopata habari zao kikamilifu wakarejea na kumfahamisha Hadhrat Uthman[ra] habari zote. Yeye aliposikia habari za watu hao alicheka na kumuomba dua Mwenyezi Mungu: 'Ee Mwenyezi Mungu, walinde watu hao na upotevu, kwani Usipowakinga basi wataangamia'. Halafu akasema kuhusiana na wale watu watatu miongoni mwa watu wa Madina walio pamoja na watu wale kwamba: 'Ammaar, yeye ana hasira kwa kuwa alimshambulia Abbas bin 'Utbah bin Abi Lahab na nikamkemea, na Muhammad bin Abu Bakr amekuwa mwenye kiburi na anadhani kwamba yeye sasa yuko juu ya sheria, na Muhammad bin Abu Hudhaifa anajiingiza mwenyewe ndani ya msiba bila ya sababu yoyote'. Halafu akawaita waasi hao na pia akawakusanya masahaba.

## Hadhrat Uthman[ra] Awaita Waasi

Watu wote walipojumuika akawapa taarifa ya hali zote na wale wapelelezi wawili pia walikuwa wamesimama kama mashahidi na wakatoa ushahidi. Hapo masahaba[ra] wote wakatoa fatuwa kwamba watu hao wauawe kwa

sababu Mtume[saw] alisema: 'Yule mtu anayewaita watu wamtii yeye au mtu mwingine wakati Imam mmoja yupo, laana ya Mungu iwe juu yake; muueni mtu wa aina hiyo hata kama awe nani. (*Muslim, Kitabul Imaara, Babu Hukmi man farraqa Amral Muslimiina wa huwa Mujtami'un*), na wakakumbusha kauli ya Hadhrat Umar[ra] aliposema: 'Mimi sioni kuwa inajuzu kwenu kumuua mtu yeyote yule bila ya mimi kushiriki'. Yaani haijuzu kumuua mtu yeyote yule bila ya serikali kuashiria. Baada ya kusikia fatuwa hii ya masahaba, Hadhrat Uthman[ra] alisema: 'Hapana, tutawasamehe na tutazikubali udhuru wao na tutawafahamisha kwa jitihada zote na hatutampinga mtu yeyote maadamu havunji hukumu yoyote ile ya sheria au hadhihirishi ukafiri.'

## Hadhrat Uthman[ra] Kujithibitisha Kutokuwa na Hatia

Halafu akasema kwamba watu hao wamesema maneno fulani ambayo nyinyi pia mwayafahamu, na mawazo yao ni kwamba wao wajadiliane nami kuhusiana na mambo hayo ili watakaporejea waweze kusema kwamba tulijadiliana na Uthman[ra] kuhusiana na mambo hayo na akashindwa. Watu hawa wanasema kwamba mimi nilisali sala kamili wakati nikiwa safarini, ilhali Mtume[saw] alikuwa akisali sala ya Qasr (fupi), (*Tirmidhii, Abwaabus safar, Babut-taksiiri fis-safari*) Lakini huko Minaa tu ndio nilisali sala kamili na hiyo pia ilitokana na sababu mbili,

moja ni kwamba huko kulikuwa na raslimali zangu na nilikuwa nimeoa huko. Pili ni hivi kwamba nilifahamu kuwa katika siku hizo watu walikuwa wamekuja kwa ajili ya Hija toka pande zote, wasiojua miongoni mwao wangesema Khalifa anasali rakaa mbili kwa hiyo sala itakuwa ni rakaa mbili tu. Je jambo hili si sahihi? masahaba[ra] wakajibu kwamba naam, ni sahihi. Lawama nyingine, akasema, wanayoitoa watu hawa ni kwamba mimi nimefanya bidaa ya kutenga *Rakh* (Kwa Kiarabu *Himaa*, eneo lililohamiwa na serikali ambamo raia hawaruhusiwi kukata miti au nyasi), ilhali lawama hii si sahihi. *Rakh* iliwekwa kabla yangu, Hadhrat Umar[ra] aliianzisha, nami nimeipanua tu kwa kuongezeka ngamia wa sadaka, na ardhi ya *Rakh* si mali ya mtu yeyote wala nami sifaidiki na chochote humo. Mimi ninao ngamia wawili tu ilhali wakati nilipokuwa Khalifa, wakati huo nilikuwa ni mwenye mali kuliko Arabuni yote. Sasa ninao ngamia wawili tu ambao wamewekwa kwa ajili ya Hija. Je hii si sahihi?' Masahaba[ra] wakajibu: 'Naam, hiyo ni sahihi.' Halafu akasema kwamba wanasema kwamba ninawafanya vijana kuwa watawala, ilhali mimi nawafanya watawala watu wale tu walio na sifa njema na mienendo mizuri. Wale waja wa Mungu wa kabla yangu waliwafanya kuwa watawala watu waliokuwa na umri mdogo zaidi ya hawa watendaji wangu niliowateua. Na Mtume[saw] alipomteua Usama bin Zaid kuwa Mkuu wa kikosi cha jeshi, zilitolewa lawama zaidi ya hizo ambazo

sasa zatolewa kwangu. Je hii si sahihi? masahaba[ra] wakajibu kwamba: Naam, ni sahihi. Hawa wanakosoa tu mbele ya watu lakini undani wenyewe wa mambo hawauelezi. Kwa uchache, kwa namna hii hii Hadhrat Uthman[ra] alizibainisha shutuma zote, kwa kuzichambua moja moja na kutoa majibu yake. Masahaba wakawa mara kwa mara wakishinikiza kwamba hao wauawe lakini Hadhrat Uthman[ra] akawa hakubaliani nao na akawaachia huru. Bw. Tabarii anasema: اَبَى الْمُسْلِمُوْنَ اِلَّا قَتْلَهُمْ وَاَبٰى اِلَّا تَرْكَهُمْ (Tabarii, J. 6, uk. 2954, chapa ya Bairut). Yaani Waislamu wote hawakuridhia jambo lingine lolote mbali ya kuwaua watu hao, lakini Hadhrat Uthman[ra] hakuwa tayari kwa namna yoyote ile kutoa adhabu.

## Hadhrat Uthman[ra] Kuwahurumia Wafisadi

Inafahamika kutokana na tukio hili kwamba hao watu mafisadi walikuwa wakitumia udanganyifu na ulaghai wa aina gani, na katika zama hizo ambapo hakukuwa na mpango wa matbaa na nyenzo za usafiri kama za siku hizi, ilikuwa ni rahisi kiasi gani kwa watu hawa kuwapoteza watu wasiokuwa na ufahamu. Lakini kwa hakika watu hao hawakuwa na sababu yoyote inayokubalika kiakili ya kufanya uasi. Haki haikuwa pamoja nao, wala wao hawakuwa pamoja na haki. Harakati zao zote ziliutegemea uongo na batili, na ni huruma tu ya Hadhrat Uthman[ra] ndio iliyowasalimisha,

waila Waislamu wangewakata vipande vipande, wao wasingeweza kuvumilia hata kidogo kwamba ile amani na utulivu walioupata kwa kuyatoa maisha yao itoweke hivi hivi kutokana na utukutu wa watukutu wachache nao walikuwa wakiona kwamba kama watu wa aina hii hawataadhibiwa kwa haraka basi utawala wa Kiislamu utasambaratika. Lakini Hadhrat Uthman[ra] alikuwa ni mwenye umbile la huruma, yeye alikuwa akitaka kwamba kadiri iwezekanavyo, watu hao wapate mwongozo na wasife katika hali ya ukafiri, hivyo akawa laini kwao na vitendo vyao vya uasi wa wazi wazi akavitabiria tu kuwa ni dhamira tu ya kutenda uasi na akaendelea kuahirisha kutoa adhabu. Inafahamika pia kutokana na tukio hili kwamba masahaba[ra] walikuwa wakiwachukia kabisa watu hawa, kwa sababu, kwanza wao wenyewe wanabainisha kwamba Madina kuna watu watatu tu walio pamoja nao na sio zaidi yao. Kama kungekuwepo na masahaba[ra] weingine pamoja nao basi wangewataja majina yao. Pili, masahaba[ra] pia walithibitisha kwa vitendo vyao kuwa wao walivichukia vitendo vya watu hawa na walikuwa wakivifahamu vitendo vyao kuwa ni vyenye kukiuka sheria kiasi hiki kwamba adhabu yao haikujuzu kuwa minghairi ya kuuawa. Kama masahaba[ra] wangekuwa pamoja nao, au kama watu wa Madina wangekuwa wanaafikiana nao,

basi watu hao hawangekuwa na haja ya hila au kisingizio chochote, wakati huo huo wangemuua Hadhrat Uthman[ra] na mahali pake wangemchagua mtu mwingine kwa ajili ya Ukhalifa. Lakini twaona kwamba badala ya watu hawa kufanikiwa kumuua Hadhrat Uthman[ra], wao wenyewe wakawa wameingia ndani ya hatari ya kuuawa na panga zilizochomolewa za masahaba, na watu hawa waliweza kusalimika na kurejea makwao kwa sababu tu ya huruma na hisani ya mja huyu mwenye huruma na ukarimu, ambaye walikuwa wakidhihirisha dhamira yao ya kumuua na kueneza uasi kiasi hiki. Chuki na ukosefu wa Taqwa wa wafisadi hawa unastaajabisha, kwamba hawakufaidika chochote kutokana na tukio hili, kila shutuma yao ilipatiwa jibu maridhawa na lawama zote zikathibitishwa kuwa si sahihi na zisizo na msingi. Waliiona huruma na ukarimu wa Hadhrat Uthman[ra], na nafsi ya kila mtu ilikuwa ikitoa ushuhuda wa jambo hili kuwa wakati huo hawezi kupatikana mtu yeyote duniani aliyekuwa mithili yake. Lakini badala ya watu hawa kutubia madhambi yao, kuionea haya dhuluma yao, kuyajutia makosa yao, kujirudi utukutu wao, wakaungua zaidi ndani ya moto wa hasira na ghadhabu na wakaona wamedhalilika kwa kukosa kwao majibu na msamaha wa Hadhrat Uthman[ra] wakaona kuwa ni matokeo ya

ubora wa mpango wao na wakarudi na mawazo ya kuitimiza dhamira yao iliyobakia mnamo siku zijazo.

## Njama Nyingine Kubwa ya Wafisadi

Watu hao waliporudi wakaanzisha tena mawasiliano ya barua na hatimaye wakaamua kuwa mnamo mwezi wa *Shawaāli*, sawa na dhamira yao ya kwanza, watoke kimsafara, kwa lengo la kwenda kuhiji na kwenda Madina na kuivuruga vuruvuru mara moja nidhamu yote na kuibadili nidhamu ya utawala sawa na matashi yao. Sawa na mpango huu, mnamo *Shawaāli*, yaani mwezi wa kumi wa mwandamo, katika mwaka wa kumi na mbili wa Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra], ndani ya mwaka wa thelathini na sita wa Hijra, watu hawa wakatoka majumbani mwao katika misafara mitatu. Msafara mmoja ulitoka Basra, mwingine Kufa na mwingine Misri. Baada ya kufikiria kutofanikiwa kwao kwa siku za nyuma na kutilia maanani jambo hili kwamba majaribio haya ni majaribio ya mwisho, Abdullah bin Sabaa mwenyewe pia alielekea Madina pamoja na msafara wa Misri. Kutoka kwa huyu kiongozi mwenyewe wa waasi ilikuwa ni alama kwamba watu hawa watajaribu kufanya kila tadbiri kwa ajili ya kulipata kusudio lao. Kwa kuwa kila kundi, kwenye eneo lake, lilidhihirisha nia ya kwenda kuhiji, watu wengine pia wakajumuika kwa lengo la kwenda kuhiji na kwa sababu hii, nia hasa za watu hawa, zikawa zimefichika kwa umma wa Waislamu. Lakini kwa kuwa watawala

walikuwa wanaijua njama yao ya siri, Abdullah bin Abi Sarha, mtawala wa Misri, alimtuma mtu fulani makhsus kwa Hadhrat Uthman[ra] na kutoa habari mapema juu ya msafara huo na njama zao za siri, iliyowafanya watu wa Madina wawe wameshatambua mapema. Hapa swali linaibuka kwamba wakati watu wa Madina na hasa masahaba[ra] walikuwa wanataka kuwaua watu hao kutokana na kuja kwao mara tatu, na wao walikuwa wakifahamu kuwa Hadhrat Uthman[ra] alitambua kwamba baada ya kuja kwa kisingizio cha kwenda Kuhiji. walikuwa na dhamira ya kufanya ufisadi, sasa kwa nini hawakufanya mpango mwingine wowote na wakafunga safari kwa mpango ule ule wa kwanza ambao Hadhrat Uthman[ra] alikuwa ameshaufahamu. Je hayo yanamaanisha kwamba watu wa Madina kwa hakika, walikuwa pamoja na watu hao na ndio sababu watu hao hawakuwa na hofu? Jibu la swali hili ni kwamba hakuna shaka ujasiri wao huo unadhihirisha kuwa watu hao walikuwa na yakini kamili ya mafanikio yao, lakini sababu yake sio hii kwamba masahaba[ra] au watu wa Madina walikuwa pamoja nao au walikuwa wakidhihirisha kuwaunga mkono, bali kama vile inavyothibitika kwa maelezo yao wenyewe kwamba walikuwepo watu watatu tu ndani ya Madina waliokuwa pamoja nao na kama vile inavyothibitika kutokana na matukio kwamba masahaba[ra] na watu wengine wa Madina walikuwa wakiwachukia sana watu hao. Hivyo, sababu ya ujasiri wao haiwezi kuwa hii kwamba watu

wale (wa Madina) walikuwa wakidhihirisha kuwaunga mkono, sababu hasa ya ujasiri wao ilikuwa ni huruma ya Hadhrat Uthman[ra]. Watu hawa walikuwa wakifahamu kwamba kama tutafanikiwa basi hilo ndilo lengo lenyewe, na kama hatutafanikiwa basi tutamuomba Hadhrat Uthman[ra] atuhurumie na kuepuka adhabu. Pili, ingawa walikuwa wameshauona mwenendo wa masahaba[ra] na watu wa Madina na walikuwa wakifahamu kwamba Hadhrat Uthman[ra] alikuwa ameshapata taarifa ya ujio wao, lakini watu hawa walikuwa wakidhani kuwa Hadhrat Uthman[ra] kwa sababu ya upole wake hatakusanya jeshi kwa ajili ya kupigana nao. Na masahaba[ra] hawatakabiliana nao, kwa sababu watu hawa walikuwa wakikisia sawa na hali yao kwamba masahaba[ra] wanadhihirisha tu uaminifu kwa Hadhrat Uthman[ra], lakini kwa hakika wanapenda kuangamia kwake. Na sababu ya wazo hili ilikuwa ni kwamba watu hawa walikuwa wakidhihirisha haya haya kwamba chochote tukifanyacho ni kwa ajili ya kulinda haki za masahaba. Hivyo walikuwa wakidhani kwamba masahaba[ra] wameathirika na udanganyifu wetu huu na wanaafikiana tu nasi mioyoni mwao.

## Waasi Kuwasili Madina

Pindi taarifa za kukaribia Madina kwa jeshi hilo zilipowasili, masahaba[ra] na watu wa Madina waliokuwa wameenda kusimamia raslimali zao karibu na Madina, wakajumuika Madina na kugawanyika katika makundi

mawili. Kundi moja likaenda nje ya Madina kukabiliana na watu hao, na kundi la pili likabaki mjini kwa ajili ya kumlinda Hadhrat Uthman[ra]. Wakati misafara yote mitatu ilipofika karibu na Madina, watu wa Basra wakaweka kambi katika eneo la Dhu Khashab, watu wa Kufa wakaweka kambi eneo la A'waas na watu wa Misri wakaweka kambi katika eneo la Dhul Marwah. Na wakashauriana kwamba sasa wafanye nini. Ingawa idadi ya jeshi hilo inakadiriwa kuanzia elfu moja na mia nane hadi elfu tatu (mbali na wale mahujaji wengine waliokuwa pamoja nao wakiwadhania kuwa wao ni msafara wa Hija), lakini hata hivyo watu hao walikuwa wakielewa kuwa ikiwa mashujaa wa Kiislamu watakuwa tayari kwa mapambano basi haitakuwa rahisi kwao kukabiliana nao, ndio sababu walipoingia tu Madina wakaona ni muhimu kwanza kupata rai ya watu wa Madina. Hivyo, watu wawili, Ziad bin An-Nadhr na Abdullah bin Al-Asamm wakawashauri watu wa Kufa na watu wa Basra kwamba papara sio nzuri, kama wao watafanya papara basi hata watu wa Misri pia watalazimika kuharakisha na mpango utaharibika. Wakasema: 'Tumepata taarifa kwamba watu wa Madina wameandaa jeshi kwa ajili ya kukabiliana nasi, na juu ya kutokuwa na taarifa kamili ya hali zetu, wamefanya maandalizi kiasi hiki, hivyo baada ya kupata taarifa kamili ya hali zetu basi watachukua tahadhari zaidi na mafanikio yetu yatakuwa ni ndoto na mawazo tu.

Hivyo, ni bora kwamba kwanza sisi tutangulie ili kupata taarifa ya hali ya mambo na kuongea na watu wa Madina. Ikiwa watu hao wataona kuwa haijuzu kupigana nasi na habari zilizotufikia kuhusiana nao zitakuwa si sahihi, basi sisi tutarudi na kuwaelezeni hali zote na hatua zifaazo zitachukuliwa'. Wote wakapendezwa na ushauri huu na watu hao wawili wakaenda Madina Kwanza wakutana na wake watakatifu wa Mtume[saw] na kuwaomba ruhusa ya kuingia Madina na wakasema kwamba sisi tumekuja kwa sababu hii tu kwamba tumuombe Hadhrat Uthman[ra] awabadilishe baadhi ya watawala na hatuna shughuli nyingine yoyote minghairi ya hiyo. Wake wote watakatifu wa Mtume[saw] wakakataa kukubali maneno yao na wakasema: 'Matokeo ya jambo hili si mazuri.' Halafu, kwa zamu, wakawaendea Hadhrat Ali[ra], Hadhrat Talha[ra] na Hadhrat Zubair[ra] na kuwaambia sababu hii hii ya kuja kwao na kudhihirisha kuwa wana nia njema, na hivyo kuwaomba ruhusa ya kuingia Madina. Lakini hata hawa masahaba[ra] watatu pia wakakataa kudanganywa nao na kuwajibu kwa uwazi kuwa hakuna heri katika harakati yao hii. (Tabarii, J. 6, uk. 2956, chapa ya Beirut)

Watu hawa wawili baada ya kufahamu habari za Madina na kutofanikiwa katika makusudio yao, waliporudi na kuwafahamisha wenzao habari zote, ndipo viongozi wachache wa Kufa, Basra na Misri wakaja Madina

kufanya majaribio ya mwisho. Watu wa Misri, chini ya mafundisho ya Abdullah bin Sabaa, walimfahamu Hadhrat Ali[ra] kuwa ni wasiyy wa Mtume[saw] na hawakuwa tayari kufanya baiat ya mtu yeyote minghairi yake. Lakini watu wa Kufa na watu wa Basra, ingawa walishirikiana nao katika uasi, lakini itikadi zao za kidini hazikufanana na watu wa Misri. Watu wa Kufa waliona kufanya baiat ya Zubair bin 'Awwaam kuwa ni yenye faida kwa makusudio yao na watu wa Basra waliona ya Talha[ra]. Kutokana na hitilafu hii, wawakilishi wa kila msafara wakawaendea watu tofauti waliotaka kuwaketisha katika kiti cha ukhalifa baada ya Hadhrat Uthman[ra].

## Watu wa Misri Kumwendea Hadhrat Ali[ra]

Watu wa Misri wakaenda kwa Hadhrat Ali[ra]. Wakati huo yeye alikuwa nje ya Madina akiongoza kikosi kimoja cha jeshi na alikuwa tayari kuwaangamiza. Watu hawa walipofika kwake wakasema: 'Kutokana na mfumo mbovu wa utawala, Hadhrat Uthman[ra] sasa hafai kuwa Khalifa, sisi tumekuja kumuondoa na tunataraji kwamba wewe utakikubali cheo hiki baada yake.' Aliposikia kauli yao hii akaonyesha ghera ile ya kidini iliyomstahili mtu wa daraja kama yake na kuwakaripia watu hao kwa ukali sana na akasema: 'Watu wema wote wanafahamu kuwa Mtume[saw], kwa njia ya bishara, aliyalaani majeshi yaliyopiga kambi Dhul Marwa na Dhu Khashab

(walipokuwa wameweka kambi watu hawa). (Al Bidaya Wannihaaya, J. 7, uk. 174, chapa ya Beirut 1966). 'Hivyo Mwenyezi Mungu Akufanyeni vibaya, rudini mlikotoka.' Hapo watu hao wakasema: 'Vizuri sana, tutarudi.' Na baada ya kusema haya wakarudi.

## Watu wa Kufa Kumwendea Hadhrat Zubair[ra]

Watu wa Kufa wakamwendea Hadhrat Zubair[ra] na kumuomba: 'Ukubali kuchukua cheo cha Ukhalifa kitakapokuwa wazi. Naye pia akawatendea vile vile kama Hadhrat Ali[ra] na kuwakaripia kwa ukali sana na akasema: 'Waaminio wote wnafahamu kwamba Mtume[saw] alisema: Majeshi yenye kupiga kambi Dhul Marwa, Dhul Khashab na A'waas watakuwa waliolaaniwa.'

## Watu wa Basra Kumwendea Hadhrat Talha[ra]

Halikadhalika watu wa Basra wakaja kwa Hadhrat Talha naye pia akawakana na kuwafahamisha juu ya bishara ya Mtume[saw], ya kuwalaani. (Tabarii, J. 6, uk. 2956-57 chapa ya Beirut).

## Kuteuliwa kwa Muhammad bin Abi Bakr kuwa Mtawala wa Misri

Watu hawa walipoiona hali hii, na kukata tamaa kabisa, hivyo hatimaye wakafanya hila hii kwamba wakadhihirisha kujutia kitendo chao na kufanya tu ombi hili kwamba baadhi ya watawala wabadilishwe. Hadhrat

Uthman[ra] alipofahamu jambo hili basi akalikubali ombi lao hili kwa upendo mkubwa na huruma, na kuhusiana na ombi la watu hao akambadili mtawala wa Misri, Abdullah bin Abi Sarha, na mahali pake akamteua Muhammad bin Abi Bakr kuwa mtawala wa Misri. Juu ya haya watu hawa, kwa dhahiri, wakafurahi na kurejea, na watu wa Madina wakafurahi kwamba Mwenyezi Mungu Ameiokoa Islam katika uasi mkubwa. Lakini walichokifahamu hakikuwa sahihi, kwa sababu dhamira za watu hao zilikuwa ni nyingine, na hakuna kazi yao yoyote iliyokuwa haina shari na ufisadi.

## Uhakika wa Tofauti za Riwaya

Inapaswa ikumbukwe kwamba huo ndio ule wakati ambapo zilianza hitilafu nyingi katika riwaya, na matukio niliyoyabainisha yamesimuliwa na wasimuliaji mbali mbali kwa njia mbali mbali kiasi ya kwamba hata ukweli umefichika kabisa na watu wengi wakadanganyika nao katika harakati zote hizi ama wakaanza kuwafahamu Masahaba kuwa walishiriki au kwa uchache wakadhani kuwa (masahaba) waliafikiana na waasi hao ndani ya mioyo yao. Lakini jambo hili si sahihi. Kuhusiana na historia ya zama hizo kuna haja ya kuchukua tahadhari kubwa. Kwa sababu baada ya zama hizo hakujaja zama zozote zisiyokuwa na watu wenye kuafikiana na kundi hili au lile, na jambo hili huwa lenye madhara makubwa sana kwa historia. Kwa kuwa wakati

uingiapo uadui mkali au upendo wa kupita kiasi, basi riwaya haiwezi kuwa jinsi ilivyosimuliwa. Hata kama wasimuliaji wasiseme uongo hata hivyo riwaya huathirika na mawazo yao binafsi. Na halafu hali za wasimuliaji wa historia sio zenye kuthibitika kiasi hicho kama za wasimuliaji wa Hadithi. Na ingawa wanahistoria wamechukua tahadhari kubwa sana, hata hivyo hawawezi kuthibitisha riwaya zao kwa ung'avu kama Hadithi. Hivyo kunahitajika tahadhari kubwa sana.

## Kanuni ya Asili ya Kusahihisha Historia

Lakini kufahamu hali sahihi si jambo lisilowezekana kwa kuwa Mwenyezi Mungu Ameziweka wazi njia za aina hiyo ambazo kwazo matukio sahihi yanaweza kufahamika vizuri, na wasimulizi wa aina hii pia wapo ambao wanayaeleza matukio kama yanavyostahili bila ya kuwa na upendeleo. Na usahihi wa historia unategemea kanuni hii ya asili kwamba matukio ya ulimwenguni yako kama mnyororo kwa kufahamu usahihi wa tukio la pekee, inafaa kuonwa kwa kulitunga katika mnyororo kwamba kiungo hicho kimekaa sawa kwenye nafasi yake au la. Kanuni hii inasaidia sana katika kuyapambanua matukio sahihi na potofu.

Ilmuradi, kwa ajili ya kuyafahamu matukio sahihi ya zama zile tahadhari yahitajika na yahitajika ukosoaji na uadilifu. Bila ya kuzingatia mlolongo wa matukio,

historia ya zama zozote zile haiwezi kufahamika kwa usahihi, hasa historia ya zama hizo. Na waandishi wa Ulaya, kwa kuitumia hitilafu hii, wakaiharibu historia ya zama hizo kwa kiasi hiki kwamba moyo wa Mwislamu, kama unayo ghera, huungua kwa kuyasoma matukio hayo na watu wengi wenye imani dhaifu hutokea kuichukia Islam. La kusikitisha ni hili kwamba hata baadhi ya wanahistoria wenyewe wa Kiislamu wamejikwaa kwa kutokuwa kwao waangalifu na wakawa sababu ya kuwapotosha wengine.

## Kutokuwa na Hatia kwa Hadhrat Uthman[ra] na Masahaba[ra] Wengine

Mimi siwezi, kwa wakati huu mfupi, kuyajadili kikamilifu makosa haya waliyoyaangukia watu hawa, lakini kwa muhtasari nitazieleza mbele yenu hali sahihi ambazo kwazo itathibitika kuwa Hadhrat Uthman[ra] na masahaba[ra] wengine walikuwa wameepukana na kila aina ya fitina au aibu, bali mwenendo wao ulikuwa ni mdhihirisho wa khulka za hali ya juu kabisa na mguu wao ulikuwa umeimarika kwenye daraja ya juu kabisa ya wema.

## Waasi Kuingia Tena Madina

Nimeshasema kwamba waasi, kwa dhahir, kwa kudhihirisha kuridhika, wakarejea majumbani kwao. Watu wa Kufa wakaelekea Kufa, watu wa Basra wakelekea Basra na watu wa Misri wakaelekea Misri, na

watu wa Madina baada ya kuona sura ya amani na utulivu na kupata utulivu kwa kurudi kwao, wakaenda kwenye shughuli zao. Lakini hazikupita siku nyingi kwamba katika wakati ambao watu wa Madina ama walikuwa wakijishughulisha katika shughuli zao au wakiwa wameketi majumbani mwao au misikitini, na hawakuwa na wazo lolote kwamba kuna adui yeyote mwenye dhamira ya kuishambulia Madina, ghafla jeshi la waasi hao likaingia Madina na kuuzunguka msikiti na nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] na kutangaza katika mitaa yote ya Madina kwamba yule anayeutaka uhai wake basi atulie nyumbani mwake na asipambane nasi waila haitakuwepo heri. Ujio wa watu hawa ulikuwa wa ghafla kiasi hiki kwamba watu wa Madina hawakuweza kujaribu kupambana nao.

Hadhrat Imam Hasan[ra] anasimulia kwamba: 'Nilikuwa nimeketi msikitini, ghafla ikatokea kelele na sauti za Takbira zikaanza kunguruma katika mitaa ya Madina (hizo zilikuwa ni sauti za Waislamu za kivita). Sote tukashangaa na kuanza kutazama kwamba chanzo chake ni nini? Nikasimama kwa magoti yangu na kuanza kutazama. Mara kwa ghafla watu hawa wakaingia msikitini na kuuteka pia msikiti na mitaa ya pembezoni.

Matokeo ya kushambulia kwao ghafla yakawa hivi kwamba nguvu ya masahaba[ra] na watu wa Madina ikatawanyika na wakashindwa kupigana nao vita na

kukabiliana nao, kwa sababu walishateka njia zote za mji na msikiti. Sasa kulikuwa na njia mbili tu zilizokuwa wazi. Moja ni hii kwamba msaada uje kutoka nje na pili ni kwamba watu wa Madina wajumuike katika sehemu fulani na kisha wakabiliane nao chini ya mpango fulani.

Kuhusiana na njia ya kwanza, wao (waasi) walikuwa na utulivu kwamba Hadhrat Uthman[ra] hatafanya hivyo, kwa sababu huruma yake na dhana yake njema ilikuwa imeongezeka sana, na daima alikuwa akichukua muradi mwingine wa utukutu wao; na kuhusiana na njia ya pili, walifanya mpango huu kwamba waliweka ulinzi kwenye mitaa ya Madina na milango yake na kutoa amri kwamba kusiwe na mjumuiko katika sehemu yoyote ile. Popote watu walipojumuika wakawa wakiwasambaratisha. Naam, walikuwa hawawazuii kuongea wenyewe au kukutana na watu mmoja au mtu wawili.

## Watu wa Madina Kuwafahamisha Waasi

Butwaa ya watu wa Madina ilipopungua kidogo, basi baadhi yao wakaja msikitini, yaliyokuwa ni Makao makuu yao (waasi) na kuanza kuwafahamisha na kudhihirisha kuchukizwa na kitendo chao hiki, lakini watu hao, badala ya kunufaika na nasaha yao, wakawatisha na kuwakemea na kuwaambia kwa uwazi kabisa kwamba kama hawatanyamanza basi hayatawasibu mazuri na watu hao watawatendea vibaya.

## Waasi Kuudhibiti Madina

Sasa Madina ikawa kana kwamba sio Makao Makuu ya Ukhalifa, utawala wa Khalifa wa zama ukawa umesitishwa, na waasi wachache wakawa wanafanya vile walivyotaka. Si masahaba[ra] wa Mtume[saw], si watu wengine wa Madina, wote ikawawia vigumu kuziokoa heshima zao. Na watu wengine, baada ya kuiona fitina hii, wakajifungia majumbani mwao. Mchana na usiku wakawa wameketi majumbani mwao na wakawa ni wenye kuduwaa kutokana na hali hiyo (Tabarii, J. 6, uk. 2962, chapa ya Beirut).

## Masahaba[ra] Wakubwa Wawauliza Waasi Sababu ya Kurejea Kwao

Kwa kuwa watu hawa safari ya nyuma waliondoka wakiwa wamedhihirisha kuridhika kwao na hawakuwa na malalamiko yoyote yaliyobakia kwa siku zijazo, masahaba[ra] wakawa wameshangazwa kwamba hatimaye ni kitu gani kilichowarudisha? Watu wengine hawakuwa na ujasiri wa kuongea mbele yao. Masahaba[ra] wachache maarufu ambao kwenye majina yao watu hawa walikuwa wamejiegemeza na ambao walikuwa wakidai kuwapenda, wao waliwauliza watu hao kwamba hatimaye nini sababu ya kurejea kwenu?

Hivyo Hadhrat Ali[ra], Hadhrat Talha[ra], Hadhrat Zubair[ra] wakawauliza watu hao sababu ya kurejea kwao. Wote kwa kuafikiana wakatoa jibu hili kwamba: 'Sisi tulikuwa

tunarejea majumbani kwetu kwa amani na utulivu, mara tukamuona mtu fulani njiani aliyekuwa amepanda ngamia wa sadaka, ambaye wakati fulani alikuwa akija mbele yetu na wakati mwingine akirudi nyuma. Baadhi ya watu wetu walipomuona wakapata shaka na kwenda kumkamata. Alipoulizwa kwamba je una barua yoyote? akakana na alipoulizwa kwamba anakwenda kwa shughuli gani akajibu, 'Sijui'. Hapo watu hao wakazidi kuwa na shaka naye. Hatimaye wakamsachi na kumkuta na barua iliyoandikwa na Hadhrat Uthman[ra], na humo mtawala wa Misri alipewa maagizo kwamba wakati waasi watakaporudi Misri, miongoni mwao uwaue fulani na fulani, na uwacharaze fulani na fulani viboko na kuwanyoa nywele na ndevu zao, na ile barua niliyoandika kupitia hao kuhusiana na kustaafishwa kwako uifahamu kuwa ni batili. Tulipoiona barua hiyo tukashangazwa mno na tukarejea mara moja. Hadhrat Ali[ra] aliposikia jambo hili mara moja akawaambia: 'Jambo hili limebuniwa hapa Madina, kwa sababu, enyi watu wa Kufa na enyi watu wa Basra! Mlijuaje kwamba watu wa Misri wameikamata barua ya aina hiyo ilhali mlikuwa kwenye umbali wa siku kadha nyinyi kwa nyini? Halafu ilikuwaje pia nyie mkarejea kwa haraka namna hii?' Watu hao hawakuweza kutoa jibu la shutuma hiyo, wala hiyo haikuwa na jibu lolote. Hivyo, wakatoa jibu hili hili kwamba: 'Sema chochote ukipendacho na kutufikiria utakavyo, sisi hatuupendi

Ukhalifa wa mtu huyu. Ajiuzulu cheo chake. Muhammad bin Maslamah[ra] aliyekuwa ni miongoni mwa masahaba[ra] maarufu, na aliyekuwa anatokana na Maansar na ambaye, kwa amri ya Mtume[saw], alimuua Kaab bin Ashraf, aliyekuwa adui mkubwa wa Mtume[saw] na wa Islam, ambaye Wayahudi walikuwa wakimchukulia kama Mfalme, baada ya shari zake kuvuka mpaka na kuwa hana kikomo katika kuwasumbua Waislamu, na hivyo kuifanyia Islam huduma kubwa, yeye alipolisikia tukio hili akawarudi papo hapo na kuwaambia kinagaubaga kwamba huu ni uongo tu mliouzua.

## Hadhrat Uthman[ra] Kuwathibitishia Waasi kujitoa Katika Shutuma yao

Ingawa masahaba[ra] waliyapinga kiakili maneno yao haya, lakini ujasiri wa watu hao sasa ukawa umepita kiasi. Juu ya dhila ile iliyowafikia wao wakalipeleka suala hili mbele ya Hadhrat Uthman[ra] na wakamtaka atoe jibu lake. Wakati huo masahaba[ra] wengi maarufu pia walikuwa wameketi katika kikao chake. Yeye akawajibu kwamba 'Kulingana na sheria ya Kiislamu kuna njia mbili tu za uamuzi wa jambo lolote lile: Ama mwenye kushitaki atoe mashahidi wawili katika kuthibitisha madai yake au mshitakiwa alishwe kiapo. Hivyo mnalazimika mtoe mashahidi wawili katika kuyathibitisha madai yenu au la mimi naapa kwa Mwenyezi Mungu Yule Ambaye hakuna mwabudiwa

yeyote minghairi Yake kwamba mimi sijaiandika barua hii wala barua hii haijaandikwa kutokana na ushauri wangu wala sikuiandikisha wala sijui ni nani aliyeiandika barua hii.' Kisha akasema: 'Nyinyi mwaelewa kwamba wakati mwingine barua za bandia pia zatengenezwa na pete zingine huweza kutengenezwa zifananazo.' Masahaba[ra] walipolisikia jibu lake hili basi wakamsadikisha Hadhrat Uthman[ra] na kumsema hana hatia ya shutuma hii. Lakini hilo halikuwaathiri watu hawa hata kidogo. Jambo hili lingewaathiri vipi wakati wao wenyewe ndio walioitengeneza barua hiyo. Mtu anaweza kumuamsha mtu aliyelala, lakini nani awezaye kumuamsha yule aliye macho na kujisingizia kuwa amelala? Viongozi wa watu hao walikuwa wanafahamu fika kwamba huu ni udanganyifu wetu wenyewe. Wangepata wapi muda wa kutafakari busara na usahihi wa majibu hayo na wafuasi wao walikuwa wameshakuwa watumwa wao. Walikuwa wakisikiliza chochote walichokuwa wakikisema na walikuwa wakikubali chochote walichokuwa wakikieleza.

## Uhakika wa Njama ya Waasi

Watu hawa walikuwa ni watu wasioweza kuathirika na chochote wala hawakuathirika, lakini kwa wenye macho jibu la Hadhrat Uthman[ra] limejaa sifa njema za soni kiasi hiki kwamba kwa jibu hilo ukosefu wa haya na uovu wa waasi hao unabainika zaidi, wakati ambapo waasi hao baada ya kughushi barua ya bandia, wanamzulia

Hadhrat Uthman[ra] shutuma za ulaghai na udanganyifu, ilhali Hadhrat Ali[ra] na Hadhrat Muhammad bin Maslama[ra], kutokana na matokeo ya matukio, wanawashutumu watu hawa kwa shutuma za udanganyifu ulio wazi. Hadhrat Uthman[ra] mwenyewe aliyeshutumiwa na kufanyiwa njama hizi anajitakasa na shutuma hizo, lakini yeye hasemi kwamba nyinyi mmeitengeneza barua hii, bali anawasitiria pia kosa lao na kusema kiasi hiki tu kwamba: Nyinyi mwafahamu kuwa mwandiko, wafanana na mwandiko mwingine, na pete ya bandia huweza kutengenezwa na ngamia pia anaweza kuibwa.

Baadhi ya watu ambao wanamfahamu Hadhrat Uthman[ra] kutokuwa na hatia ya shutuma hiyo na wanataka kuwa na dhana nzuri pia kuhusiana na watu hao wanadhani ya kwamba Marwan mwenyewe ndiye aliyeighushi barua hii na kuituma. Lakini kwa rai yangu, wazo hili si sahihi hata kidogo. Matukio yanaeleza kwa uwazi kabisa kwamba barua hii ilitengenezwa na waasi hao hao, sio na Marwan wala na mtu mwingine yeyote. Na dhana hii kwamba kama wao (waasi) wangekuwa ndio walioighushi, basi walimpataje mtumwa wa Hadhrat Uthman[ra] na ngamia wa sadaka? Na wao waliutengenezaje mwandiko wa mwandishi wa Hadhrat Uthman[ra]? Na muhuri wa pete ya Hadhrat Uthman[ra] ulipigwaje juu yake? Wazo hili ni potofu. Kwa sababu

tunazo sababu zake za kutosha kwamba barua hii ilitengenezwa na watu hao hao, ingawa inaonekana kutokana na matukio, na hii ndio yaelekea kuwa sahihi zaidi, kwamba udanganyifu huu ulikuwa ni wa viongozi wachache, na hakuna cha kushangaza kwamba ingeweza kuwa ni kazi ya Abdullah bin Saba pekee na wanafunzi wake wachache makhsus, na watu wengine, hata kama walikuwa ni viongozi wa jeshi, pengine walikuwa hawana habari.

## Dalili Saba za Kuthibitisha Njama ya Barua

Uthibitisho wa jambo hili kwamba njama hii ilifanywa na baadhi ya watu miongoni mwa watu hawa ni huu:

Imeshathibitika hapo awali kuhusiana na watu hawa kwamba kwa ajili ya kupata matashi yao walikuwa hawajiepushi na kusema uongo, kama vile walivyotumia uongo dhidi ya Walid bin 'Utba na Said bin Al-'Aas. Halikadhalika walieneza mashitaka ya uongo dhidi ya tawala mbali mbali ambayo masahaba[ra] mashuhuri walifanya uchunguzi wake na kukuta kuwa si sahihi. Hivyo, wakati imeshathibitika kuhusiana na watu hawa kwamba hawakujiepusha na kusema uongo, hivyo hakuna sababu yoyote ya kutosema kuwa hawana hatia na kuwatuhumu watu ambao hawajathibitika kuwa waongo.

Kama vile Hadhrat Ali[ra] na Hadhrat Muhammad bin Maslama[ra] walivyolaumu kwamba kurudi haraka kwa namna hii kwa watu hawa na kuiingia kwao Madina kwa wakati mmoja, inatoa ushahidi wa jambo hili kwamba hii ilikuwa ni njama. Kwa sababu kama inavyothibitka toka kwenye historia, watu wa Misri walikuwa wakisema kwamba walimkamata yule mjumbe katika eneo la Buwaib, ambaye kutokana na maelezo yao, alikuwa akipeleka barua ya Hadhrat Uthman[ra] kwa mtawala wa Misri. Kutoka Madina hadi Buwaib kuna, kwa akali, vituo sita — umbali wa safari ya siku sita — na iko kwenye sehemu ile inakoanzia njia ya kwenda Misri. Wakati watu wa Misri walipokuwa wamefika hadi katika sehemu hii, basi watu wa Kufa na pia watu wa Basra wangekuwa wameshapita takriban vituo sita kuelekea maeneo yao na kwa namna hii chochote kilichotokea kwa watu wa Misri taarifa yake ingewafikia misafara hiyo miwili kwa angalau siku kumi na mbili au kumi na tatu, na baada ya kujumuisha siku za kuondoka na kurudi kwao, watu hawa wangeweza kufika Madina kwa takriban siku ishirini na nne. Lakini watu hawa wakarejea baada ya kitambo kidogo sana. Hivyo inathibitika kwa uwazi kabisa kwamba kabla hata hawajaondoka Madina, watu hawa walikuwa wameshapanga mpango kwamba mnamo tarehe fulani misafara yote irudi Madina na kuiteka mara moja Madina. Na kwa kuwa msafara wa Misri ulikuwa pamoja

na Abdullah bin Sabaa, naye alikuwa ni mtu mwerevu mno, yeye, kwa upande mmoja, aliona hivi kwamba watu watamuuliza kuwa: kwa nini umerudi bila ya sababu? na upande wa pili alikuwa na wazo hili kwamba jambo hili litakuwa linagonga hata ndani ya mioyo ya wenzake kwamba kwa nini ahadi imevunjwa baada ya uamuzi? Ndio sababu akatengeneza barua ya bandia na kuweka pazia juu ya akili za wenzake na kuuchochea zaidi moto wa hasira na ghadhabu ndani ya mioyo yao, na halikuwa jambo gumu kumuiba ngamia wa sadaka na kumhonga mtumwa yeyote yule na kushirikiana naye.

Tukio lenyewe la kukamatwa kwa barua hii, kama linavyoelezwa, pia lilikuwa kinyume na kawaida, kwa sababu kama Hadhrat Uthman[ra] au Marwan wangetuma barua ya aina hii, sasa ingewezekanaje kwamba mtumwa yule mara awe anakuja mbele yao na wakati mwingine awe akijificha. Harakati hii anaweza tu kuifanya mtu yule anayetaka kujikamatisha. Mtumwa yule, kwa kauli ya watu hao, aliamriwa afike Misri kabla ya msafara huo. Halafu kwenye eneo la Buwaib palipo lango la Misri, linawezaje kuingia akilini wazo la kwenda kwake pamoja nao. Kuna tofauti kubwa sana kati ya safari ya msafara na ile ya mtu mmoja. Msafara hauwezi kusafiri kuitumia kasi ile awezayo kuitumia mtu mmoja, kwa sababu mahitajio ya msafara huwa ni mengi sana na wanyama wote wa msafara huwa hawana kasi za kufanana. Hivyo

iliwezekanaje kwamba msafara ufike hadi Buwaib na mjumbe yule bado awe tu na msafara, wakati huo alipaswa awe ameshakaribia alikokuwa akielekea. Hali ile waielezayo ya mjumbe huyu, hiyo inaweza kunasibishwa na jasusi, lakini haiwezi kunasibishwa na mjumbe. Halikadhalika mjumbe huyo alipokamatwa, maswali na majibu yaliyotokea hayakuwa na uhalisia hata kidogo, kwa sababu yeye anasema kwamba yeye ni mjumbe, lakini hakuwa amepewa barua yoyote wala hakupewa ujumbe wowote wa maneno. Ni nani awezaye kutoa jibu hili minghairi ya mwehu au yule anayetaka watu wamtilie shaka. Kama kweli mtu huyo angekuwa ni mjumbe, sasa alikuwa na haja gani ya kusema kuwa mimi nimetumwa na Hadhrat Uthman[ra] au na mtu mwingine? Haiwezi pia kusemwa kwamba yeye alikuwa ameshikamana hasa na ukweli, kwa sababu inasemwa kwamba yeye alikuwa na barua, lakini yeye akasema kwamba sina barua yoyote. Hivyo, kulingana na maelezo ya watu hawa, mjumbe huyo, bila shaka, alisema uongo. Hivyo, swali ni hili kwamba kwa nini alisema uongo ambao ulimfanya agundulike kwa urahisi? Kwa nini hakusema uongo ule ambao ungeweza kumfanya asigundulike katika hali kama hiyo. Kwa uchache, matukio yote hayo yanaonyesha kwamba tukio la barua na lile la kupeleka barua lilikuwa ni la uongo tangu mwanzo hadi mwisho. Mmoja miongoni mwa waasi hawa hawa, (anayeshukiwa zaidi ni Abdullah

bin Sabaa), alibuni barua ya bandia na kumpa mtu fulani ili aichukue na kujipitisha karibu na msafara. Lakini si jambo lenye kuingia akilini kwamba msafiri akamatwe katika njia inayopitwa sana na watu. Na yule aliyeibuni barua alikuwa akitaka kwamba kadiri iwezekanavyo, tukio hili litimizwe kwa mkono wa mtu mwingine, ndio sababu akamuagiza mpelekaji wa barua kuwa asafiri na msafara ule kwa namna ambayo shaka ipatikane mioyoni mwa watu, na watakapouliza maswali kuondoa shaka yao, basi utoe majibu yatakayozidisha shaka ili watu wenyewe waanze kumsachi na baada ya kumuona nayo barua wawe na yakini kuwa Hadhrat Uthman[ra] amewadanganya.

Madhumuni ya barua hiyo pia yanadhihirisha kwamba barua hiyo ni ya bandia na haikuwa imebuniwa na Mwislamu yeyote aliye mjuzi, kwa kuwa katika baadhi ya riwaya, madhumuni yake yameelezwa hivi kwamba ndevu za fulani na fulani zinyolewe, ilhali kunyoa ndevu kumekatazwa katika Islam. Na katika tawala za Kiislamu adhabu iliyoweza kutolewa ilikuwa ni ile ile tu inayoafikiana na Islam. Haikujuzu hata kidogo kwamba mtu yeyote alishwe nguruwe kama adhabu au anyweshwe pombe au anyolewe ndevu, kwa kuwa jambo hilo limekatazwa. Adhabu pekee zinazothibitika ndani ya Islam ni za kuua, kupiga, kutoza faini na kutenganishwa na jamii kwa njia ya kufukuzwa nchini

au kwa sura ya kifungo. Mbali ya hizo hakuna adhabu yoyote inayothibitika ndani ya Islam wala maimamu wa Waislamu hawajawahi kutoa adhabu ya aina hii na hata Hadhrat Uthman[ra] mwenyewe au magavana wake hawakuwahi kutoa adhabu ya namna hii. Hivyo adhabu ya aina hii kuwemo katika maandishi ndani ya barua hii ni ushahidi wa kutosha wa jambo hili kwamba barua hii ilibuniwa na mtu ambaye alikuwa hafahamu undani wa Islamu.

Matukio ya kabla ya barua hii pia yanalipinga jambo hili kwamba barua hii ilitoka kwa Hadhrat Uthman[ra] au kwa Katibu wake, kwa sababu riwaya zote zimeafikiana katika jambo hili kwamba Hadhrat Uthman[ra] alionyesha upole mno katika kuwaadhibu watu hawa. Kama angependa, basi wakati ule watu hawa walipokuja kwa mara ya kwanza, angewaua wakati huo huo. Kama aliwaachia wakati huo, basi walipokuja mara ya pili lazima angeweza kuwakamata viongozi wa waasi, kwa sababu wao walikuwa wameshafanya uasi wa wazi wazi na masahaba[ra] walikuwa wameshajiaandaa kupigana nao vita. Lakini wakati huo, baada ya kuwatendea kwa upole, kumuandikia barua mtawala wa Misri ya kuwaadhibu watu hao, lilikuwa ni wazo lisilokubalika na akili. Na pia haiwezi kusemwa hivi kwamba baada ya kuuona ulaini wa Hadhrat Uthman[ra], Marwan akaandika barua ya aina hii, kwa sababu Marwan alikuwa

akifahamu vyema jambo hili kwamba Hadhrat Uthman[ra] alikuwa ni mkali sana katika kusimamisha sheria. Hakuweza hata kwa dakika moja kuwazia moyoni mwake kwamba anaweza kusalimika na adhabu baada ya kuandika barua ya aina hiyo. Tena, kwa nini akaiandika tu kwa mtawala wa Misri? Kwa nini asingeandika barua za aina hiyo kwa watawala wa Basra na Kufa pia, ambazo kwazo uamuzi ungefanyika dhidi ya maadui wote kwa wakati mmoja. Kuandikwa barua hii kwa jina la mtawala wa Misri pekee inatoa dalili ya jambo hili kwamba, ndani ya misafara ya Kufa na Basra hakukuwepo mtu mwenye hila kama Abdullah bin Sabaa.

Kama isemwe hivi kwamba maagizo ya aina hii yalitolewa pia kwa watawala wa maeneo hayo mawili, lakini wapelekaji hawakukamatwa, basi jibu lake ni hili kwamba kama ingekuwa hivyo, basi jambo hilo lisingeweza kufichika, kwa sababu kama shutuma hii itolewe kwa Abdullah bin 'Aamir kwamba kwa kuwa kwake jamaa wa Hadhrat Uthman[ra] ndio sababu akanyamaza, basi Hadhrat Musa Ash'ari[ra] aliyekuwa miongoni mwa masahaba[ra] mashuhuri, na ambaye Kurani Tukufu yenyewe imemtaja kuwa ni mwenye imani kamili, na ambaye wakati huo alikuwa ndiye mtawala wa Kufa, asingekaa kimya hata kidogo na lazima angelifichua jambo hili. Basi, ukweli ni huu huu

kwamba barua hii ilikuwa ni ya bandia na mtu fulani miongoni mwa watu wa msafara wa Misri ndiye aliyeibuni. Na kwa kuwa, mbali na msafara wa Misri, hakukuwa na mtu yeyote, miongoni mwa watu wa misafara mingine, aliyekuwa na uwezo wa kufanya harakati za aina hii, wala katika kipindi hicho wasingeweza kuibwa ngamia wengi wa Baitul Mal wala watumwa wengi kiasi hicho wasingeweza kukamatwa, ndio sababu hazikubuniwa barua kwa majina ya watawala wa maeneo mengine.

Yule mtumwa anayedhihirishwa kuipeleka ile barua ndiye aliyeweza kutoa mwanga zaidi wa barua hii kuliko watu wote, lakini yastaajabisha kwamba ingawa Hadhrat Uthman[ra] aliomba apatiwe mashahidi, mtumwa huyo hakupelekwa wala hatajwi popote katika matukio ya baadae, hali inayodhihirisha kwamba kuhudhurishwa kwake kulikuwa kinyume na masilahi yao. Labda waliogopa kwamba angekuja mbele ya masahaba[ra] angedhihirisha ukweli wa mambo. Hivyo, kumficha pia ni uthibitisho wa jambo hili kwamba mbunifu wa barua hii lilikuwa ni kundi hilo hilo la waasi.

Uthibitisho madhubuti kabisa wa jambo hili kuwa ni watu hawa hawa walioibuni barua hii ni kwamba hii sio barua ya kwanza waliyoibuni, bali minghairi ya hiyo, katika kuchochea moto wa uasi huu huu, walibuni barua nyingine kadhaa. Hivyo kubuni barua hii haikuwa

vigumu kwao, wala katika uwepo wa tukio haiwezi kunasibishwa kwa mtu mwingine. Barua zile walizokuwa wakizibuni hapo awali zilikuwa ni kwa ajili ya kumpa jina baya Hadhrat Ali[ra], na humo mlikuwa na madhumuni ya aina hii hii kwamba: Enyi watu hamakisheni dhidi ya Hadhrat Uthman[ra]. Kupitia barua hizo watu walikuwa wakihamakishwa, nao, baada ya kuona Hadhrat Ali[ra] akisadikisha, wakawa wananasa ndani ya maneno ya Abdullah bin Sabaa. Lakini inaonekana kwamba kulikuwa na agizo la kuyaficha sana madhumuni ya barua hizo ili Hadhrat Ali[ra] asifahamu na kuwapinga. Na waanzilishi wa uasi walikuwa na sababu ya kiakili ya kutoa agizo la kuficha, yaani kama barua hizi zingedhihirika, basi Hadhrat Ali[ra] angeingia kwenye matatizo. Kwa njia hii watu walikuwa hawadhihirishi madhumuni ya barua hizo kwa ajili ya kumsitiri Hadhrat Ali[ra], na kwa sababu ya jambo hilo kuendelea kufichika, uongo wa waanzilishi wa uasi haukuweza kufichuka. Lakini hatimaye uongo huwa hauwezi kufichika kwa muda mrefu zaidi, hasa wakati mamia ya watu wanapokuwa wameambiwa. Barua iliyoandikwa kwa kutumia jina la Hadhrat Uthman[ra] ilikamatwa, na watu wa kawaida wa Kufa wakarudi kwa ghadhabu kubwa. Basi kundi moja miongoni mwao wakamuendea Hadhrat Ali[ra] na kumuomba msaada. Mara tu Hadhrat Ali[ra] alipolisikia tukio lote akawa ameshalifahamu kuwa ni la uongo, na kutokana na busara zake alizobarikiwa

na Mungu, udanganyifu wa watu wa Misri ukawa unamdhihirikia. Yeye akakataa moja kwa moja kwa kuwaambia: Mimi siwezi kushirikiana nanyi katika shughuli za aina hii. Wakati huo baadhi yao, kutokana na jadhba, hawakuweza kuwa waangalifu na wakasema bila ya kujizuia kwamba: Sasa kwa nini ulikuwa ukituandikia barua? Jambo hili lilikuwa ni la kumshangaza mno Hadhrat Ali[ra] Akalikana kabisa jambo hilo na kudhihirisha kutolifahamu na kusema: Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, mimi sijawahi kuandika barua yoyote kwenu. (Tabarii, J. 6, uk. 2965, chapa ya Beirut). Hapo hata watu hao wakashangaa sana, kwani kwa hakika, hata wao wenyewe walikuwa wamedanganywa na wakaanza kutazamana kwa mshangao na kuuliza: Je nyinyi mwadhihirisha hasira kwa ajili ya mtu huyu na kumpigania? Yaani mtu huyu ni mwoga kiasi hiki kwamba baada ya kufanya yote haya, anayakanusha ulipofika wakati. (Mungu Apishe mbali).

Inaonekana, kutokana na tukio hili, kwamba walikuwepo baadhi ya watu miongoni mwa watu hawa, waliokuwa na umahiri wa kutengeneza barua za bandia, na pia kwamba watu wa aina hiyo walikuwemo miongoni mwa watu wa Misri, kwa sababu barua zilizoandikwa kwa kutumia jina la Hadhrat Ali[ra] ziliweza kuandikwa tu kwa watu wa Misri waliokuwa wakidai

kumpenda Hadhrat Ali[ra], hivyo barua hii iliyokuwa ikinasibishwa na Hadhrat Uthman[ra] kukamatwa ndani ya msafara wa watu wa Misri, ni uthibitisho wa wazi wa jambo hili kwamba mwandishi wake hakuwa mtu yeyote wa Madina, bali alikuwa ni mtu wa msafara ule ule wa Misri.

Kwa kuwa tukio la barua ni la muhimu sana kwa watu wanaomshutumu Hadhrat Uthman[ra], ndio sababu nimebainisha uchunguzi wangu juu ya jambo hili kwa kina. Na ingawa tukio hili laweza kuelezwa kwa maelezo zaidi, lakini mimi nadhani kwamba chochote kilichoelezwa chatosha katika kuthibitisha jambo hili kwamba barua hii ilikuwa ni ya kubuniwa na ya bandia na kwamba waghushi wa barua hii walikuwa ni Abdullah bin Sabaa na wenzake, hakuwa Marwan wala mtu mwingine yeyote (shani ya Hadhrat Uthman[ra] iko juu sana kuweza kufanya mambo kama haya).

## Waasi Wawanyanyasa Watu wa Madina

Sasa narejea tena kwenye mlolongo wa matukio. Kutokana na kishindo cha barua hii ya bandia na kiburi cha kuiteka ghafla Madina, waasi hawa wakaanza manyanyaso makubwa sana. Upande mmoja walikuwa wakimshinikiza Hadhrat Uthman[ra] ajiuzulu ukhalifa, na upande wa pili walikuwa wakiwasumbua watu wa Madina wasijaribu kumsaidia Hadhrat Uthman[ra]. Watu wa Madina wakawa hawana uwezo kabisa. Askari wenye

silaha wapatao elfu mbili au elfu tatu hivi, walikuwa wamezifunga njia, njia panda na milango ya mji. Haikuwa rahisi kupambana nao. Lakini katika hali hii kwamba hawakuwa wakiwaruhusu hata watu wachache kujumuika, na ikawa haiwezekani kujumuika sehemu moja watu zaidi ya wawili au wanne, hata ikawa muhali kuwazia hata moyoni kupambana na jeshi la waasi. Na hata kama baadhi ya wakereketwa wenye kutawaliwa na jadhba zao wangejiandaa kwa vita, basi wasingepata matokeo yoyote mbali ya maangamio. Msikiti ulikuwa ni mahali ambapo watu waliweza kujumuika, lakini watu hawa, kwa uerevu mkubwa, wakawa pia wameshaandaa mpango wake, nao ni huu kwamba walikuwa wakienea kwenye msikiti wote kabla ya sala na kwa njia hii wakawatenganisha watu wa Madina wasiweze kufanya lolote.

## Nasaha za Hadhrat Uthman[ra] kwa Waasi

Juu ya kuwepo kwa fujo hizi na uasi, Hadhrat Uthman[ra] alikuwa akiendelea kwenda kusalisha msikitini na pia waasi hawa wakawa hawapingani naye juu ya jambo hili na wakawa hawamzuii kuongoza sala, kiasi ya kwamba hata baada ya waasi hawa kuiteka Madina, mnamo Ijumaa ya kwanza kabisa baada ya Hadhrat Uthman[ra] kumaliza sala ya Ijumaa, akawanasihi watu hawa na kusema: “Enyi maadui wa Islam! Mwogopeni Mwenyezi Mungu. Watu wote wa Madina wanalifahamu jambo hili

kuwa Mtume[saw] aliwalaanini, hivyo tubuni na zifuteni dhambi zenu kwa wema, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Hazifuti dhambi kwa kitu kingine chochote isipokuwa kwa wema." Hapo Muhammad bin Maslama Ansari[ra] akasimama na kusema: "Mimi nalisadikisha jambo hili." Waasi hawa wakahisi kwamba wenzao wana dhana mbaya dhidi ya Hadhrat Uthman[ra], lakini kama masahaba[ra] wakianza kumsadikisha (namna ile) na kundi lao likaja kufahamu kuwa Mtume[saw] alitoa bishara makhsus kuhusiana nao, basi huenda watu wakatengana nao. Hivyo, wakaanza kuzizuia harakati hizo na jambazi Hakim bin Jabalah ambaye nimeshamtaja hapo awali, akamkamata na kumkalisha chini kwa nguvu Muhammad bin Maslama[ra] aliyekuwa sahaba aliyemkurubia sana Mtume[saw] aliyekuwa amesimama kwa ajili ya kuusaidia Ukhalifa na sio kwa ajili ya kuibua fitina. Hapo, Zaid bin Thabit[ra], aliyekabidhiwa huduma yenye shani ya kukusanya Kurani Tukufu akasimama kusadikisha lakini mtu mwingine pia akamketisha.

## Waasi Wavunja Fimbo ya Mtume[saw]

Baada ya hapo mtu fulani wa kundi hili la watu wanaojidai kuipenda Islam, akamnyang'anya Hadhrat Uthman[ra] ile fimbo ambayo Mtume[saw] alikuwa akiiegemea wakati akitoa hotuba na pia Hadhrat Abu Bakr[ra] alifanya hivyo baada yake na pia Hadhrat Umar[ra]. Na hakutosheka na hapo, bali akaiweka kumbukumbu

hii iliyokuwa sababu ya maelfu ya baraka kwa ajili ya umati wa Islam, kwenye magoti yake na kuivunja. Sawa, walikuwa na chuki dhidi ya Hadhrat Uthman[ra], walikuwa na chuki dhidi ya Ukhalifa, lakini walikuwa wanadai kumpenda Mtume Mtukufu[saw], sasa walipataje ujasiri wa kuivunja kumbukumbu hii ya Mtume[saw] kwa utovu wa adabu wa aina hii. Leo Ulaya imefikia kwenye kilele cha juu kabisa cha Udaharia (kukana uwepo wa Mwenyezi Mungu), lakini hisia hii bado imebaki ndani yake ya kuheshimu kumbukumbu za watakatifu wake. Lakini watu hawa juu ya kudai kwao kuwa Waislamu, wakaivunja na kuitupa fimbo yenye baraka ya Mtume[saw]. Hii inaonyesha kwamba jadhba ya kuinusuru Islam ilikuwa ya kujionyesha tu, waila viongozi wa kundi hili walikuwa mbali na Islam jinsi walivyo leo maadui wakubwa wa Islam.

## Waasi Wapiga Changarawe Msikitini Mwa Mtume[saw] na Kumjeruhi Hadhrat Uthman[ra]

Hata baada ya kuivunja fimbo ya Mtume[saw], mioyo ya watu hawa bado haikutosheka nao ndani ya msikiti huu ambao msingi wake uliwekwa na Mtume Muhammad[saw] na ujenzi wake ulifanywa na mikono mitakatifu kabisa, wakaanza kuvurumisha mvua ya changarawe na kuwatoa nje ya msikiti wa Mtume[saw] masahaba[ra] na watu wa Madina kwa changarawe, na Hadhrat Uthman[ra] akavurumishiwa changarawe kiasi hiki kwamba akazirai

na kuanguka kutoka kwenye mimbari na watu wachache wakamnyanyua na kumpeleka nyumbani.

Huu ulikuwa ndio mfano wa 'upendo' ule waliokuwa nao watu hawa kwa ajili ya Islam na wale waliokuwa wakiitekeleza sheria ya Kiislamu, na hizo zilikuwa ndio zile 'khulka bora' walizotaka kuziendesha ndani ya ulimwengu wa Islam kwa kumuengua Hadhrat Uthman[ra] toka kwenye Ukhalifa. Baada ya tukio hili nani awezaye kusema kwamba lile kundi liliosimama dhidi ya Hadhrat Uthman[ra] lilikuwa na uhusiano wowote na masahaba[ra] au kwamba kutokana na baadhi ya utendaji wa Hadhrat Uthman[ra] wakalazimika kufanya njama, au kwamba sababu ya hasira yao ilikuwa ni kwa ajili ya kuuhami Uislamu. Vitendo vyao viovu vyatoa ushahidi wa kutosha wa jambo hili kwamba hawakuwa na uhusiano wowote na Islam wala hawakuwa na upendo wowote na dini na wala hawakuwa na huba yoyote kwa masahaba[ra]. Wao walikuwa wamejitayarisha kuharibu amani na utulivu wa nchi kwa ajili ya kutimiza makusudio yao ya siri na walikuwa wakijaribu kuitoboa ngome ya Islam.

## Masahaba[ra] Wawa Tayari Kupigana Vita na Waasi

Baada ya tukio hili lenye kutisha, masahaba[ra] na watu wa Madina wakafahamu kuwa, ndani ya mioyo ya watu hao

mmejaa bughudha zaidi ya kiasi hicho wanachokidhihirisha. Ingawa hawakuwa na uwezo wa kufanya chochote, lakini baadhi ya masahaba[ra] walioyaona mauti kuwa ni afadhali kuliko hali hiyo, wao wakawa tayari kwamba hata yatokee nini sisi lazima tutapigana nao vita. Watu wanne au watano kupambana na jeshi hili la watu elfu mbili au tatu, kwa mtazamo wa kidunia, ilionekana pengine huo ni wehu, lakini kwa wale watu waliotoa muhanga kila kitu kwa ajili ya Islam, kupigana kwa ajili ya kuihami hakikuonekana kuwa kitu kigumu. Masahaba[ra] wafuatao pia walikuwa ni miongoni mwa wale waliokuwa tayari kupigana katika vita hivyo: Saad bin Malik[ra], Hadhrat Abu Huraira[ra], Zaid bin Samit[ra], na Hadhrat Imam Hasan[ra]. Habari hizi zilipomfikia Hadhrat Uthman[ra], basi mara moja akawaagiza kwa kusema: Katu msipigane na watu hao na nendeni majumbani mwenu.

Bila shaka mapenzi aliyokuwa nayo Hadhrat Uthman[ra] kwa masahaba[ra] wa Mtume[saw] na kwa ukoo wa Mtume[saw] yalisitisha vita ile iliyokuwa itokee kati ya masahaba[ra] wachache waliojitolea nafsi zao na jeshi lile la waasi elfu mbili tatu hivi. Lakini kutokana na tukio hilo tunakuja kufahamu kwa uwazi kabisa kuwa ni hamaki gani iliyokuwa ikizalika ndani ya baadhi ya masahaba[ra] kutokana na ukorofi wa watu hao. Kwa sababu watu wachache kuwa tayari kupambana na jeshi hilo imara

kwawezekana kwa sura hii hii tu kwamba watu hao walikuwa wanaona kulitii jeshi hilo kulikuwa ni kubaya kuliko mauti. Kushiriki kwa Abu Huraira[ra] na Hadhrat Hasan[ra] katika kundi hilo ni jambo linalopaswa kutafakariwa hasa. Kwa sababu Abu Huraira[ra] hakuwa mtu wa kivita na kabla ya hapo hakuwahi kutoa huduma yoyote ile ya kijeshi. Halikadhalika Hadhrat Imam Hasan[ra], mwana wa shujaa naye pia akiwa ni shujaa na jasiri, lakini yeye alikuwa akipenda sana suluhu na amani na kulingana na bishara fulani ya Mtume[saw] yeye alikuwa ni mwanamfalme wa amani (Mustadrak ul-Haakim, juzu 3, kitab Ma'rifatus Sahaba, bab Ikhbarin Nabiyyi biannal Hasana yuslahu bihi baina fiataini minal Muslimiina). Wakati huo watu wawili hawa kushika upanga mkononi na kusimama kunatoa dalili kwamba masahaba[ra] na watu wengine wa Madina walikuwa wamechukizwa mno na fujo za waasi hawa.

## Wenzi Wakubwa Watatu wa Waasi Ndani ya Madina

Kulikuwa na watu watatu tu katika wenyeji wa Madina waliokuwa pamoja na watu hawa. Mmoja alikuwa ni Muhammad bin Abi Bakr aliyekuwa mtoto wa Hadhrat Abu Bakr[ra] na wanahistoria wanadhani kwamba kutokana na sababu hii kwamba watu walikuwa wakimheshimu kwa sababu ya baba yake, hivyo akaanza kujidhani kwamba mimi pia nina hadhi, waila hakuwa

na fadhila ya kidunia wala hakuwahi kuishi pamoja na Mtume[saw] wala baadae hakufanya jitihada makhsus ya kujifunza dini. Alizaliwa mnamo siku za Hajjatul Wadaa' (Hija ya mwisho ya Mtume[saw]) na wakati wa kufariki kwa Mtume[saw] yeye alikuwa bado ni mtoto anayenyonya. Alikuwa na miaka minne tu wakati Hadhrat Abu Bakr[ra] alipofariki, na pia hakupata fursa ya kufaidika na malezi ya mtu huyo asiye na kifani.

(Tahdhiibut Tahdhiib, J. 9, uk. 70, Chapa ya Lahore).

Mtu wa pili alikuwa ni Muhammad bin Abi Hudhaifa. Huyu pia hakuwa miongoni mwa masahaba[ra]. Baba yake alikufa shahidi katika vita vya Yamama. Na Hadhrat Uthman[ra] akabeba jukumu la kumlea na akawa amemlea tangu utotoni. Wakati Hadhrat Uthman[ra] alipokuwa Khalifa, basi akaomba apewe cheo fulani. Hadhrat Uthman[ra] akakataa, hapo akaomba ruhusa kwamba: Nitoke nje nikafanye kazi yoyote. Akampa ruhusa naye akaenda Misri. Baada ya kwenda huko akajumuika na wenzi wa Abdullah bin Sabaa na kuanza kuwahamakisha watu dhidi ya Hadhrat Uthman[ra]. Wakati watu wa Misri walipokuja kuishambulia Madina yeye akaja pamoja nao, lakini baada ya umbali kidogo akarejea na hakuwepo Madina katika wakati wa fitina hii. (Tabarii, J. 6, uk. 3029, Chapa ya Beirut).

Mtu wa tatu alikuwa ni 'Ammaar bin Yasir, huyu alikuwa ni miongoni mwa masahaba[ra] na sababu ya

kudanganyika kwake ni kwamba alikuwa hajui siasa. Wakati Hadhrat Uthman[ra] alipomtuma Misri kwamba atoe taarifa kuhusiana na utendaji wa mtawala wa huko, basi Abdullah bin Sabaa akampokea na kuingiza mawazoni mwake upinzani dhidi ya mtawala wa Misri na kwa kuwa Gavana huyo alikuwa anatokana na watu waliompinga sana Mtume[saw] katika siku za ukafiri na alisilimu baada ya ushindi wa Makka, hivyo yeye akanaswa na watu hao kwa haraka sana. Baada ya kutia dhana mbaya dhidi ya mtawala, pole pole wakamfanya awe na dhana mbaya dhidi ya Hadhrat Uthman[ra]. Lakini, kwa vitendo hakushiriki hata kidogo kwenye uasi, kwa sababu ingawa alikuwepo Madina wakati Madina ikishambuliwa, alibakia kimya nyumbani mwake na hakushiriki kwa namna yoyote katika kukabiliana na waasi hao. Kwa vitendo hakushiriki hata kidogo katika uasi na mwenendo wake ulikuwa umeepukana kabisa na vitendo vibaya vya watu hawa.

## Hadhrat Uthman[ra] Alazimishwa Kujiuzulu Ukhalifa

Minghairi ya watatu hawa, hakukuwepo mtu yeyote mwingine miongoni mwa watu wa Madina, awe sahaba au asiwe sahaba, aliyeafikiana na waasi hao. Kila mtu alikuwa akiwalaani, lakini wakati huo walikuwa wameshika mamlaka yote. Walikuwa hawajali lawama ya mtu yeyote. Kwa siku ishirini watu hawa walikuwa wakijaribu kwa maneno tu kwamba kwa hali yoyote ile

Hadhrat Uthman[ra] aenguliwe kwenye Ukhalifa, lakini Hadhrat Uthman[ra] akalikataa kabisa jambo hili na akasema: Siwezi kulivua shati alilonivisha Mwenyezi Mungu wala siwezi kuuacha umati wa Muhammad[saw] bila mlinzi kwamba yeyote atakaye amdhulumu mwingine. (Tabarii, J. 6, uk. 2990, chapa ya Beirut). Akawa akiwafahamisha watu hawa kwamba wajiepushe na uasi huu na akawa akisema: Leo watu hawa wanafanya uasi na wanakerwa na uhai wangu, lakini wakati mimi nitakapokuwa sipo basi watatamani kwamba laiti siku moja ya umri wa Uthman ingekuwa sawa na mwaka mzima na asingetengana nasi mapema, kwa sababu baada yangu kutakuwa na umwagaji mkubwa wa damu na haki zitanyang'anywa na nidhamu itaharibika. (Basi, katika zama za Banu Umayya, Ukhalifa ukageuka na kuwa utawala na waasi hao wakapata adhabu kiasi hiki kwamba wakausahau ukorofi wote).

## Kuzingirwa kwa Nyumba ya Hadhrat Uthman[ra]

Baada ya kupita siku ishirini watu hawa wakafikiri kwamba sasa uamuzi ni lazima ufanyike kwa haraka ili isije ikatokea kwamba majeshi yaje kutoka mikoani na tuadhibiwe kutokana na matendo yetu, kwa hiyo wakamzuia Hadhrat Uthman[ra] asitoke nyumbani kwake na kuzuia vitu vya kula na kunywa visiingie nyumbani

mwake na kudhani kwamba labda kwa njia hii Hadhrat Uthman[ra] atalazimika kuyakubali madai yetu.

Sasa mamlaka ya Madina yalikuwa mikononi mwa watu hawa na majeshi yote matatu yakaungana na kumkubali Kiongozi wa jeshi la Misri, Ghaafiki, kuwa kiongozi wao. Hivyo, Mtawala wa Madina wa wakati huo akawa kama ndiye Ghaafiki; Kiongozi wa jeshi la Kufa Ashtar na Kiongozi wa jeshi la Basra Hakiim bin Jabalah (ndiye yule yule jambazi ambaye kutokana na kuiba mali za watu walio ndani ya himaya ya serikali, Hadhrat Uthman[ra] akaagiza azuiliwe nyumbani huko Basra), wote wawili wakawa wanafanya kazi chini ya uongozi wa Ghaafiki. Na kutokana na hii jambo hili likathibitika kwa mara nyingine kwamba mzizi hasa wa fitina hii ulikuwa ni watu wa Misri alipokuwa akifanya kazi Abdullah bin Sabaa. Ghaafiki akawa anasalisha katika msikiti wa Mtume[saw] na masahaba[ra] wa Mtume[saw] wakawa wamefungiwa majumbani mwao au wakawa wanalazimika kusali nyuma yake.

Wakati watu hawa walipokuwa hawajaamua kuizingira nyumba ya Hadhrat Uthman[ra], wakawa hawawasumbui sana watu, lakini walipoizingira tu wakaanza kuwasumbua watu wengine. Sasa Madina, badala ya kuwa nyumba ya amani, ikawa mahali pa vita. Heshima na hadhi ya watu wa Madina ikawa hatarini na

hakukuwa na mtu aliyetoka nyumbani bila ya silaha na yeyote aliyepambana nao walikuwa wakimuua.

## Hadhrat Ali[ra] Awanasihi Wazingiraji

Watu hawa walipomzingira Hadhrat Uthman[ra] na kuzuia hata maji yasiingie ndani basi Hadhrat Uthman[ra] akamtuma mtoto fulani wa jirani yake kwa Hadhrat Ali[ra] na Hadhrat Talha masahaba[ra] na kwa Hadhrat Zubair[ra] na kwa wake wa Mtume[saw] kwamba watu hawa wametuzuilia hata maji yetu, kama mwaweza kufanya chochote basi jaribuni kutufikishia maji. Miongoni mwa wanaume, kwanza kabisa alikuja Hadhrat Ali[ra] na kuwafahamisha watu hawa kwa kuwaambia: Hivi mwafanya kitu gani? Kitendo chenu hakifanani na cha waaminio wala na cha makafiri. Msizuie vyakula na vinywaji kwenda nyumbani kwa Hadhrat Uthman[ra]. Hata watu wa Roma na wa Uajemi wanawapa maji na chakula wafungwa wao na kitendo chenu hiki, kulingana na sheria ya Kiislamu, hakijuzu kwa namna yoyote ile. Kwani Hadhrat Uthman[ra] amewakosea nini kiasi ya kwamba muone inajuzu kumfunga na kumuua. Nasaha hii ya Hadhrat Ali[ra] haikutoa athari yoyote kwao. Wakasema kwa uwazi kabisa kwamba hata itokee nini hatutaruhusu maji wala chakula kufika kwa mtu huyu. Hili ndio lile jibu walilompa mtu yule ambaye walikuwa wakimsema kuwa ni *wasiyy* na mrithi wa kweli wa Mtume[saw] Na je! baada ya jibu hili kuna haja ya ushahidi

mwingine wowote wa kulithibitisha jambo hili kwamba kundi hili linalodai kuwa Hadhrat Ali[ra] ni *wasiyy*, halikutoka majumbani mwao kwa ajili ya kuihami haki na kwa ajili ya mapenzi ya watu wa ukoo wa Mtume[saw], bali kwa ajili ya kutimiza matamanio ya nafsi zao.

## Waasi Walivyomtendea Hadhrat Ummi Habiba[ra]

Miongoni mwa wake wa Mtume[saw] kwanza kabisa alifika Hadhrat Ummi Habiba[ra] kwa ajili ya kumsaidia. Alikuwa amempanda nyumbu. Alikuwa pia ameleta kiriba cha maji, lakini kusudio lake hasa lilikuwa hili kwamba Hadhrat Uthman[ra] alikuwa na wasia wa mayatima na wajane wa Banu Umayya. Yeye alipoona kwamba waasi wameyafungia maji ya Hadhrat Uthman[ra] basi akahofia kwamba wasia ule usije nao ukapotea, naye alitaka kwamba kwa namna yoyote wasia huo uhifadhiwe, waila angeweza kumfikishia maji kwa njia nyingine yoyote. Alipofika mlangoni kwa Hadhrat Uthman[ra], waasi wakataka kumzuia. Watu wakawaambia kuwa huyu ni mama wa waaminio, Ummi Habiba lakini juu ya hayo watu hao hawakujali na wakaanza kumpiga nyumbu wake. Ummul Mu'miniin, Ummi Habiba[ra] akasema: 'Nahofia kwamba wasia wa mayatima na wajane wa Banu Umayya usije kupotea, hivyo nataka kuingia ndani ili nifanye mpango wa kuuhifadhi. Lakini watu hawa wenye bahati mbaya wakamjibu mke mtakatifu wa Mtume[saw]: 'Unasema uongo,' na kwa kumshambulia

nyumbu wake, wakazikata kamba za tandiko la nyumbu wake na tandiko likapinduka na ilikaribia Hadhrat Ummi Habiba[ra] aanguke na kufa shahidi kwa kukanyagwakanyagwa na waasi hao. Lakini baadhi ya watu wa Madina waliokuwa karibu wakawahi kumuokoa na kumfikisha nyumbani.

(Tabarii, J. 6, uk. 3010, chapa ya Beirut)

## Mfano wa Ghera ya Kidini wa Hadhrat Ummi Habiba[ra]

Hivi ndivyo watu wale walivyomtendea mke mtakatifu wa Mtume[saw]. Hadhrat Ummi Habiba[ra] alikuwa na mapenzi na uaminifu kwa Mtume[saw] kiasi hiki kwamba baada ya kupita miaka 15-16 hivi ya kutengana, baba yake aliyekuwa kiongozi wa Waarabu na katika Makka alikuwa akiheshimika kama mfalme, alipokuja Madina kwa shughuli makhsus ya kisiasa na akaenda kumuona (binti yake huyo), basi bibi huyo akaliondoa tandiko la Mtume[saw] alilokuwa amelikalia (baba yake huyo) kwa sababu hii kwamba ilikuwa nje ya uwezo wake wa kuvumilia kuona mwili ulionajisika wa mshirikina ukigusana na nguo iliyotakasika ya Mtume[saw]. Yastaajabisha kwamba Hadhrat Ummi Habiba[ra] alizingatia utakatifu wa nguo ya Mtume[saw] hata wakati Mtume[saw] mwenyewe akiwa hayupo, lakini waasi hawa hawakujali utakatifu wa mke mtakatifu wa Mtume[saw], wakati Mtume mwenyewe akiwa hayupo. Wajinga

wakasema kwamba mke wa Mtume[saw] ni mwongo, ilhali chochote alichokisema kilikuwa ni sahihi. Hadhrat Uthman[ra] alikuwa msimamizi wa mayatima wa Banu Umayya na baada ya kuuona uadui uliokuwa ukizidi wa watu hawa basi hofu yake ilikuwa ni sahihi kwamba mali za mayatima na wajane zisipotee. Waongo walikuwa ni wale waliodai kumpenda Mtume[saw] na huku wakibeba dhima ya kuiangamiza dini yake, sio Ummul Muuminiin, Ummi Habiba[ra]. (Tabarii, J. 6, uk. 3029, Chapa ya Beirut).

## Hadhrat Aisha[ra] Ajitayarisha Kwenda Kuhiji

Habari za yale aliyotendewa Hadhrat Ummi Habiba[ra] zilipoenea Madina, masahaba[ra] na watu wa Madina wakapigwa butwaa na wakafahamu kwamba sasa kuweka tumaini lolote la kheri kwa watu hawa ni bure. Wakati huo huo Hadhrat Aisha[ra] akafunga nia ya kwenda kuhiji na akaanza matayarisho ya safari. Watu walipofahamu kwamba alikuwa anakaribia kuondoka Madina basi baadhi wakamuomba kwamba kama ubakie hapa hapa basi pengine waweza kupatikana msaada wa kusitisha fitina na waasi wakapata athari fulani. Lakini akakataa na kusema: Je mwataka nitendewe vile vile kama alivyotendewa Ummi Habiba[ra]? Kwa haki ya Mwenyezi Mungu mimi siwezi kuihatarisha heshima yangu (kwa sababu hiyo ilikuwa ni heshima ya Mtume[saw]). Kama mimi nitendewe chochote

nitalindwaje. Ni Mungu tu Ajuaye kuwa watu hawa wataendelea mpaka wapi katika uasi wao na nini itakuwa hatima yao.' Hadhrat Aisha Siddika[ra] alipokuwa akiondoka akafanya mpango fulani, ambao kama ungefanikiwa basi pengine uasi ungepungua kwa kiasi fulani, nao ni huu kwamba akamwambia ndugu yake, Muhammad bin Abu Bakr kwamba wewe pia twende pamoja kuhiji, lakini akakataa. Hapo Hadhrat Aisha[ra] akasema: 'Nifanye nini, sina uwezo. Kama ningekuwa na uwezo, ningewazuia watu hawa kufanikiwa katika dhamira zao.'

## Hadhrat Uthman[ra] Awaandikia Barua Watawala wa Mikoa

Hadhrat Aisha[ra] alienda kuhiji na pia baadhi ya masahaba[ra] walioweza kuondoka Madina wakaondoka na watu waliobakia, ukiacha masahaba[ra] maarufu wachache, wakawa wamekaa majumbani mwao na hatimaye Hadhrat Uthman[ra] pia akahisi kwamba watu hawa hawawezi kukubali kwa kutumia upole na akawaandikia barua moja watawala wote wa mikoa ambayo muhtasari wake ni huu:

Baada ya Hadhrat Abu Bakr[ra] na Hadhrat Umar[ra], bila ya kutamani wala kuomba, nilijumuishwa miongoni mwa wale watu waliopewa jukumu la kushauriana kuhusiana na Ukhalifa, halafu bila ya mie kutamani au kuomba nikachaguliwa kwa ajili ya Ukhalifa, nami

nimekuwa nikiifanya kazi ile ile waliyokuwa wakiifanya Makhalifa wa kabla yangu. Nami sikuanzisha bidaa yoyote, lakini ndani ya mioyo ya watu wachache imepandwa mbegu ya uovu na shari imeibuka na wakaanza kufanya njama dhidi yangu na wakadhihirisha jambo fulani mbele ya watu na mioyoni wakaweka jingine. Na wakaanza kunitolea lawama ambazo zilitolewa pia kwa Makhalifa wa kabla yangu. Lakini mimi, juu ya kufahamu hayo, nikanyamaza kimya na watu hawa wakajifaidisha visivyo na huruma yangu na kuzidi katika maasi. Na mwishowe, kama makafiri, wakaishambulia Madina. Hivyo kama mnaweza kufanya chochote basi fanyeni mpango wa kutoa msaada. Hali kadhalika barua nyingine ambayo muhtasari wa madhumuni yake ni kama yafuatayo akawaandikia waliokuja kuhiji na kuituma baada ya siku chache.

## Barua ya Hadhrat Uthman[ra] kwa Mahujaji

Mimi ninakuelekezeni kwa Mwenyezi Mungu na kukukumbusheni neema zake. Wakati huu kuna baadhi ya watu wanaeneza fitina na wanajishughulisha katika kujaribu kuleta mfarakano ndani ya Islam. Lakini watu hao hata hawakulifikiria hili kwamba ni Mungu Anayemteua Khalifa kama vile Asemavyo: وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِیۡنَ اٰمَنُوۡا مِنۡکُمۡ وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَیَسۡتَخۡلِفَنَّہُمۡ فِی الۡاَرۡضِ[13] (An-Nuur, 24:56), na

[13] Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini kati yenu na kufanya vitendo vizuri kuwa Atawafanya Makhalifa katika Ardhi.

wala hawakuuthamini umoja ilhali Mwenyezi Mungu Ameagiza: وَ اعْتَصِمُوْا بِحَبْلِ اللّٰهِ جَمِيْعًا[14] (Aali Imran, 3:104). Na wakayakubali maneno ya wale wanaonilaumu na hawakulijali agizo hili la Kurani Tukufu: يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِنْ جَآءَكُمْ فَاسِقٌۢ بِنَبَاٍ فَتَبَيَّنُوْۤا[15] (Al-Hujuraat, 49:7) na hawakuifanyia adabu baiat yangu ilhali Mwenyezi Mungu Anasema kuhusiana na Mtume[saw] kwamba [16] اِنَّ الَّذِيْنَ يُبَايِعُوْنَكَ اِنَّمَا يُبَايِعُوْنَ اللّٰهَ (Al-Fat'h, 48:11) nami ni naibu wa Mtume[saw]. Hakuna umati wowote uwezao kupata maendeleo bila ya kuwa na kiongozi, na kama hakuna Imamu yeyote basi shughuli yote ya Jumuiya itaharibika na kuangamia. Watu hawa wanataka kuuangamiza umati wa Kiislamu na hawana kusudio lolote lingine mbali na hilo, kwa sababu mimi nililikubali jambo lao na nikatoa ahadi ya kuwabadili watawala, lakini hata juu ya hayo, watu hao hawakuacha ukorofi. Sasa kati ya mambo haya matatu wao wanalitaka moja wapo: Kwanza ni kwamba wale watu wote waliopata adhabu katika zama zangu kisasi chao kilipwe kwangu na kama sikubaliani na hayo basi niuache Ukhalifa na watu hao wamteue mtu mwingine yeyote mahali pangu. Kama nisipokubaliana hata na haya basi watu hawa wanatishia kwamba

[14] Shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote.

[15] Enyi mlioamini, kama akikujieni fasiki na habari yoyote basi ipelelezeni.

[16] Hakika wale wanaofanya Baiat yako hao wanafanya Baiat ya Mwenyezi Mungu.

watawatumia ujumbe watu wote wanaoafikiana nao kwamba watoke nje ya utii wangu. Jibu la jambo la kwanza ni hili kwamba kabla yangu pia Makhalifa walikuwa wakati mwingine wakifanya makosa katika maamuzi, lakini hawakuadhibiwa hata kidogo, na maana ya kunipangia adhabu za kiasi hiki zinaweza kuwa nini minghairi ya kutaka kuniua?

Jibu litokalo kwangu kuhusiana na kujiuzulu Ukhalifa ni hili kwamba kama watu hawa wanikate vipande vipande kwa koleo basi nitakuwa radhi lakini siwezi kutengana na Ukhalifa.

Likawa limebakia jambo la tatu kwamba watu hawa watawatuma watu wao sehemu zote (kushawishi) ili asitokee yeyote wa kuyakubali maneno yangu. Hivyo, mimi sio mwenye kuwajibika kwa Mwenyezi Mungu, kama watu hawa wanataka kutenda jambo fulani kinyume na sheria basi na wafanye. Hata mwanzoni walipofanya baiat yangu mimi sikuwalazimisha. Yule mtu anayetaka kuvunja ahadi, mimi siridhii kitendo chake hiki wala Mwenyezi Mungu Haridhii; naam afanye apendavyo."

Kwa kuwa siku za Hija zilikuwa zinakaribia na watu walikuwa wakijumuika Makka toka pande zote, Hadhrat Uthman[ra] kwa kuwazia hivi kwamba isije huko pia kukaibuka fujo ya aina fulani na kwa kuwazia hivi pia kwamba zifanyike harakati kwa Waislamu waliojumuika

kwa ajili ya Hija kuwasaidia watu wa Madina, akamfanya Abdullah bin Abbas[ra] kuwa kiongozi wa Hija na kumsafirisha. Hadhrat Abdullah bin Abbas[ra] alisema: Mimi napendelea zaidi kufanya jihadi dhidi ya watu hawa, lakini Hadhrat Uthman[ra] akamlazimisha kwa kumwambia aende kuhiji na katika siku za Hija afanye kazi kama Kiongozi wa Hija ili waasi wasiweze kueneza shari zao huko na zifanywe harakati kwa wale watu waliojumuika huko za kuwasaidia watu wa Madina na akamtuma nayo hiyo barua iliyotajwa juu. Waasi walipofahamu juu ya barua hizo wakaanza kuzidisha mateso na wakawa wanaitafuta fursa ya jambo hili kwamba namna gani wapate kisingizio chochote cha kuanzisha vita na kumuua Hadhrat Uthman[ra], lakini juhudi zao zote zikawa za bure na Hadhrat Uthman[ra] akawa hawapi fursa yoyote ya kupata kisingizio cha kufanyia ukorofi.

## Waasi Watupa Mawe Ndani ya Nyumba ya Hadhrat Uthman[ra]

Hatimaye wakachoka kusubiri na kupanga njama hii kwamba usiku uingiapo na watu wakiwa wamelala, hao wakawa wanatupa mawe ndani ya nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] na kwa njia hii wakawa wanawahamakisha watu wa nyumbani ili wapande mori na wao watupe mawe ili waweze kuwaambia watu kuwa wao ndio walioanza kutushambulia ndipo tukalazimika kujibu

mapigo. Lakini Hadhrat Uthman[ra] akawakataza watu wote wa nyumbani mwake kujibu mapigo. Siku moja alipopata fursa alikuja karibu na ukuta na kusema: Enyi watu! Kwa rai yenu mimi ni mtu niliyekutendeeni dhambi lakini watu wengine walifanya kosa gani? Mnapopiga mawe hata watu wengine wanakuwa katika hatari ya kujeruhiwa. Wakakataa katakata kwa kusema: 'Sisi hatukupiga mawe,' Hadhrat Uthman[ra] akasema: "Kama nyinyi sio mnaopiga nani basi anayepiga?" Wakasema: 'Pengine Mwenyezi Mungu Ndiye Anayepiga.' (Mungu Apishe mbali). Hadhrat Uthman[ra] akasema: "Nyinyi mwasema uongo, kama Mwenyezi Mungu Angetupiga mawe basi jiwe hata moja lisingetukosa, lakini mawe mliyoyapiga nyinyi yanaangukia pia hapa na pale." Baada ya kusema hayo akaondoka mbele yao.

## Juhudi Nzuri za Masahaba[ra] za Kuiondoa Fitina

Ingawa masahaba[ra] hawakupewa fursa ya kukusanyika kwa Hadhrat Uthman[ra], lakini hata hivyo hawakughafilika na jukumu lao. Katika wakati uliofaa walizigawanya shughuli zao katika sehemu mbili. Waliokuwa wazee na ambao athari za khulka zao zilihimili sana kwa watu, wao walikuwa wakiutumia wakati wao kuwanasihi watu, na wale ambao hawakuwa na athari yoyote kwa watu au vijana, wao

walijishughulisha katika kujaribu kumlinda Hadhrat Uthman[ra].

Miongoni mwa waliokuwa katika kundi lililotajwa mwanzo walikuwa ni Hadhrat Ali[ra] na Hadhrat Saad bin Waqqaas[ra] , mshindi wa Faaris, walikuwa mstari wa mbele kabisa katika kuzipunguza fitina. Hasa Hadhrat Ali[ra] katika siku hizo za fitina aliacha kazi zake zote na kujikita katika kazi hiyo. Hivyo, miongoni mwa mashahidi wa kujionea kwa macho wa matukio hayo, alikuwa ni mtu fulani aitwaye jina Abdur Rahman anayesimulia kwamba: 'Katika siku hizo za fitina nilimuona Hadhrat Ali[ra] ameachana na kazi zake zote na kuwazia usiku na mchana katika kuzipoza hasira za maadui wa Hadhrat Uthman[ra] na katika kumuondolea shida (Hadhrat Uthman[ra]). Wakati fulani maji yalichelewa kumfikia, yeye akamkasirikia sana Hadhrat Talha[ra] aliyekuwa amekabidhiwa jukumu hili, na hakupumzika hadi maji yalipoingia nyumbani mwa Hadhrat Uthman[ra].

Kundi la pili, mmoja mmoja, wawili wawili, walipopata fursa kwa kuitafuta, wakaanza kujikusanya ndani ya nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] au ndani ya nyumba za majirani zake na wakaweka dhamira madhubuti ya jambo hili kwamba sisi tutayatoa maisha yetu lakini hatutaruhusu chochote kiufikie uhai wa Hadhrat Uthman[ra]. Katika kundi hili mbali ya watoto wa Hadhrat

Ali[ra], Hadhrat Talha[ra] na Hadhrat Zubair[ra] walishiriki pia kundi la baadhi ya masahaba[ra]. Watu hawa walikuwa wakiilinda nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] usiku na mchana na hawakumruhusu adui yeyote kumfikia. Na ingawa idadi hii ndogo isingeweza kukabiliana na jeshi lenye askari wengi kiasi hicho, lakini kwa kuwa waasi walikuwa wanataka waweke kisingizio chochote na kumuua Hadhrat Uthman[ra], hivyo hawakushinikiza sana (kukabiliana nao). Kutokana na hali za wakati huo akili inashangaa kwa mwanga unaopatikana wa jinsi Hadhrat Uthman[ra] alivyoitakia mema Islam. Jeshi la karibu watu elfu tatu liko mbele ya mlango wake na hakuna njia yoyote ya kujiokoa nalo. Lakini wale watu wanaotaka kujitahidi kumuokoa, hao pia anawazuia akiwaambia ondokeni msihatarishe maisha yenu, kwani watu hawa wana uadui na mimi tu, hawana upinzani wowote na nyinyi. Jicho lake lilikuwa likiutazama ule wakati ambapo Islam itakuwa kwenye hatari kubwa mikononi mwa waasi hao. Na sio tu umoja wa kidhahiri, bali hata nidhamu ya kiroho itakaribia kuchafuka na alikuwa akifahamu kwamba wakati huo kila sahaba atakuwa akihitajika kwa ajili ya kuilinda na kuisimamisha Islam.

Hivyo yeye hakuwa akitaka kwamba uhai wa masahaba[ra] upotee kwa ajili ya juhudi isiyo na faida ya kumuokoa, na kila mmoja alikuwa akimpa nasaha hii hii kwamba msipingane na watu hao, na alikuwa akitaka kwamba

kadiri iwezekanavyo kwa ajili ya kuzizuia fitina za siku zijazo, kundi lile lisalimike lililokaa na Mtume[saw]. Lakini juu ya yeye kuwafahamisha, wale masahaba[ra] waliopata fursa ya kufika nyumbani kwake, walikuwa hawalegei katika kuyatekeleza majukumu yao, na walikuwa wakitoa kipaumbele kwa hatari zilizopo juu ya zile zitakazokuja baadae. Na kama uhai wao ulikuwa umesalimika kwa wakati huo, basi ni kwa sababu hii tu kwamba watu wale (waasi) walikuwa hawaoni haja ya kuharakisha (kutekeleza malengo yao) na walikuwa wakitafuta kisingizio. Lakini hatimae ukaja pia ule wakati ambapo ikawa haiwezekani kusubiri zaidi, kwa sababu ule ujumbe wa Hadhrat Uthman[ra] wenye kutikisa moyo alioutuma kwa Waislamu waliojumuika kwa ajili ya Hija, ulikuwa umesomwa kwenye mjumuiko wa Mahujaji na sauti yake ikawa inavuma kutoka upande mmoja wa bonde la Makka hadi mwingine. Na Waislamu waliojumuika katika Hija wakaamua kwamba baada ya Hija hawatazikosa pia thawabu za (kupigana vita ya) Jihadi na watahakikisha wanawatokomeza kabisa waasi wa Misri na wenzao. Majasusi wa waasi wakawapasha habari za uamuzi huu na kukawa na athari kubwa ya hofu katika kambi yao kiasi ya kwamba kukawa na minong'ono miongoni mwao kwamba sasa hakuna njia yoyote ile minghairi ya kumuua mtu huyu (Hadhrat Uthman[ra]), na kama hatutamuua basi hakuna shaka yoyote ya kuuawa kwetu na Waislamu.

Habari hii ikaizidisha zaidi hofu hiyo kwamba barua za Hadhrat Uthman[ra] zimeshafika hadi Siria, Kufa na Basra, na watu wa huko, ambao tangu mwanzo walikuwa wanasubiri maagizo ya Hadhrat Uthman[ra], walihamaki zaidi baada ya kuwasili kwa barua hizo, na masahaba, kwa kuyaelewa majukumu yao, wametoa fatuwa ya kupigana Jihadi dhidi ya waasi hao katika misikiti na vikao mbali mbali kwa kuwakumbusha Waislamu majukumu yao na kusema kwamba yule ambaye hakufanya jihadi leo basi ni kama hajafanya chochote. Huko Kufa 'Uqbah bin Amr[ra], Abdullah bin Abi Aufa[ra] na Handhala bin Rabii' At-Tamimi[ra] na masahaba[ra] wengine watukufu wakawahamasisha watu kuwasaidia watu wa Madina. Na huko Basra Imran bin Husain[ra], Anas bin Malik[ra], Hashim bin 'Aamir[ra] na masahaba[ra] wengine wakafanya hivyo. Huko Siria, 'Ubada bin Saamit[ra], Abu Umama[ra][17] na masahaba[ra] wengine wakawahamasisha watu waiitikie sauti ya Hadhrat Uthman[ra], na huko Misri Khaarija na watu

[17] Kulingana na riwaya ya Tabarii, Hadhrat Abu Dardaa Answari[ra] alikuwemo miongoni mwa masahaba[ra] waliokuwa wakihamasisha watu kumsaidia Hadhrat Uthman[ra] huko Siria. Lakini kulingana na riwaya nyingine inaonekana huyu alikuwa ameshafariki kabla ya kuuawa shahidi kwa Hadhrat Uthman[ra] kama inavyothibitika ndani ya vitabu vya Isti'aab na Isaba, na hii habari ndio sahihi. Lakini kama vile ilivyokwisha elezwa hapo awali yeye pia alikuwa akijitahidi katika uhai wake kuiondoa fitina hii.

wengine pia wakafanya hivyo. Na baada ya kukusanyika majeshi kutoka nchi zote, wakawa wanakuja Madina.

(Tabarii, J. 6, uk. 2960, chapa ya Beirut)

## Waasi Waishambulia Nyumba ya Hadhrat Uthman[ra]

Kwa uchache, hofu ya waasi ikaongezeka zaidi baada ya kupata habari hizi. Hatimaye wakataka kuishambulia nyumba ya Hadhrat Uthman[ra] na kuingia ndani kwa nguvu. Masahaba[ra] wakapambana nao, na vita kali ikatokea kati yao. Ingawa masahaba[ra] walikuwa wachache lakini ghera yao ya imani ilikuwa inafidia uchache wa idadi yao. Sehemu hiyo iliyopiganwa vita, yaani mbele ya nyumba ya Hadhrat Uthman[ra], sehemu hiyo ilikuwa finyu na kwa sababu hiyo waasi wakashindwa kunufaika zaidi na wingi wao. Hadhrat Uthman[ra] alipopata taarifa ya vita hii, akawakataza masahaba[ra] kupigana. Lakini wao waliona ni kinyume na uaminifu na ni kinyume na amri ya utii kwamba wamuache pekee Hadhrat Uthman[ra] wakati huo. Na juu ya Hadhrat Uthman[ra] kuwakataza kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu, wao wakakataa kurudi nyuma.

## Hadhrat Uthman[ra] Awausia Masahaba[ra]

Mwishowe Hadhrat Uthman[ra] akashika ngao mkononi na kutoka nje na kuwaingiza masahaba[ra] nyumbani mwake na kuamuru milango yote ifungwe na kuwausia

masahaba[ra] wote na wasaidizi wao kwamba: "Mwenyezi Mungu Hakukupeni dunia ili muiinamie, bali Amekupeni kwa sababu hii kwamba mkusanye kwayo masurufu ya Akhera. Hii dunia itatoweka na ni Akhera tu ndiyo itakayobakia. Hivyo, msighafilishwe na kitu chenye kutoweka. Toeni kipaumbele kwa kitu chenye kubakia juu ya kile chenye kutoweka, na mkumbuke kukutana kwenu na Mwenyezi Mungu, na msiruhusu Jumuiya isambaratike, na msiisahau neema ile ya Mwenyezi Mungu kwamba mlikuwa karibu kuangukia ndani ya shimo la maangamio na Mwenyezi Mungu, kwa Fadhili Zake, Akawaokoa na kuwafanya ndugu." Baada ya hapo akawaruhusu wote waondoke na kusema: "Mwenyezi Mungu Awe Mlinzi na Msaidizi wenu. Nyote sasa tokeni nje ya nyumba na pia muwaite wale masahaba[ra] waliozuiwa kunifikia, hasa Hadhrat Ali[ra], Hadhrat Talha[ra] na Hadhrat Zubair[ra]."

Watu hao wakatoka nje na masahaba[ra] wengine pia wakaitwa. Wakati huo kulikuwa na hali fulani iliyokuwa imezalika na kulikuwa na huzuni fulani iliyokuwa imeenea kiasi ya kwamba hata waasi nao ikawaathiri. Na kwa nini isingekuwa hivyo, wote walikuwa wakiona kwamba mshumaa uliowashwa na Mtume[saw], baada ya kutimiza muda wake duniani ukawa unatoweka machoni mwa watu wa dunia hii. Kwa uchache, waasi hawakuingilia kati, na masahaba[ra] wote wakajumuika.

Watu walipojumuika yeye (Hadhrat Uthman[ra]) akapanda juu ya ukuta wa nyumba yake na kusema: "Sogeeni karibu yangu." Wote waliposogea, akasema: "Enyi watu, kaeni chini." Hapo masahaba[ra] wakakaa chini, na waasi nao kwa kuathirika na haiba ya kikao wakaketi. Wote walipokwisha kaa chini basi akasema: "Watu wa Madina! Mimi nakukabidhini kwa Mwenyezi Mungu na kumuomba dua hii kwamba Akufanyieni mpango bora wa Ukhalifa baada yangu. Baada ya leo hadi wakati ule Mwenyezi Mungu Atakapotoa uamuzi juu yangu sitatoka nje wala sitampa yeyote yule mamlaka yale ambayo kwayo akutawaleni katika dini na dunia. Na jambo hili nitamuachia Mwenyezi Mungu kwamba Amchague yeyote Amtakaye kwa ajili ya kazi yake." Baada ya hapo akawaapisha masahaba[ra] na watu wengine wa Madina kwamba wasiyaingize maisha yao kwenye hatari kubwa kwa kumlinda yeye na waende majumbani mwao.

Kukatokea tofauti kubwa miongoni mwa masahaba[ra] kutokana na agizo lake hili, hitilafu ambayo hauonekani mfano wake hapo kabla. Masahaba[ra] hawakujua chochote isipokuwa kutii amri. Lakini leo katika kuitii amri hii, baadhi yao wakaona kwamba huo hautakuwa utii bali ni usaliti. Baadhi ya masahaba[ra] wakitoa kipaumbele kwenye upande wa utii wakaachana na dhamira ya kukabiliana tena na maadui na labda

wakafahamu kuwa kazi yetu ni kutii tu, sio kazi yetu kutazama kuwa kutakuwa na matokeo gani kutekeleza amri hii, lakini baadhi ya masahaba[ra] wakakataa kuitii amri hiyo, kwa sababu waliona kwamba bila shaka kumtii Khalifa ni faradhi, lakini kama Khalifa atoe agizo hili kwamba niacheni mimi na mwende zenu maana yake inakuwa hii kwamba msishikamane na Ukhalifa, basi kwa hakika utii huu unazaa usaliti. Na pia walikuwa wakiona hivi kwamba Hadhrat Uthman[ra] kuwarudisha kwao majumbani ilikuwa ni kwa kuyalinda maisha yao, sasa wao wangewezaje kwenda majumbani mwao na kumuacha mtu mwenye upendo kiasi hicho katika hatari. Masahaba[ra] wote maarufu walikuwemo ndani ya kundi hili lililotajwa mwishoni. Hivyo, juu ya kuwepo amri hii, watoto wa Hadhrat Ali[ra], Hadhrat Talha[ra] na Hadhrat Zubair[ra], chini ya agizo la baba zao, wakaweka ulinzi kwenye mlango wa Hadhrat Uthman[ra] huku panga zao zikiwa nje ya ala.

## Kurejea kwa Mahujaji Kwawatia Hofu Waasi

Hofu na jadhba ya waasi ikawa haina mipaka wakati miongoni mwa wale watu waliomaliza Hija walipokuwa wakirudi mmoja mmoja na wawili wawili na kuanza kuingia Madina na wakafahamu kwamba sasa wakati wa uamuzi wa hatima yetu umekaribia sana. Hivyo Mughira bin Al-Akhnas akawa mtu wa kwanza kabisa aliyeingia Madina kwa ajili ya kuzipata thawabu ya jihadi, na

pamoja na hayo waasi wakapata habari kwamba jeshi la watu wa Basra linalokuja kuwasaidia Waislamu limeshafika eneo la *Ṣiraār* lililopo mwendo wa siku moja toka Madina. Kwa kuathirika na habari hizi wakaamua kwamba kwa namna yoyote ile ni lazima waitimize haraka dhamira yao. Na kwa kuwa wale masahaba[ra] na wenzao, ambao juu ya kukatazwa na Hadhrat Uthman[ra] hawakuacha kumlinda Hadhrat Uthman[ra] na wakasema wazi kwamba ikiwa tukutelekeze wakati mikono yetu ina nguvu za kupambana sasa tutamuonyesha uso gani Mwenyezi Mungu. Kutokana na uchache wa idadi yao sasa wakawa wanalinda sehemu ya ndani ya nyumba na hivyo ikawa si vigumu kwa waasi kufika hadi mlangoni. Wakakusanya malundo ya kuni na kuyachoma moto mbele ya mlango ili upate kuungua na kuipata njia ya kuingilia ndani. Masahaba[ra] walipoiona hali hii, wakaona si vizuri kukaa ndani. Wakishika panga wakataka kutoka nje, lakini Hadhrat Uthman[ra] akalikataza jambo hilo na kusema kwamba: "Baada ya kuichoma moto nyumba sasa ni jambo gani lililobakia? Sasa kilichokuwa kitokee kimeshatokea. Msiyahatarishe maisha yenu na nendeni majumbani mwenu. Watu hawa wana uadui tu na dhati yangu, lakini hivi karibuni watu hawa watajutia waliyoyatenda. Mimi namuondolea majukumu ya kunitii kila anayelazimika kunitii na ninaiachia haki yangu hiyo (Tabarii, J. 6, uk. 2002, chapa ya Beirut). Lakini masahaba[ra] na watu wengine hawakulikubali jambo hili

na wakachomoa panga zao na kutoka nje. Walipokuwa wakitoka Hadhrat Abu Huraira[ra] pia akaja, na ingawa yeye hakuwa mtu wa vita, naye pia akaungana nao na kusema: Ni vita gani inayoweza kuwa bora kuliko vita hii ya leo? Na halafu akatazama upande wa waasi na kusema: وَيٰقَوْمِ مَا لِيْٓ اَدْعُوْكُمْ اِلَى النَّجٰوةِ وَتَدْعُوْنَنِيْٓ اِلَى النَّارِ ؕ۝ yaani, Enyi watu wangu! Mimi nina nini, nawaiteni kwenye uokovu nanyi mwaniita kwenye moto. (Al Mu'min, 40:42)

## Masahaba[ra] Wapigana na Waasi

Vita hii ilikuwa ni vita makhsus. Na masahaba[ra] wachache walioweza kukusanyika wakati huo wakapambana kwa nguvu zote na jeshi hilo kubwa. Hadhrat Imam Hasan[ra] aliyekuwa ni mtu wa kupenda sana suluhu, bali alikuwa ni mwanamfalme wa amani, yeye pia katika siku hiyo aliwashambulia maadui huku akisoma mashairi ya vita. Beti za kivita zake na za Muhammad bin Talha[ra] siku hiyo zinafaa hasa kutajwa kwa sababu kutokana nazo taswira halisi ya mawazo yao ya moyoni yadhihirika wazi.

Hadhrat Imam Hasan[ra] alikuwa akiwashambulia waasi huku akisoma ubeti huu:

لَا دِيْنُهُمْ دِيْنِيْ وَلَا اَنَا مِنْهُمْ    حَتّٰى اَسِيْرَ اِلٰى طَمَارِ شَمَامِ

Yaani dini ya watu hawa sio dini yangu, wala sina uhusiano wowote na watu hawa, nami nitapigana nao hadi wakati ule nitakapofika kwenye kilele cha mlima

Shamami. (Tabarii, J. 6, uk. 3014, chapa ya Beirut). Shamam ni mlima fulani wa Uarabuni unaofananishwa na kufika kileleni na kuyafikia malengo. Na maana ya Hadhrat Hasan[ra] ni kwamba: Nitaendelea kupigana nao hadi nitakapopopata makusudio yangu na sitafanya nao suluhu, kwa sababu kati yetu hakuna tofauti ndogo hata kwamba tuwe na uhusiano nao bila ya kuwashinda. Hayo ndiyo mawazo yaliyofura ndani ya moyo wa mwanamfalme wa amani. Sasa twaligeukia ubeti wa kivita wa mtoto wa Talha, Muhammad. Yeye anasema:

اَنَا ابْنُ مَنْ حَامٰى عَلَيْهِ بِاُحُدٍ وَ رَدَّ اَحْزَابًا عَلٰى رَغْمِ مَعَدٍّ

Yaani, mimi ni mtoto wa yule aliyemlinda Mtume[saw] siku ya Uhud na kuwashinda Waarabu juu ya kwamba walitumia nguvu zote. Yaani hata hili la leo ni tukio kama la Uhud, na kama vile baba yangu alivyoikinga mishale kwa mkono wake na kuutobokesha lakini hakumfanya Mtume[saw] apate kudhurika, mimi pia nitafanya hivyo hivyo.

Hadhrat Abdullah bin Zubair[ra] pia alishiriki katika vita hivyo na kujeruhiwa vibaya. Marwan pia alijeruhiwa vibaya sana hadi akafikwa na mauti. Mughira bin Al Akhnas aliuawa. Yule mtu aliyemuua alipoona kwamba hakuwa amejeruhiwa bali amekufa, akasema kwa sauti ya juu: *Inna lillaahi wa inna ilaihi Rajiuun*. Mkuu wa kikosi akamkaripia kwa kumwambia: Waonyesha huzuni kwenye fursa hii ya furaha? Yule akasema: leo usiku

nimeona ndani ya ruya kwamba mtu fulani anasema: "Mpe habari za Jahanamu muuaji wa Mughira". Hivyo baada ya kufahamu kuwa mimi ndiye muuaji wake ni lazima nipate huzuni yake.

Mbali na watu hawa waliotajwa, walikuwepo pia watu wengine waliojeruhiwa na kuuawa, na kundi la kumhifadhi Hadhrat Uthman[ra] likazidi kupungua. Lakini ikiwa waasi, juu ya kuwepo maonyo ya kimbingu, hawakuacha upinzani wao, na kuendeleza mapambano dhidi ya kundi lenye kupendwa na Mwenyezi Mungu, basi upande mwingine waaminio nao hawakuonyesha upungufu wowote katika kuonyesha mfano wa imani wa daraja ya juu. Ingawa walinzi wengi waliuawa au kujeruhiwa lakini hata hivyo kikundi kidogo kiliendelea kuulinda mlango.

Kwa kuwa, kwa dhahiri, waasi walikuwa wameshapata ushindi, wao, kwa hila ya mwisho, wakamtuma mtu fulani kwa Hadhrat Uthman[ra] kwamba ajiuzulu Ukhalifa, kwa sababu walikuwa wakifahamu kuwa kama atajiuzulu mwenyewe basi Waislamu hawatakuwa na haki wala fursa ya kuwaadhibu. Yule mjumbe alipofika kwa Hadhrat Uthman[ra], basi Hadhrat Uthman[ra] akasema: "Mimi hata katika zama za ujahili (kabla ya kufika Islam) nilijiepusha na mabaya na hata ndani ya Islam sikuzivunja sheria zake. Kwa nini na kwa kosa gani nikiache cheo hiki alichonipa Mwenyezi Mungu?

Sitalivua kamwe shati hili alilonivisha Mwenyezi Mungu." Mtu huyo alirudi baada ya kulisikia jibu hilo na kuja kuwaambia wenzake maneno haya: "Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, tumenasa katika msiba mzito. Kwa haki ya Mwenyezi Mungu! bila ya kumuua Hadhrat Uthman[ra] hatuwezi kusalimika kukamatwa na Waislamu (kwa sababu kwa sura hii utawala utakuwa umepinduliwa na nidhamu itakuwa imeharibika na hakuna yeyote atakayeuliza) na kumuua hakujuzu kwa namna yoyote ile."

Kauli hizi za mtu huyu hazitoi tu dalili ya hofu waliyokuwa nayo watu hao, bali yatoa pia dalili ya jambo hili kwamba hata wakati huo, Hadhrat Uthman[ra] hakuwa ameruhusu jambo lolote litokee ambalo kwalo watu hawa wangeweza kulitumia kama kisingizio, na mioyo yao ilikuwa inahisi kwamba kumuua Hadhrat Uthman[ra] hakujuzu kwa sura yoyote ile.

## Abdullah Bin Salaam[ra] Awanasihi Waasi

Wakati watu hawa walipokuwa wakipanga njama za kumuua Hadhrat Uthman[ra], Hadhrat Abdullah[ra] bin Salaam, ambaye hata wakati alipokuwa kafiri (bado hajasilimu), alikuwa ni mtu mwenye kuheshimika sana kwa watu wake na ambaye Wayahudi walimkubali kuwa kiongozi wao na walikuwa wakimfahamu kuwa ni mwanazuoni asiye na kifani, alikuja na kusimama mlangoni na kuanza kuwanasihi watu hao na

kuwakataza kumuua Hadhrat Uthman[ra] kwa kuwaambia: "Enyi watu! Msiuchomoe upanga wa Mwenyezi Mungu juu yenu wenyewe. Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, kama mtauchomoa upanga huo, basi hamtapata tena fursa ya kuurudisha ndani ya ala. Daima vita na magomvi yataendelea miongoni mwa Waislamu. Tumieni akili, leo mnatawaliwa kwa bakora pekee (kwa kawaida adhabu za kisheria zilikuwa ni kuchapa bakora), na kama mkimuua mtu huyu basi kazi ya utawala haitafanyika bila ya upanga (yaani watu watakuwa wanauawa kwa makosa madogo madogo). Kumbukeni kwamba wakati huu walinzi wa Madina ni Malaika, kama mtamuua basi Malaika wataiacha Madina." Watu hawa wakatumia fursa ya nasaha hii kwa kumkatalia sahaba wa Mtume[saw], Abdullah[ra] bin Salaam, na kumkejeli kuhusiana na siku zake za awali kwa kumwambia: 'Ewe mwana wa mwanamke wa Kiyahudi, mambo haya yanakuhusu nini wewe?" Yasikitisha kwamba watu hawa walikumbuka tu hivi kuwa Abdullaha[ra] bin Salaam alikuwa ni mwana wa mwanamke wa Kiyahudi lakini wakasahau kuwa yeye aliposilimu, Mtume[saw] alidhihirisha furaha kubwa mno kwa kusilimu kwake, na alishiriki pamoja na Mtume[saw] katika kila hali ya msiba na shida; na vivyo hivyo wakawa pia wamesahau jambo hili kwamba Abdullah bin Sabaa, Kiongozi wao mwenye kuwapotosha kwa kumsema Hadhrat Ali[ra] kuwa ndiye mrithi wa Mtume[saw]

na kuwasimamisha dhidi ya Hadhrat Uthman[ra], naye pia alikuwa ni mwana wa mwanamke wa Kiyahudi bali mwenyewe alikuwa ni Myahudi na alikuwa tu akidhihirisha kuwa yeye ni Mwislamu.

## Waasi Wamuua Hadhrat Uthman[ra]

Hadhrat Abdullah[ra] bin Salaam akaondoka zake baada ya kukata tamaa juu ya watu hawa. Na upande mwingine baada ya kuona kwamba kumuua Hadhrat Uthman[ra] kupitia mlangoni ni vigumu kwa sababu wale watu wachache waliokuwepo upande ule kuzuia walikuwa ni watu waliokuwa wamejitolea kufa na kupona, wakaamua kwamba waruke ukuta wa jirani fulani na kwenda kumuua Hadhrat Uthman[ra]. Hivyo, kutokana na dhamira hii, waasi wachache wakaruka ukuta wa jirani fulani na kuvamia chumbani mwake. Walipoingia ndani Hadhrat Uthman[ra] alikuwa akisoma Kurani Tukufu na tangu alipozingirwa alikuwa usiku na mchana akijishughulisha na shughuli hii hii kwamba anasali au anasoma Kurani Tukufu na mbali na hayo hakuielekea shughuli nyingine yoyote. Katika siku hizo alifanya kazi moja tu nayo ni hii kwamba kabla ya waasi hao hawajazivamia nyumba, aliwateua watu wawili kwa ajili ya kuilinda Hazina, kwa sababu, kama ilivyothibitika, kwamba usiku wa kuamkia siku hiyo alimwona Mtume[saw] katika ruya na Mtume[saw] akamwambia: "Uthman! Jioni ya leo ufuturu pamoja

nasi." Kutokana na ndoto hii akawa amepata yakini kwamba mimi leo nitakufa shahidi. Hivyo, kwa kuyazingatia majukumu yake akawaagiza watu wawili kwamba wasimame kwenye mlango wa Hazina kulinda ili mtu yeyote asijaribu kuiibia Hazina wakati wa fujo.

## Matukio ya Kuuawa Shahidi kwa Hadhrat Uthman[ra]

Kwa uchache waasi hawa walipoingia ndani wakamkuta Hadhrat Uthman[ra] akisoma Kurani Tukufu. Miongoni mwa hao walioshambulia, alikuwemo pia Muhammad bin Abu Bakr, na kutokana na mamlaka aliyokuwa nayo juu ya watu hawa akafahamu kuwa ni faradhi kwake awe mbele mbele katika shughuli, hivyo akaenda mbele na kuzikamata ndevu za Hadhrat Uthman[ra] na akamsukuma kwa nguvu. Kutokana na kitendo chake hichi, Hadhrat Uthman[ra] akasema tu hivi kwamba: "Ewe mwana wa ndugu yangu, kama baba yako (Hadhrat Abu Bakr[ra]) angekuwepo wakati huu basi asingefanya hivi asilan. Umepatwa na nini? Wanikasirikia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Je mbali na haya una hasira yoyote kwangu kwamba nimekulazimisha kutoa haki za Mwenyezi Mungu?" Hapo Muhammad bin Abu Bakr akaona haya na kurudi nyuma lakini watu wengine wakabakia hapo hapo. Na kwa kuwa habari za yakini zilikuwa zimeshafika kwamba usiku huo jeshi la Basra litaingia Madina na fursa hiyo ilikuwa ni fursa ya

mwisho kwa ajili yao, watu hawa wakaamua kwamba hawatarejea bila ya kukamilisha kazi yao. Na mmoja wao akasogea mbele na kumpiga kichwani Hadhrat Uthman[ra] kwa nondo na halafu ile Kurani Tukufu iliyokuwepo mbele ya Hadhrat Uthman[ra] akaipiga teke na kuitupa. Kurani hiyo ikabingirika na kurejea kwa Hadhrat Uthman[ra] na matone ya damu yaliyokuwa yakitiririka toka kichwani mwake yakaangukia juu yake (Kurani). Ukiachilia mbali tukio la kuidhalilisha Kurani, lakini pazia la ucha Mungu na uaminifu wa watu hawa lilichanika kabisa kutokana na tukio hili.

Ile aya ambayo damu yake iliangukia, yenyewe ilikuwa ni utabiri mkubwa sana ambao ulitimia kwa shani kubwa katika wakati wake, kwamba hata mtu mwenye moyo mgumu kabisa alifumba macho yake kwa hofu, baada ya kuziona herufi zile zilizoangukiwa na damu. Aya yenyewe (iliyoangukiwa na damu) ni hii: فَسَيَكْفِيْكَهُمُ اللّٰهُ ۚ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ Ni lazima Mwenyezi Mungu Atakulipizia kisasi kwao na Mwenyezi Mungu ni mwenye Kusikia sana mwenye Kujua mno. (Al-Baqara, 2:138)

Baada ya hapo mtu mwingine aliyeitwa Saudaan akasogea mbele na kutaka kumshambulia kwa upanga. Pigo la kwanza akalizuia kwa mkono wake na mkono wake ukakatika. Hapo (Hadhrat Uthman[ra]) akasema: "Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, huo ndio ule mkono wa kwanza kuandika Kurani Tukufu." Baada ya hapo

akampiga dhoruba ya pili akitaka kumuua, mke wake (Hadhrat Uthman[ra]) Naila[ra], akaja na kujiweka katikati. Lakini mwenye bahati mbaya huyo hakusita kumpiga upanga hata mwanamke na akampiga, na kutokana na pigo hilo vidole vya mke wa Hadhrat Uthman[ra] vikakatika. Kisha akamshambulia tena Hadhrat Uthman[ra] na kumjeruhi vibaya sana. Baada ya hapo, mtu huyu mwenye bahati mbaya akawaza kuwa bado hajakata roho huyu, huenda akanusurika. Wakati huo huo alipokuwa ameshazimia kutokana na maumivu ya majeraha, akiwa na mitikiso kutokana na ukali wa maumivu, akamkamata shingo yake na kumkaba, na hakuiachia shingo yake hadi roho yake (Hadhrat Uthmanra) ilipoachana na mwili huu wa udongo ikiitikia mwaliko wa Mtume[saw] wa kwenda Akhera. Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Mwanzoni, mke wa Hadhrat Uthman[ra], kwa kuathirika na hofu iliyosababishwa na mandhari hayo, alishindwa kusema lakini hatimaye alipaza sauti na wale watu waliokuwa wamekaa mlangoni wakaja ndani mbio mbio. Lakini wakati huo msaada ulikuwa hauna faida, kilichokuwa kitokee kilishatokea. Mtumwa huru fulani aliyetolewa utumwani na Hadhrat Uthman[ra], alipouona ule upanga wenye damu mkononi mwa Saudan aliyemuua Hadhrat Uthman[ra], akashindwa kujizuia na akasogea mbele na kukikata kichwa cha mtu yule kwa

upanga. Hapo mtu fulani miongoni mwa waasi akamuua huyo. Sasa kiti cha enzi cha utawala wa Kiislamu kikawa hakina Khalifa. Watu wa Madina wakaona kuwa ni upuuzi sasa kuendelea na juhudi zao na hivyo kila mmoja akarudi nyumbani kwake. Waasi hao, baada ya kumuua Hadhrat Uthman[ra], wakaanza kuwadhalilisha watu wa nyumbani mwa Hadhrat Uthman[ra]. Mke wa Hadhrat Uthman[ra] aliondoka kuihama sehemu hiyo. Wakati akiondoka, maleuni mmoja miongoni mwa waasi hao akawaambia wenzake: Tazameni makalio yake yalivyo makubwa.

Bila shaka, kwa ajili ya mtu mwenye soni, awe mfuasi wa dini yoyote ile, inakuwa ni vigumu kwake hata kuliwazia jambo hili, kwamba katika wakati kama huo ambapo sahaba wa zamani wa Mtume[saw], mkwe wake, mfalme wa nchi zote za Kiislamu na halafu Khalifa wa zama, watu hawa wametoka kumuua sasa hivi, halafu wadhihirishe mawazo machafu ya aina hiyo. Lakini ukosefu wa haya wa watu hawa ukawa umezidi kiasi hiki kwamba hawakuwa mbali na kuweza hata kufanya kitendo chochote kiovu. Watu hawa hawakusimama kwa nia yoyote njema wala kundi lao halikuwa kundi la watu wema. Baadhi yao walikuwa ni wale waliodanganywa na Myahudi Abdullah bin Sabaa na kuwa wapenzi wa mafundisho yake ya ajabu ya kuipinga Islam. Baadhi yao walikuwa ni waliovutiwa kupita kiasi

na Usoshalisti na Ubolsheviki. Baadhi yao walikuwa ni wale wahalifu waliopata kuadhibiwa, waliokuwa wakitaka kulipiza kisasi chao cha siku nyingi. Wengine walikuwa ni wezi na majambazi waliokuwa wakiona njia ya mafanikio yao kupitia fitina hii. Hivyo ukosefu wao wa haya sio wa kushangaza, bali kama watu hao wasingefanya harakati hizo basi lingekuwa jambo la kustaajabisha.

Wakati watu hawa walipokuwa wakipora mali na kuua, mtumwa huru mwingine hakuweza kuvumilia kusikia vilio vya watu wa nyumbani mwa Hadhrat Uthman[ra], hivyo akamshambulia yule muasi aliyemuua mtumwa huru wa kwanza na kumuua. Hapo waasi hao wakamuua na yeye pia. Wakayavua mapambo ya akina mama na kutoka nje ya nyumba wakifanya dhihaka.

## Waasi Waipora Baitul Maal — Hazina

baada ya hapo waasi hawa wakawatangazia wenzao na kuwaambia waende Hazina na kupora kila kilichomo humo. Kwa kuwa ndani ya Hazina hamkuwa na chochote minghairi ya mifuko miwili ya rupia, waliokuwa wakiilinda, baada ya kuona kuwa Khalifa wa zama ameshafariki, na kupambana na watu hawa hakuna faida yoyote, wakaamua hivi kwamba wawaache wafanye wapendavyo na hivyo wakazitupa funguo za hazina na kuondoka zao. Kwa hiyo waasi wakaenda kuifungua Hazina na kuiba kila kilichokuwemo na kwa

namna hii wakawa wamepiga muhuri wa kudumu juu ya ukweli wa jambo hili kwamba watu hawa walikuwa ni wezi na majambazi na hawakuwa na uhusiano wowote ule na Islam wala Waislamu. Je hili si jambo la kushangaza kwamba watu wale waliokuwa wakimshutumu Hadhrat Uthman[ra] kwa shutuma hii kwamba alikuwa akiwapa fedha watu wasiostahiki, kitu cha kwanza walichokifanya baada ya kufariki kwa Hadhrat Uthman[ra] kikawa ni kupora mali za nyumba yake na halafu za Hazina. Lakini Mwenyezi Mungu Hakuruhusu kutimia kwa matamanio yao hata katika suala hili, kwa sababu ndani ya Hazina wakati huo hamkuwa na chochote minghairi ya rupia chache zisizoweza kutimiza tamaa yao.

## Masahaba[ra] Wahamaki kwa Kifo cha Hadhrat Uthman[ra]

Habari za kifo cha Hadhrat Uthman[ra] zilipowafikia masahaba[ra], wakapata uchungu mkubwa sana. Hadhrat Zubair[ra] alipopata habari akasema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Ewe Mwenyezi Mungu! Mrehemu Uthman[ra] na umlipizie kisasi." Alipoambiwa kuwa waasi hao sasa wanaona haya na kujutia waliyoyafanya, akasema: "Hizi zilikuwa ni njama." Halafu akaisoma aya hii: وَحِيْلَ بَيْنَهُمْ وَ بَيْنَ مَا يَشْتَهُوْنَ (Saba', 34:55), Mwenyezi Mungu Alikuwa Ametia kizuizi katika kutimia kwa matamanio yao. Yaani

chochote walichokitaka sasa kilionekana kutotimia, wakawa wanauona ulimwengu wote wa Kiislamu umehamaki dhidi yao, ndio sababu wanadhihirisha kujuta. Wakati Hadhrat Talha[ra] alipopata habari hii, naye pia akasema hivi hivi: "Mwenyezi Mungu Amrehemu Uthman[ra] na Alipe kisasi dhidi ya watu hawa kwa ajili ya Hadhrat Uthman[ra] na Islam" Alipoambiwa kuwa watu hao sasa wanajuta akasema: Waangamie hawa. Na akasoma aya hii tukufu: فَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ تَوْصِيَةً وَّ لَآ اِلٰٓى اَهْلِهِمْ يَرْجِعُوْنَ Hawatapata fursa ya kufanya wasia wala hawataweza kurejea kwa familia zao. (Yaa Siin, 36:51)

Vivyo hivyo, Hadhrat Ali[ra] alipopata taarifa akasema: "Mwenyezi Mungu Amrehemu Hadhrat Uthman[ra] na baada yake Amteue mrithi bora kwa ajili yetu. Naye pia alipoambiwa kuwa watu hao sasa wanaona haya, basi akaisoma aya hii: كَمَثَلِ الشَّيْطٰنِ اِذْ قَالَ لِلْاِنْسَانِ اكْفُرْ ۚ فَلَمَّا كَفَرَ قَالَ اِنِّيْ بَرِيْٓءٌ مِّنْكَ اِنِّيْٓ اَخَافُ اللّٰهَ رَبَّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۱۷﴾ Yaani mfano wao ni kama ule wa Shetani amwambiaye mtu: Kufuru. Na anapokufuru humwambia mimi sina uhusiano na wewe, mimi namuogopa Mwenyezi Mungu. (Al-Hashr, 59:17)

Yale majeshi yaliyokuwa yakija kwa ajili ya kumsaidia Hadhrat Uthman[ra] yalipotambua kuwa ameuawa, wakarejea watokako toka maili chache tu kutoka Madina, hawakupenda kwenda tena Madina, kwani wasingeweza kutoa msaada wowote kwa Hadhrat Uthman[ra] kwa kwenda kwao huko na kulikuwa na hatari

isije fujo kuongezeka. Na Waislamu, kwa kawaida, walikuwa hawapendi kupigana bila ya Imam.

Sasa Madina ikawa imebaki chini ya madaraka ya watu hawa hawa (waasi), na harakati walizozifanya watu hao ndani ya siku hizo ni za kushangaza mno. Walishamuua Hadhrat Uthman[ra] na wakawa hawataki hata maiti yake izikwe na hivyo kutoweza kuzikwa kwa siku tatu. Hatimae kundi moja la masahaba[ra] likafanya hima na kumzika nyakati za usiku. Hata watu hawa pia waliwawekea vizuizi, lakini baadhi ya watu hawa wakatishia kupambana nao kwa nguvu zote ndipo wakanywea. Waasi hao walizitoa nje ya nyumba maiti za watumwa huru wote wawili wa Hadhrat Uthman[ra] na kuzitupa porini na kuwalisha mbwa. (Tabarii, J. 6, uk. 3049, chapa ya Beirut). Twajikinga kwa Mwenyezi Mungu Atuepushe na hayo.

## Muhtasari na Matokeo ya Matukio Yaliyotajwa

Haya ndio yale matukio sahihi yaliyotokea katika siku za mwisho za Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra]. Baada ya kuyafahamu, hakuna mtu yeyote awezaye hata kudhani kwamba Hadhrat Uthman[ra] au masahaba[ra] walikuwa wanahusika chochote na fitina hizi. Hii ni hadhi yake ya pekee jinsi Hadhrat Uthman[ra] alivyofanya kazi kwa huba, ikhlasi na uvumilivu ndani ya miaka sita ya mwisho ya Ukhalifa wake. Mfano wa aina hiyo hauwezi kupatikana ndani ya jumuiya yoyote ile mbali na ile ya

waja watakatifu wa Mwenyezi Mungu. Alikalia kiti cha Ukhalifa katika hali ya kutojipendelea na katika hali hiyo hiyo ya kutojipendelea akarejea kwa Mola wake. Katika nyakati za hatari kiasi hicho ambapo hata damu za wenye subira kubwa zingechemka, yeye alichukua mwelekeo wa aina hii, kiasi ya kwamba hata wale waliokuwa na kiu ya damu yake, walishindwa kutafuta hata kisingizio dhaifu kabisa cha kumuulia na mwishowe wakalazimika kumnyanyulia upanga, wakikiri (kwa kitendo hicho) kuwa wao ni wadhalimu, na kutokuwa na kosa kwa Hadhrat Uthman[ra].

Halikadhalika yathibitika kwa uwazi kabisa kutokana na matukio hayo, kwamba masahaba[ra] hawakuwa na malalamiko yoyote dhidi ya Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra]. Wao hadi mwishoni walikuwa waaminifu, na hata wakati ilipokuwa haiwezekani kutoa msaada wa aina yoyote kwake, hata hapo walihatarisha maisha yao na kuendelea kumlinda. Pia yathibitika kutokana na matukio haya, kwamba katika fujo hizo hakukuwa na hisa yoyote ile iliyosababishwa na uteuzi wa watawala alioufanya Hadhrat Uthman[ra] wala si dhuluma za watawala hao zilizosababisha hayo, kwa sababu hakuna dhuluma yoyote inayothibitika kuwa waliitenda. Na hata shutuma za kwamba Hadhrat Ali[ra], Hadhrat Zubair[ra] na Hadhrat Talha[ra] walifanya njama za siri, zilikuwa si sahihi kabisa. Masahaba[ra] hao watatu walijaribu

kuiondoa fitina hiyo kwa uamnifu na kwa huruma ya namna hii kwamba sio tu hata ndugu wa damu hawezi kufanya zaidi ya hivyo, bali hata hawezi kufanya sawa na hivyo. Shutuma zinazotolewa dhidi ya Ma-Ansaar (watu wa Madina) kwamba walimkasirikia Hadhrat Uthman[ra] si sahihi, kwa sababu tunaona kwamba viongozi wote wa Ma-Ansaar walikuwa wakijitahidi katika kuiondoa fitina hii.

Sababu ya asili ya uasi ilikuwa hii hii kwamba maadui wa Islam walipoona kwamba Islam haiangamii kwa njama za dhahiri, wakageukia kwenye njama za siri na kwa kutumia majina ya baadhi ya masahaba[ra] maarufu, wakataka kuanzisha kwa siri mfarakano miongoni mwa Waislamu. Njia walizotumia sasa zimeshadhihirika kwa watu. Wakawashirikisha wale wahalifu waliowahi kuadhibiwa na kuwatia tamaa majambazi. Wakazua mawazo ya usawa bandia na kuudhoofisha mfumo wa utawala. Wakadhoofisha imani ya watu ndani ya pazia la dini na kuunda kundi fulani kwa hila na njama nyingi. Halafu kwa kutumia uongo, mbinu bandia na upotoshaji, wakatengeneza hali ambazo zikawawia vigumu Hadhrat Uthman[ra] na masahaba[ra] wengine kukabiliana nazo. Sisi hatujui hatima ingekuwaje, lakini twafahamu kutokana na matukio haya kwamba wakati huo, hata kama ungekuwepo ukhalifa wa Hadhrat Umar[ra], bado fitina hii lazima ingeibuka na lawama hiyo

hiyo aliyoshutumiwa nayo Hadhrat Uthman[ra] angeshutumiwa nayo pia Hadhrat Umar[ra], kwa sababu Hadhrat Uthman[ra] hakufanya kazi yoyote ile ambayo Hadhrat Umar[ra] na Hadhrat Abu Bakr[ra] hawakuifanya.

Kwa kuwa, kutokana na ufinyu wa wakati, matukio ya ukhalifa wa Hadhrat Ali[ra] yalielezwa kwa dakika chache na kwa muhtasari mno, ndio sababu wakati wa kuzirejea nimeiondoa sehemu hiyo.